# CHUO KIKUU CHA KENYATTA

# SHULE YA SAYANSI ZA KIJAMII

# IDARA YA KISWAHILI

## MIGOGORO YA KISAIKOLOJIA KATIKA RIWAYA ZA *MKAMANDUME* NA *UNAITWA NANI?*

**GEORGE OLUOCH SCOTT**

**NAMBARI YA USAJILI: C50/CE/28276/2015**

**TASNIFUHII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

**NOVEMBA 2020**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu chochote kingine kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

**GEORGE OLUOCH SCOTT NAMBARI YA USAJILI: C50/CE/28276/2015**

**SAHIHI** ………………………………………… **TAREHE** 05/11/2020

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

**PROF. GEOFFREY KITULA KING'EI**……………… **TAREHE** 6/11/2020

**(Msimamizi)**

**DKT. RICHARD MAKHANU WAFULA**……………… **TAREHE** 6/11/2020

**(Msimamizi)**

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mama yangu mpendwa Zipporah Adhiambo Scott kwa kunipa moyo wa kuendelea na masomo yangu hata nilipopata changamoto za hapa na pale. Wake zangu wapendwa Rose Auma Oluoch na Jemediah Nyaboke Oluoch. Wote wawili walinipa mazingira matulivu niliyohitaji kukamilisha kazi yangu. Vilevile sitawasahau wanangu Daina Anyango Oluoch, Levine Atieno Oluoch, Danwilliam Scott Oluoch na Shally Stacy Oluoch kwa uvumilivu wenu na kunitumainisha. Mungu awabariki na kuwapa maisha marefu kwa kuwa na moyo wa uvumilivu na uelewa.

# SHUKRANI

Kwanza ninachukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na nguvu za kutimiza malengo yangu. Hakuna jambo lolote ambalo lingetimia bila yeye kunileta umbali huu, kwa kunipa hekima, moyo wenye uvumilivu na matumaini tele hata katika changamoto nyingi zilizokumba utafiti wangu.

Pili, ninawashukuru sana wasimamizi wangu Prof. Geoffrey Kitula King'ei na Dkt. Richard Makhanu Wafula. Msaada walionipa, fikra, maarifa na miongozo ya kila namna ilinifaa sana kufikia kiwango hiki. Pia siwezi kusahau mwongozo na ushauri niliopewa na wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta. Wahadhiri hawa ni kama vile: Dkt. P. Ngugi, Dkt. Chacha, Dkt. Osore, Dkt. Onyango, na wengine wote. Mungu awape maisha marefu.

Vilevile, ninachukua nafasi hii kuwashukuru wake zangu; Rose Auma Oluoch na Jemedia Nyaboke Oluoch kwa kunihimiza kuendelea na masomo, kunitia moyo na kuniunga mkono katika harakati zangu za utafiti. Siwezi kumsahau babangu marehemu William Scott Kitoto aliyenitandikia zulia la elimu na kunifumbia fumbo la elimu ambalo nimeng'ang'ana kulifumbua tangu utotoni. Sitamwacha nyuma mamangu mpendwa Ziporrah Adhiambo Scott kwa kunihimiza kufuata ndoto yangu ya kuwa msoni mtajika.

Mbali na hayo, ningependa kumshukuru mwanafunzi mwenzangu Elizabeth Kerre tuliyeogelea naye katika bahari ya masomo pamoja. Ulinipa moyo wakati mlima ulipoendelea kuwa mgumu kukwea. Bila wewe huenda nisingemaliza mchakato huu kwa wakati unaofaa. Mungu akubariki na kukupa maisha marefu.

Mwisho, ninamshukuru rafiki yangu Dkt.Gerface Ochieng Ojwang' kwani ndiye aliyekuwa mwasisi wa mchakato wangu wa shahada hii. Namshukuru kwa ushauri wake ulionijia mara kwa mara nilipoelekea kugonga mwamba. Aidha sitasahau kutaja msaada wa kifedha uliyonipa na kuhakikisha nimekamilisha kazi yangu kwa wakati unaostahili.

# IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia suala la migogoro ya kimawazo katika riwaya ya Kiswahili kwa kutilia maanani *Mkamandume* (2013) ya Said A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2012) ya Wamitila K. Riwaya ya Kiswahili imezidi kupanua mawanda yake katika karne ya ishirini na moja kuliko karne zilizopita na hivyo basi kuzidi kuwa changamano. Ili kuelewa ploti na wahusika katika riwaya ya Kiswahili, ni muhimu kuchunguza migogoro ya kimawazo miongoni mwa wahusika na namna migogoro hiyo inavyoathiri ploti. Hata hivyo tafiti za awali zilizowahi kufanywa, zilishughulikia suala hili kwa kuangazia tu migogoro kwa ujumla. Watafiti wengi waliowahi kushughulikia riwaya ya Kiswahili kama vile Lomatoro (2014) aliangazia suala la migogoro kama mada ndogo tu ya utafiti wake. Hivyo basi utafiti huu uliziba pengo hili kwa kuchanganua riwaya teule za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012). Malengo ya utafiti huu yalikuwa: kubaini umuhimu wa migogoro ya kisaikolojia katika kuzua dhamira ya mwandishi; kufafanua namna migogoro ya kisaikolojia ilivyowawezesha waandishi kuwakuza wahusika katika riwaya hizi na vilevile kufafanua namna migogoro ya kimawazo ilivyokuza riwaya teule kimsuko na kuifanya kuwa na mshikamano mwema. Nadharia ya Upembuzi ya Mao Tse-Tung (1937) inayoshughulikia mikinzano katika jamii ndiyo ilitumiwa katika uchanganuzi wa data. Hii ni kwa sababu nadharia yenyewe ilikuwa na mihimili ambayo ingeweza kuchanganua data husika kikamilifu zaidi. Utafiti huu ulitumia mbinu ya kimaelezo katika uchanganuzi wa data. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha mambo matatu; kwanza, migogoro ya kimawazo kati ya wahusika mbalimbali ni kipengele muhimu ambacho huwawezesha waandishi kujenga maudhui yao mbalimbali. Pili, migogoro ya kimawazo ndiyo iliyowawezesha waandishi wa riwaya hizi mbili kuwakuza wahusika wao vyema zaidi na mwisho; migogoro ya kimawazo iliwawezesha waandishi wa riwaya za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012) kusuka ploti zao kwa weledi unaostahili. Utafiti huu utawafaa zaidi waandishi wa riwaya za Kiswahli kwa kuinua uelewa wao wa wahusika na ukuzaji wa ploti ikizingatiwa kwamba jamii ya sasa imezidi kuwa changamano zaidi. Aidha, utafiti huu utainua viwango vya uhakiki wa riwaya ya Kiswahili katika karne ya ishirini na moja na kuvifanya bora zaidi.

**ABSTRACT**

This research intended to analyze psychological conflicts in two Swahili novels: *Mkamandume* (2013) by Said A. Mohamed and *Unaitwa Nani?* (2012) by Wamitila K. The Swahili novel has shown a tremendous growth in the $21^{st}$ century compared to the past centuries and is becoming more complex with time. For us to have a better understanding of the plot, characters and themes of the Swahili novel, we need to analyze psychological traits of these characters. Despite the fact that psychological conflict is an important aspect of plot development, a few research have generally tackled this issue. Lomatoro (2014) did research on Levels of Realism and Creativity on specific Swahili novels and only touched on general conflicts. Therefore, this research filled this gap by looking into psychological conflicts as depicted in the aforementioned Swahili novels. Objectives of this research were: to find out the role of psychological conflicts in the development of main themes in Swahili novels, to illustrate how psychological conflicts assist authors to develop character traits and the effects of psychological conflict on plot. Mao's Dialectic theory (1937) was used in the analysis of data because it had three principles which adequately answered the research questions. This research used analytical method where the researcher depended on facts and information already available; analyzed them to make a critical evaluation of the material and gave findings based on the three principles of Mao's Dialectic theory. From the research, it emerged that: psychological conflict is an important aspect in building of main themes in the Swahili novel, generating character traits as well as developing the plot. This research will assist Swahili authors to have a better way of developing their plots, characters and themes. This research will also enhace Swahili literary criticism given that the society in the $21^{st}$ century is quite dynamic.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | | |
|---|---|---|
| Kusanisi | : | Mchakato unaotokana na mgongano kati ya tasnifu na tabaini na kuunda kitu kilicho kikamilifu. |
| Mabadiliko ya migogoro | : | Hali ya migogoro mipya kutokea kila mara hata baada ya migogoro ya awali kutatuliwa. |
| Migogoro ya kimawazo | : | Mivutano au mikinzano inayojitokeza akilini mwa mhusika mmoja au mawazo ya wahusika mbalimbali yanayotofautiana. |
| Muungano wa mikinzano | : | Hali ya kuwepo kwa migogoro midogo midogo inayoungana kukamilisha mgogoro mkuu. |
| Ploti | : | Mpangilio wa matukio kimaksudi katika hadithi unaofanywa na mwandishi ili kuleta mtiririko wa mawazo yanayoweza kubainisha dhamira yake. |
| Tabaini | : | Migogoro ya ndani kwa ndani katika tasnifu. |
| Tasnifu | : | Kitu kisicho kikamilifu katika ulimwengu halisi ambacho ni picha ya kitu kikamilifu katika ulimwengu wa kinjozi. |
| Ubia wa migogoro | : | Hali ya migogoro kujitokeza katika kila jamii na katika kila kitu Ulimwenguni. |
| Ukamilifu wa mikinzano | : | Hali ya kutegemeana na kukamilishana kiasi cha kuwa na |

mtagusano na mwingiliano wa vipengele mbalimbali vya migogoro ili migogoro yenyewe iweze kusimama.

| | |
|---|---|
| Upekee wa migogoro: | Kila mgogoro una upekee au jambo moja linaloutofautisha na mgogoro mwingine. |
| Upembuzi : | Ni nadharia ya fasihi inayoshughulikia mambo matatu ambayo ni: Ubia wa migogoro, Upekee wa Migogoro na mabadiliko ya migogoro. |

## YALIYOMO

Ungamo……………………………………………………………………………….……i

Tabaruku…………………………………………………………………...…….…ii

Shukrani……………………………………………………………………………..iii

Ikisiri…………………………………………………………………..…..……v

Absract………………………………………………………………………....……vi

Ufafanuzi wa istilahi……………………………………………………..……...……vii

### SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi…………………………………………………………………...……..1

1.1 Usuli wa Mada…...……………………………..……..…………………………………...1

1.2 Suala la Utafiti…………………………………………………………………...…..3

1.3 Maswali ya Utafiti……………………...……………………………………………….5

1.4 Malengo ya Utafiti…………………………………………………………...………5

1.5 Sababu za Kuchagua Mada………………………………………………………………..5

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti……………………………………………………………………7

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii…………………………………………………………….8

1.8 Misingi ya Nadharia……………………………………...……………………….22

1.8.1 Nadharia ya Upembuzi…………………………………………………………..23

1.8.2 Nadharia ya Upembuzi ya Mao……….………………………………….………...24

1.9 Mbinu za Utafiti………………………………………………………………......28

1.9.1 Mahali pa Utafiti……………………………………………………………………29

1.9.2 Muundo wa Utafiti……………………………………………………………………….29

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli…………………………………………………….…………29

1.9.4 Ukusanyaji wa Data……………………………………………………………...30

1.9.5 Uchanganuzi wa Data…………………………………………………………………...….30

1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo……..……………………………………………………….30

1.10 Hitimisho………………………………………………………………..………..…...30

## SURA YA PILI

MIGOGORO YA KIMAWAZO, DHAMIRA YA WAANDISHI NA MAUDHUI KATIKA RIWAYA ZA *MKAMANDUME* NA *UNAITWA NANI?*

2.1 Utangulizi…………………………………..…………………………………….…32

2.2.0 Muhtasari wa *Mkamandume*…………………………………..…………...33

2.3.0 Muhtasari wa *Unaitwa Nani?* ……………………………………………………..35

2.4.0 Migogoro ya kimawazo, dhamira ya mwandishi na maudhui katika riwaya ya *Mkamandume* ……………………..……………………………...………..…38

2.4.1 Uharibifu wa mazingira na athari zake ……………………..…………………….…41

2.4.2 Dhuluma dhidi ya raia……………………………………………………………...…43

2.4.3 Ukiukaji wa haki za watoto………………………………………………………...…46

2.4.4 Unyanyasaji wa kijinsia……………………..…………………………………..48

2.4.5 Tamaa………………………………………………………………………………49

2..4.6 Kukata tamaa………………………………………………………………………50

2.4.7 Umaskini……………………………..…………………………………………51

2.4.8 Usaliti……...……..……………………………………………………………55

2.4.9 Utabaka…………………………….………………………………………………50

2.5.1 Migogoro ya kimawazo, dhamira ya mwandhisi na maudhui katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* ……………………………………………………………………………56

2.5.2 Ndoa…………………………………………………………………………………..58

2.5.3 Elimu ya mtoto wa kike…………………………………………...………….62

2.5.4 Dhuluma dhidi ya wanawake……………………………..…………………….65

2.5.5 Uwajibikaji na malezi……………………………………………………………...…68

2.5.6 Utamaduni……………………………………………………………………………….70

2.5.7 Hitimisho…………………………………………………………………………...71

## SURA YA TATU

MIGOGORO YA KIMAWAZO NA UKUZAJI WA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA ZA *MKAMANDUME* NA *UNAITWA NANI?*

3.1.0 Utangulizi…………………………………………………………………..…73

3.2.0 Namna migogoro ya kimawazo ilivyomwezesha mwandishi wa *Mkamandume* kuwakuza wahusika wake……………………………………………………….74

3.2.1 Mkamandume……………………………………………………………………75

3.2.2 Time…………………………..…………………………………………………78

3.2.3 Soud…………………………...………………………………………………80

3.2.4 Nadia…………………..………………………………………………………84

3..2.5 Mzee Mkasi…………………...………………………………………………...87

3.2.6 Bwan Sleyyum………………………………………………………….…….89

3.2.7 Viwe……………………………………………………………………………..90

3.2.8 Tufaa…………………………………..………………………………………92

3.3.0 Migogoro ya kimawazo na ukuzaji wa wahusika katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*....93

3.3.1 Mwanamke……………………………………………………………………...94

3.3.2 Mwanamke ni mvumilivu………………………………………………………….95

3.3.3 Mwanamke ni jasiri……………………………………………………………...…97

3.3.4 Mwanamke ni mtiifu……………………………………………………………....98

3.3.5 Mwanamke ni mwenye utu…………………………………………………………..98

3.3.6 Mwanamke ni nafiki…………………………………………………..…..…99

3.3.7 Mwanamke ni katili……………………………………………………...………..100

3.3.8 Mwanamke ni msaliti……………………………………………..…..…………..101
3.3.9 Mwanamke ni mwongo……………………….……………………..…..…103
3.3.10 Mwanamume…………………………………………………………….……103
3.3.11 Mwanamume ni mvumilivu……………………………………….......…104
3.3.12 Mwanamume ni mwenye bidii………………………………..……..…..……105
3.3.13 Mwanamume ni katili……………………………..…………………….……….106
3.3.14 Mwanamume ni msaliti……………………..…………………………...….107
3.3.15 Mwanamume ni Mnafiki………………………………………………........108
3.3.16 Mwanamume ni mwenye tamaa……………………………….…………..…..…109
3.3.17 Hitimisho…………………………………………………………….....……110

**SURA YA NNE**

MIGOGORO YA KIMAWAZO NA PLOTI KATIKA RIWAYA ZA *MKAMANDUME* NA *UNAITWA NANI?*

4.0 Utangulizi………………………………………………………………………111
4.1.0 Migogoro ya kimawazo na ploti katika riwaya ya *Mkamandume*…………………..113
4.1.2 Muungano wa mikinzano…………………………………………………………113
4.1.3 Ukamilifu wa mikinzano………………………………………………….……115
4.1.4 Mabadiliko ya migogoro………………………………………………………….123
4.2.0 Namna migogoro ya kimawazo ilivyomwezesha mwandishi wa riwaya ya *Unaitwa Nani?* Kukuza ploti yake……………………………………………..……..127
4.2.1 Muungano wa mikinzano…………………………………………………………127
4.2.2 Ukamilifu wa mikinzano………………………………………………….……132
4.3.0 Hitimisho………………………………………………………………………….136

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1.0 Muhtasari………………………………………………………………...…….138

5.2.0 Matokeo ya Utafiti…………………………………………….…….………139

5.3.0 Mchango wa utafiti…………………………………………………………….143

5.4.0 Changamoto za utafiti…………………………………………………..……144

5.4.0 Mapendekezo…………………………..……………………………………131

Marejeleo……………………………………………………………………..……….146

Kiambatisho 1……………………………………………………………...……150

Kiambatisho 2………………………………………………………...………151

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imebainisha usuli wa utafiti na kuonyesha kuwa pana pengo kuhusu migogoro ya kimawazo kwani migogoro iliyowahi kushughulikiwa ilihusu utamaduni, utabaka, jinsia na kadhalika bila kubainisha kwamba chanzo cha migogoro hii yote ilikuwa migogoro ya kimawazo. Aidha, migogoro iliyowahi kutafitiwa ilihusu tamthilia. Sura hii imeweka wazi malengo na mipaka ya utafiti. Vilevile, yaliyoandikwa na waandishi wa awali kuhusu migogoro yaliangaziwa na misingi ya nadharia kuwekwa. Nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ni nadharia ya Upembuzi ya Mao Tse Tung.

## 1.1 Usuli wa Mada

Mgogoro ni kipengele muhimu sana katika kazi yoyote ya fasihi. Migogoro ndiyo nyenzo kuu inayoendesha kazi yoyote ya fasihi na kuipa nafasi ya kuainishwa kama kazi nzuri au chapwa. Kwa mujibu wa Majumbeni (2016), migogoro ni misuguano, mikinzano au kutoelewana kwa pande mbili au zaidi katika kazi ya fasihi. Katika kazi ya fasihi panaweza kuwepo na migogoro ya aina mbalimbali ambayo ndiyo huelekeza mtiririko wa vitushi katika kazi hiyo.

Wamitila (2003) anasema kuwa migogoro ni mivutano inayokuwa kati ya mhusika mmoja na mwingine katika kazi ya fasihi au katika akili ya mhusika mmoja na huchukua sehemu kubwa ya usimulizi wowote ule wa fasihi. Amebainisha namna migogoro mbalimbali inavyoweza kujitokeza katika kazi za fasihi. Kwanza, anasema kuwa panaweza kuwa na migogoro kati ya mhusika fulani na nguvu au kani nyingine au

mhusika mwingine. Pili, mivutano hiyo inaweza kuwa kati ya mhusika na jamii kwa jumla. Na mwisho, migogoro inaweza kuwepo kati ya mhusika na nguvu nyingine za nje.

Utafiti huu, uliegemea zaidi sehemu ya fasiri hizi zinazosisitiza kuwa migogoro ni mivutano katika akili ya mhusika mmoja katika kazi ya fasihi. Utafiti uliowahi kufanywa hapo awali kuhusu migogoro ulichunguza migogoro katika tanzu za tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Wafula (1999) alichunguza migogoro ya kitamaduni katika tamthilia tatu ambazo ni *Wakati Ukuta*,*Uasi* na *Hatia* huku Nanjala (2015) akiangazia migogoro ya kitamaduni katika hadithi fupi za Kiswahili. Murithi (2002) alichunguza migogoro katika tamthilia ya Kiswahili huku akichanganua tamthilia za *Mashetani*, *Kilio cha Haki* miongoni mwa nyingine. Mungah (1999) naye alishughulikia migogoro kwa ujumla katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*. Hata hivyo, kuna migogoro mingi katika riwaya za Kiswahili. Migogoro yenyewe ni kama ile ya kitamaduni, migogoro ya pengo la vizazi na migogoro ya kitabaka na ikichunguzwa vyema, itabainika kwamba hii yote ina asili yake katika migogoro ya kimawazo. Mgogoro ambao pia umewahi kuzungumziwa kwa kiwango kidogo ni ule wa Muindi (1990) ulojitokeza kati ya makahaba na jamii katika riwaya za S.A. Mohamed – *Mwana wa Yungi Hulewa* na *Utengano*.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), migogoro ndiyo nyenzo kuu inayoendesha usimulizi wa kazi yoyote ya fasihi. Hii inachukuliwa kama kaida kuu katika ujenzi wa msuko. Kwa kuwa migogoro ndiyo nyenzo muhimu zaidi inayoelekeza ploti katika utunzi wowote wa kazi za fasihi, ni muhimu kuichunguza ili kuipa umuhimu unaostahili. Utafiti huu umechunguza migogoro ya kimawazo katika riwaya ya kisasa ya Kiswahili ili kuziba

pengo hili. Riwaya zilizochanganuliwa ni *Mkamandume (2013)* ya Said A. Mohamed na *Unaitwa Nani? 2012* ya Wamitila K.

Utafiti huu ulichunguza mambo matatu makuu ambayo ni: namna migogoro inaweza kuendeleza dhamira ya waandishi katika riwaya za *Unaitwa Nani*? (2012) na *Mkamandume* (2013); jinsi migogoro ya kisaikolojia ilivyowasaidia waandishi hawa kuwakuza wahusika wao katika riwaya husika na namna migogoro hii ilivyousuka ploti ya riwaya huku ukichuguza hatua zinazosababisha mshikamano wa riwaya nzima. Ili kuafikia haya yote, migogoro ya kimawazo miongoni mwa wahusika mbalimbali katika riwaya hizi mbili ilichunguzwa na jinsi migogoro hiyo ilivyowawezesha waandishi hawa kutimiza malengo yao. Utafiti huu ulitumia Nadharia ya Upembuzi ya Mao Tse Tung (1937) kwa sababu ndiyo iliyokuwa na mihimili iliyoweza kuchanganua vyema zaidi migogoro ya kimawazo na kuitumia kama dira yake.

**1.2 Suala la Utafiti**

Kimapokeo, migogoro katika fasihi ni kipengele ambacho kilihusishwa zaidi katika tamthilia na ndiyo huwa sifa bainifu ya utanzu huu. Ingawa suala la migogoro hubainika zaidi katika tamthilia, hata tanzu nyinginezo kama vile hadithi fupi na riwaya haziwezi kusuka ploti zao vyema bila ya kuwepo kwa migogoro. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, fasihi ni kioo cha jamii ambacho huakisi hali ya maisha ya kila siku katika jamii na kuiwasilisha kwa njia ya ubunifu na upekee mkubwa. Ili maisha haya yaweze kuakisiwa vyema zaidi, fasihi andishi hutumia tanzu mbalimbali kama vile riwaya, hadithi fupi, tamthilia na ushairi. Ploti za kazi hizi zote husukwa kupitia kwa wahusika mbalimbali ambao ndio vipaza sauti wa waandishi. Ili wahusika watumiwe vyema

kuwasilisha ujumbe wa waandishi, waandishi wenyewe huzua migogoro miongoni mwa wahusika hao.

Mbali na kuwa suala la migogoro limechukua nafasi kubwa katika tanzu za fasihi, utafiti uliowahi kufanywa hapo awali ni ule wa Wafula (1999), Murithi (2002) na Kahara (2011) uliochunguza suala la migogoro katika tamthilia. Katika utanzu wa hadithi fupi, suala hili lilishughulikiwa na Nanjala (2015). Aidha, Mungah (1999) na Mayaka (1991) wameangazia migogoro katika riwaya lakini suala hili lilijitokeza kama mada ndogo tu katika tafiti zao. Ingawa imebainika kwamba suala la migogoro ni muhimu katika kusuka ploti ya riwaya, halijashughulikiwa kwa kina katika riwaya ya Kiswahili ya kisasa ambayo huwa na mawanda mapana na hujumuisha wahusika waliokomaa kihisia na kisaikolojia. Migogoro ya kimawazo ndiyo inayobainisha riwaya kuwa utanzu wa kihalisia. Hivyo basi, jambo hili bado linahitaji kufanyiwa utafiti wa kina ili kuifanya riwaya ya Kiswahili iwe inayoangazia matatizo ya jamii ya sasa.

Licha ya riwaya ya Kiswahili kukomaa na kupanua mawanda yake katika karne ya ishirini na moja, utafiti wa kina wa migogoro ya kisaikolojia umeachwa nyuma kwani yaliyochunguzwa ni migogoro ya aina nyingine bila kuzingatia kwamba migogoro mingine yote huibuliwa na migogoro ya kisaikolojia. Ni muhimu suala la migogoro ya kisaikolojia lishughulikiwe katika riwaya ya Kiswahili kwa sababu riwaya ya sasa ina wahusika wengi wenye itikadi, mitazamo, falsafa na matamanio changamano. Hivyo basi, utafiti huu ulijaza pengo hili kwa kuchunguza namna migogoro ya kimawazo ilivyojitokeza katika riwaya za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012) na jinsi migogoro yenyewe ilivyowaathiri wahusika hao na jamii zao.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

1. Migogoro ya kimawazo imewezaje kuibua na kuendeleza dhamira na maudhui katika riwaya za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani*? (2012).
2. Migogoro ya kimawazo imewasaidia vipi waandishi wa *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani*? (2012) kuwakuza wahusika wao katika riwaya hizi?
3. Migogoro ya kimawazo imezikuza vipi riwaya za *Mkamandume* (2012) na *Unaitwa Nani* (2012) kimsuko na kuzifanya kuwa na mshikamano mwema katika ploti zao?

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kuchanganua suala la migogoro ya kimawazo katika riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?* kwa kudhihirisha malengo yafuatayo:

1. Kubaini namna migogoro ya kimawazo ilivyoweza kuzua dhamira na maudhui katika riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?*
2. Kufafanua namna migogoro ya kimawazo ilivyowawezesha waandishi wa riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?* kuwakuza wahusika katika riwaya hizi.
3. Kuchunguza namna migogoro ya kimawazo ilivyowawezesha waandishi wa riwaya za *Mkamandume* (2012) Said A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2012) Wamitila W. kukuza riwaya zao kimsuko na kuzifanya kuwa na mshikamano mwema katika ploti.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Swali kuu linalopaswa kuulizwa ni: Kwa nini wasomi washughulikie suala la migogoro ya kimawazo katika riwaya ya Kiswahili? Kuna sababu kadhaa zinazofanya suala hili kuwa muhimu. Riwaya ya Kiswahili imepanua mawanda yake katika karne

ya ishirini na moja kuliko karne zilizopita. Wahusika wanaojitokeza katika riwaya ya Kiswahili ya kisasa wamezidi kuwa changamano na wenye matakwa mengi ambayo hayawezi kutimizwa kwa kuwachanganua kwa kutumia njia sahili. Aidha wahusika hawa wamemkaribia zaidi binadamu halisi wakilinganishwa na wale waliojitokeza katika riwaya za awali ambao baadhi yao walitumiwa kama vibonzo vya kuwasilisha mawazo ya mtunzi. Hivyo basi, ili kuwaelewa vyema wahusika hawa kisaikolojia na vilevile kuielewa ploti ya riwaya ya kisasa wahusika hawa wanapaswa kuchunguzwa kisaikolojia.

Mbali na kuwa migogoro ya kimawazo ni kipengele muhimu katika kuendesha ploti ya riwaya, hakuna utafiti wa kina uliowahi kufanywa kuhusu suala hili. Hivyo basi utafiti huu umeziba pengo hili kwa kutalii na kuchunguza suala hili kwa kina na uzito unaostahili. Ni muhimu kutambua kwamba usomaji wa kazi zinazoshughulikia migogoro ya kimawazo zinaweza kuwafaidi wanachuo wanaonuia kuendeleza utafiti wao kuhusu jinsi migogoro ya kimawazo inavyoathiri binadamu katika ulimwengu halisi kwani utawaelekeza namna ya kufanya utafiti wao katika maabara yao ambayo ni ulimwengu halisi.

Vilevile, ni muhimu kutambua kwamba wahusika hawawezi kuchanganuliwa kikamilifu katika kazi ya fasihi bila kuwepo kwa migogoro ya kimawazo miongoni mwao. Migogoro ndiyo huwakuza wahusika mbalimbali. Wahusika hao wanapokuzwa vizuri ploti ya kazi ya fasihi hujengeka kwa njia inayostahili. Utafiti huu umekuwa wa manufaa kwa kuendeleza suala hili na kulikuza ipasavyo ili

waandishi wa baadaye nao waweze kujumuisha wahusika waliokamilika na kukaribia zaidi binadamu halisi katika uandishi wao.

Ingawa waandishi wengi wa riwaya wametumia suala la migogoro kuendeleza dhamira zao na sifa za wahusika wao, ni wachache tu ndio wamezua migogoro ya kimawazo kwa viwango vikubwa na kuonyesha athari zake kwa wahusika wao. Utafiti huu umetumia riwaya hizi mbili – *Mkamandume* (2013) ya Said A. Mohamed na *UnaitwaNani?* (2012) ya K. Waitila kwa sababu ndizo riwaya zilizokuwa na data muhimu na wahusika changamano wanaoonyesha usawiri ulio mpevu na kubainisha kwa uwazi zaidi athari za migogoro ya kisaikolojia

Aidha, *Mkamandume* ni mojawapo ya riwaya changamano na yenye kurasa nyingi zaidi iliyowahi kuandikwa katika Kiswahili katika karne ya ishirini na moja. Vivyo hivyo riwaya ya *UnaitwaNani?* ilitekeleza wajibu mkubwa katika utafiti huu kwa sababu ina data toshelevu kwa utafiti huu kwani mle ndani mlikuwa na mivutano kadhaa ya kimawazo.

Kilicho muhimu zaidi katika utafiti huu ni kwamba umeziba pengo ambalo limekuwapo kwa muda mrefu kuhusu kipengele cha migogoro ya kisaikolojia katika riwaya ya Kiswahili hasa katika karne hii ya ishirini na moja.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Katika fasihi, kuna migogoro ya aina mbalimbali ambayo hutumiwa kukuza kazi hizo. Wamitila (2003) anasema kwamba panaweza kuwa na migogoro ya aina tatu katika kazi za fasihi. Kwanza, kuna migogoro kati ya mhusika fulani na mhusika

mwingine. Pili, kuna mivutano kati ya mhusika na jamii kwa jumla. Aidha, pana uwezekano wa migogoro kukatokana na mvutano wa kiakili wa mhusika.

Utafiti huu ulishughulikia zaidi migogoro ya kimawazo katika riwaya za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012). Aidha, kazi nyingine zilipitiwa tu hasa katika sehemu ya uchanganuzi wa data kwa kuwa zilingiliana na uchanganuzi huu na kuutia nguvu ila hazikuwa sehemu ya kimsingi ya kazi hii.

Riwaya za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012) ziliteuliwa kwa sababu ndizo zilizokuwa na data mwafaka zaidi kuhusu migogoro ya kisaikolojia mbali na kuwa zimechapishwa katika karne ya ishirini na moja. Aidha, utafiti huu ulishughulikia kazi za waandishi wengine mbali na S.A. Mohamed na K.W. Wamitila ili kutoa ithibati na kutilia mkazo hoja muhimu katika uchunguzi wake. Kazi hizi zilikuwa za manufaa sana kwa utafiti huu kwani zilifafanua zaidi mada yenyewe kama ilivyojitokeza katika sehemu ya yaliyoandikwa.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Ingawa kuna tafiti nyingi zilizoshughulikia suala la migogoro katika kazi za fasihi, kuna tafiti chache zilizogusia migogoro katika riwaya kwa ujumla. Mgogoro ni kipengele muhimu katika kazi zote za fasihi na inakuwa vigumu kuendeleza ploti ya hadithi yoyote bila ya kuwepo kwa migogoro iliyokuzwa vyema. Usawiri wa wahusika katika riwaya ni jambo linalowezekana tu kwa sababu ya kuwepo kwa migogoro miongoni mwao. Bila ya migogoro, inakuwa vigumu kuwakuza wahusika katika riwaya.

Fanon (1952) anasema kuwa, ili kujenga umoja wa kitaifa lazima pawepo na mwingiliano wa kitamaduni na kupotea kwa migogoro iliyokita mizizi miongoni mwa watu wa rangi tofauti. Anasisitiza kwamba mtu mweusi ana migogoro ya aina mbili: migogoro kati ya mtu mweusi na mweusi na migogoro kati ya mtu mweusi na Mzungu. Haya yote yanatokana na ukoloni. Mzungu anaamini kwamba mtu mweusi si binadamu na amemfanya kuamini kwamba anapojifunza lugha ya Mzungu anakaribia zaidi kuwa binadamu. Jambo hili limewaingia watu weusi akilini kiasi kwamba wanapigana na dhamiri zao kuacha utamaduni wao na kung'ang'ania utamaduni wa Mzungu. Jambo hili limezua migogoro ya kimawazo miongoni mwa Waafrika. Mawazo haya yalisaidia kueleza chanzo cha migogoro ya kiawazo miongoni mwa Waafrika katika riwaya ya *Mkamandume*. Wakoloni walipoingia Malelejimema, waliwapumbaza Waafrika na kubadili sera ya ardhi ambayo ilikuja kuwa chanzo cha migogoro ya kisaikolojia akilini mwa wahusika kama Mkamandume, Soud, Nadia Time na wengine.

Nazareth (1972) akirejelea shairi la Okello Oculi, anazungumzia migogoro iliyopo kati ya matabaka mawili; tabaka la chini na tabaka la juu. Mgogoro huu ni wa kijamii ambao umeletwa na matatizo yaliyosababishwa na mwanadamu mwenyewe na suluhisho lake pia linaweza kutokana tu na mwanadamu. Aidha, Nazareth anarejelea tamthilia ya *Antigone* (1961) iliyoandikwa na Anouilh. Hapa anarejelea mgogoro unaojitokeza kati ya mhusika mkuu ambaye ni msichana mdogo aliyeamua kupigania maadili na kaida zote zilizoendeleza utu akipuuza sheria mpya za serikali zilizowekwa na mtawala mpya aliyeshikilia kwamba nchi yao lazima ihifadhiwe kwa

vyovyote vile. Jambo hili linaleta mgongano kati ya mhusika huyu na utawala. Kwa hivyo, Nazareth anauliza maswali yafuatayo:

a) Je, ni wakati gani sheria za nchi zinaweza kuwa za kukandamiza?
b) Je, sheria hizo zinaweza kukiukwa na wale wanaoziona kama sheria dhalimu?
c) Je, ni maswali yapi hutokea akilini mwa mtawala anayetunga sheria za kidhalimu zinazoishia kukiukwa na watawaliwa

Vilevile, Nazareth (1972) katika makala yake "*Is A Grain of Wheat a Political Novel?"* Anaangazia migogoro iliyokuwepo baina ya Mwafrika na Mzungu wakati wa ukoloni. Anarejelea riwaya ya Ngugi wa Thiong'o *A Grain of Wheat* kufafanua kwamba uhasama kati ya Waafrika na Wazungu ulitokana na utawala wa kidhalimu ulioendelezwa na Wazungu dhidi ya Wakenya. Jambo hili linawafanya Wakenya, hasa Wakikuyu, kuunda jeshi la Mau Mau ambalo lilikuwa na lengo moja tu la kurejesha uhuru wao kutoka mikononi mwa mkoloni. Hata hivyo, jambo hili haliwi rahisi kwani hata miongoni mwa Waafrika wenyewe mlikuwa na wasaliti ambao kisirisiri waliwasaliti wenzao lakini watu hawakuwafahamu kuwa wasaliti. Mawazo haya yanalenga vyema yale yanayopatikana katika riwaya ya *Mkamandume* (2013) kwani hata mingoni mwa Wamalelejimema palikuwa na wale walioconekana kama wasaliti na kuuawa kwa kufyekwa vichwa.

Yanayodhihirika kutoka kwa uchanganuzi huu wa Nazareth, ni kwamba mgogoro ni suala changamano na lenye mzunguko kiasi kwamba migogoro midogo midogo ndiyo huchangia na kukamilisha mgogoro mkuu unaojitokeza katika jamii. Jambo hili lilikuwa la manufaa katika utafiti huu kwa kuwa lilibainisha namna migogoro midogo

inavyojenga na kukamilisha mgogoro wa kimawazo ambao pia huishia kujenga migogoro mingine katika jamii.

Eagleton (1976) anasema kwamba mawasilisho ya fikra, dhana na ung'amuzi wa binadamu hujikita katika ulimwengu wake halisi, lugha yake na maisha halisi. Anasisitiza kwamba ubunifu wa kifasihi huanza kwa maneno yasemwayo na wanadamu, wayafikiriayo au mawazo yazaliwayo nao. Anasisitiza kwamba maisha hayatokani na ung'amuzi bali ung'amuzi hutokana na maisha na kwa kuwa wanajamii huwa na mitazamo tofauti tofauti kuhusu ulimwengu wao, mara nyingi fikra zao hukinzana. Kazi za kisanii hazitokani na ombwe tupu au fikra za kisaikolojia za mwandishi bali hutokana na migongano itokanayo na namna wanajamii wanavyouona ulimwengu. Mbali na hayo, anasema kwamba wanadamu hawana uhuru wa kuchagua uhusiano na maingiliano kati yao bali hayo yote hutokana na ulimwengu wao halisi.

Mambo yanayoweza kufasiriwa kutokana na mawazo haya ya Eagleton ni kuwa suala la migogoro ni suala ambalo huanzia akilini mwa binadamu. Kabla ya mgogoro wowote kujitokeza katika jamii, huanzia kwenye akili ya binadamu ambaye huishi katika mazingira fulani yanayoathiri mkondo wake wa mawazo. Mazingira ya mwanadamu huelekeza mawazo yake kuchukua mwelekeo fulani ambao unaweza kutofautiana na mwelekeo wa mwanajamii mwingine ambaye anaweza kuwa amekulia katika mazingira yale yale lakini masuala mengine yakaathiri mtazamo wake na hivyo kuzua migogoro ya kimtazamo kati ya wahusika hao.

Morroe (1977) anasema kwamba mwandishi wa riwaya anapochanganya ubunifu wake na ukweli hutafuta maelezo na kujifunza kuhusu jamii anayoiandikia, namna jamii hiyo inavyoishi na mambo yanayoweza kuzua migongano kati ya wanajamii hao. Akimrejelea Harriet Martineau (mwandishi maarufu katika mwaka wa 1830) Morroe anasema kwamba mwandishi huyu alibuni kazi zilizochanganua mambo yaliyohusu sanaa na uchumi na namna hali ya uchumi ilivyozua migogoro. Harriet alikiri kwamba jambo la pekee linalostahili kufanywa ni kutoa ploti kutoka kwa jamii halisi kwani humo ndimo mnamopatikana migongano yote inayoweza kufanya kazi ya fasihi kuwa hai na ya kuvutia. Alisisitiza kwamba hata waandishi maarufu kama Shakespeare na Scott waliweza tu kubobea kwa kuonyesha mikinzano iliyokuwa katika jamii zao wakati huo.

Haya yote yanayoelezwa na Morroe (1977) yanatudhihirishia kwamba; ili kazi yoyote ya fasihi iweze kufanikiwa lazima mwandishi afahamu namna ya kusuka ploti yake vyema na ploti huweza kusukika vyema tu iwapo migogoro inayojitokea katika kazi husika itashughulikiwa ipasavyo. Kwa kuwa mgogoro unajitokeza kama kipengele muhimu katika fasihi, itakuwa vyema kusema kwamba bila ya kuwepo kwa mgogoro uliobainishwa vyema katika kazi ya fasihi, inakuwa vigumu kutunga kazi inayovutia. Hata hivyo, hii haina maana kwamba mgogoro ndio kipengele muhimu zaidi katika fasihi. Hapa tunasisitiza umuhimu wa migogoro lakini vipengele mbalimbali vya fasihi hutegemeana na kukamilishana. Kwa mfano, mgogoro hauwezi kubainika vyema bila ya msanii kutumia lugha kwa namna ifaayo na kukuza maudhui yake itakikanavyo. Mawazo haya yaliingiliana vyema na utafiti huu kwani riwaya za

*Unaitwa Nani?* (2012) na *Mkamandume* (2013) zilidhihirika kwamba chanzo cha migogoro ya kimawazo kilikuwa tofauti za kiuchumi iongonimwa wahusika mbalimbali.

Muindi (1990) ameshughulikia usawiri wa wahusika makahaba katika riwaya za S.A. Mohamed akisema kwamba wengi wa wahusika hawa hujiingiza katika ukahaba kwa sababu ya migogoro iliyopo baina yao na jamii. Anaangazia migogoro iliyopo baina ya Mamwinyi na mabinti zao waliotawishwa. Anasema:

> Aghalabu Mamwinyi walipendelea kuwatawisha wake na mabinti zao ... katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa* sawa na *Utengano*, watawa wake waliweza kuvunja miiko ya utawa na kujitafutia uhuru wanaotaka (uk. 60)

Anadhihirisha migongano iliyokuwa kati ya wanawake na wanaume. Wanawake na mabinti zao walihisi kwamba wanaume waliwanyanyasa na kuwanyima uhuru wa kujiamualia mambo. Mawazo haya yana uwiano na yale yanayojidhihirisha kwenye riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2012). Humo, mnapatikana wanawake kama vile Kasekesi, Mwanamuka, Kamene na wengine ambao walinyanyaswa na wanaume.

Mayaka (1991) akizungumzia suala la migogoro anasema kwamba kilichobainika kufikia sasa ni kuwa wasomi ama wamejitenga au wametengwa na jamii. Kwa kiasi kikubwa utengano huu unatokana na kisomo chao ambacho kimewafunza njia mpya za uzalishaji mali ambazo zinapingana na za jamii. Kwao sasa ubinafsi umewapofusha kiasi cha wengine kuibia jamii bila haya. Lengo kuu ni kujiendeleza wao wenyewe. Hivyo basi, panatokea wakati fulani mtu binafsi anapoyakataa malengo ya jamii na kujitenga. Hali hii ndiyo inawapata wasomi na inaweza

kuangaliwa kama ukengeushi wa kutengwa na kujitenga na jamii. Anasisitiza kwamba ili tuweze kuuelewa mgongano huu kwa ukamilifu, inabidi tumchunguze msomi zaidi kwa upande wa utamaduni huku tukizingatia tamaduni mbili; ule wa Kiafrika (wa jadi) na wa Kimagharibi (wa sasa) , na mifumo ya uzalishaji mali ambayo tamaduni hizi zinawakilisha. Mbali na kuwa na elimu ya kigeni, usomi unaambatana na utamaduni wa kigeni ambao unakinzana na ule wa jamii ya jadi. Mikinzano hii ndiyo humvuruga msomi na wengine kati yao huchanganyikiwa. Hili sasa ni tatizo la kijamii na ni jukumu la waandishi kulimulika.

Mayaka (1991) anasema kwamba Msomi Mwafrika huwa na elimu ambayo humpa kibali cha kupata kazi za hadhi na matakwa yake huwa ya kibinafsi. Anachotaka ni kupandishwa vyeo na kujiimarisha mwenyewe. Hali hii ndio huleta migongano baina ya msomi na wanajamii wengine. Anasisitiza kwamba tatizo hutokea wakati msomi anaposhindwa kuingia vizuri katika mfumo wa kijamii, anapojaribu kuhamisha fikra ngeni alizozipata katika usomi wake na kuzileta nyumbani kwa jamii inayozingatia maadili ya kijadi. Wakati jambo hili linapotokea, msomi huwa ameng'olewa kutoka kwa utamaduni wake wa jadi. Yeye sasa anatekeleza kazi ya kuwa 'gari' la kubebea mawazo ya kimagharibi na kuyapeleka kwa jamii yake.

Utafiti wa Mayaka, unatubainishia namna migogoro inavyoweza kutokea katika jamii kutokana na ukengeushi wa wasomi. Jambo hili limekuwa muhimu katika utafiti huu kwani tumechunguza namna migogoro ya namna hii inavyoweza kuzua migogoro ya kiakili kwa wahusika mbalimbali katika riwaya za *Mkamandume* (2013) na

*UnaitwaNani?* (2012) na athari za migogoro kama hiyo kwa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Wafula (1999) alichunguza kwa kina swala la migogoro ya kitamaduni inayotokana na pengo la kizazi kwa kuchanganua tamthilia tatu ambazo ni *Wakati Ukuta*, *Uasi*, na *Hatia*. Anaangazia suala hili kwa kuonyesha namna migogoro ya kitamaduni inavyozua matatizo yanayosababishwa na usasa na ukuaji wa miji. Katika uchanganuzi wake, anasema kwamba dhamira ya mgongano wa tamaduni tofauti imechunguzwa na waandishi tofauti kama Ngugi wa Thiong'o (1974), Chinua Achebe (1973) na Okot P'Bitek'. Anasisitiza kwamba Ngugi na Achebe wanakubaliana kwamba Ukoloni na Ukristo ndizo sababu muhimu zinazozua migogoro baina ya imani ya Mwafrika na ile ya Mzungu.

Hapa, Wafula anatupa mtazamo mwingine wa migogoro inayochukua mkondo wa dini. Mwafrika na Mzungu wana imani tofauti kuhusiana na dini. Watu hawa walipotagusana hasa wakati wa ukoloni, palitokea migongano ya kidini na kwa kuwa imani za kidini huenda sambamba na utamaduni wa jamii, inakuwa vigumu kuepuka migongano ya kitamaduni pia. Hivyo basi, migongano hii ya kidini inazua mingonano mingine.

Mungah (1999) katika uchanganuzi wake wa riwaya mbili za Kezilahabi – *Nagona* na *Mzingile* anazungumzia suala hili la migogoro kwa kubainisha kwamba mwanadamu huzua migogoro akilini mwake anaposumbuka kutafuta ukweli ambao siku zote humtoroka badala ya kuyashughulikia maisha yake. Mhakiki huyu

anasisitiza kwamba Kezilahabi anayaona maisha kama ambayo binadamu hana haja ya kujishughulisha nayo bali kuyaishi kama yalivyo. Maisha yake ndiyo anapaswa kuyazingatia lakini yeye hujishughulisha kutafuta ukweli ambao haupo.

Mungah anazidi kusema kwamba Kezilahabi amedhihirisha kushindwa kwa dini kama asasi. Katika juhudi za mwanadamu za kusaka ukweli wa maisha na uhalisi wake, dini imekuwa ni asasi mojawapo muhimu. Masuala muhimu yahusuyo maisha na ambayo mwanadamu huwa hana majibu yake huelekezewa kwa Mungu kupitia dini. Lakini katika kuhakiki riwaya za *Nagona* na *Mzingile* inadhihirika kwamba dini imeshindwa kutoa jawabu toshelezi. Hii ndiyo sababu padiri anajibiwa ifuatavyo na Babu, anapowauliza wazee kama miongoni mwao hamna Mkristo: "Mbona unacheza ngoma yako nje ya duara?” (*Nagona* uk. 10). Waumini huwa na njia zao za kusaka ukweli ilhali “wapagani”, kama anavyowaita mwandishi, huwa na njia zao pia. Ndiyo sababu Babu anamwambia Padiri kuwa anacheza ngoma yake nje ya duara. Dini imeshindwa kumpa mwanadamu jawabu analotaka na viongozi wake wameonyeshwa wakiwa walevi. Hivyo mawazo yake yanamwelekeza kutafuta njia za kitamaduni za kutafuta ukweli ambao umemponyoka kwa karne nyingi.

Viongozi wa dini walipaswa kuwa vielelezo wa kufuatwa na watu wengine hasa katika maisha na mienendo yao. Lakini kama ambavyo Kezilahabi ameyasawiri maisha katika riwaya hizi mbili ukweli umekuwa kitendawili kigumu na hata kwa wale ambao walipaswa kuwa kielelezo chake wamelemewa na mtihani huu mgumu. Badala yake wanajiingiza katika mambo ya ulimwengu na wanakuwa walevi kupindukia. Basi dini kama asasi muhimu maishani mwa binadamu imelemewa kwa

vile viongozi wake wameonyeshwa kama watu wasiofuata kanuni zake. Mchanganuzi huyu anatupa taswira kuwa maisha ni vurumai tupu. Hii ndiyo maana anamshirikisha kila mtu katika ngoma kuu katika riwaya ya *Nagona*.

Katika uchanganuzi wa Mungah tumeweza kubaini kwamba mara nyingine mwanadamu huweza kuzua migongano kuhusu suala fulani ambalo humsumbua. Katika uchanganuzi wa *Nagona* na *Mzingile*, kitendawili anachotafuta kukitegua ni ukweli. Ukweli huu umemponyoka na asasi mbalimbali katika jamii kama vile dini na serikal zimeshindwa kuupata. Jambo hili linazua mikinzano katika jamii kwani kila asasi inatafuta njia zake tofauti za kushughulikia masuala fulani muhimu. Maridhiano yanapokosekana katika njia hizi mbalimbali, panatokea migogoro katika jamii. Katika utafiti huu tumebaini tofauti za kimawazo ambazo zinaweza kuwa chanzo cha kukosekana kwa maridhiano hasa kwa kuzingatia wahusika mbalimbali katika riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?*

Murithi (2002) katika uchanganuzi wake anadhihirisha migogoro katika thamthilia ya *Mashetani*. Anasisitiza kwamba mwandishi Hussein anashughulikia migogoro ya kiuchumi na kisiasa katika bara la Afrika. Anadhihirisha kwamba kuna mivutano baina ya matabaka ya wenye uwezo na wanaonyanyaswa. Migogoro yenyewe inabainika kupitia kwa miingiliano ya kisiasa na kiuchumi. Mwishoni mwa tamthilia, inabainika kupitia kwa familia za Juma na Kitaru kwamba matabaka mawili mbalimbali hayawezi kupatana kwa vyovyote. Mhakiki huyu pia anazungumzia mivutano ya nafsi. Anasema kwamba Shetani anawakilisha viongozi wa kikoloni na wakoloni mamboleo ambao wamewatawala Waafrika wanyonge (binadamu)

wasiokuwa na nguvu za kiuchumi. Baadaye, Shetani (Mkoloni) anampa Binadamu (Mwafrika) siri (elimu) inayomzindua na kudai uhuru wake. Kwa hivyo nafsi za Mashetani na Binadamu zinavutana. Waafrika wanadai uhuru wao lakini wakoloni wanakataa kuwapa uhuru huo. Mapinduzi yanapofaulu, viongozi wanaochukua hatamu wanaendeleza sera za kishetani kwani wanazidisha dhuluma dhidi ya wanyonge. Kwa mujibu wa uchanganuzi huu, Juma anayependa ubwana na Kitaru anayependa usawa wanapewa nafasi zinazopingana hivyo kuzua mgogoro baina yao. Juma anaona kuwa kusomea chuo kikuu kunampa tikiti ya kupata ubwana naye Kitaru anaona kuwa elimu ya chuo kikuu ni ya kumfanya mtu kujielewa zaidi.
Kuna mivutano kati ya familia ya Kitaru na familia ya Juma. Baada ya wakoloni kuondoka, familia ya Kitaru imeendelea kupanda kiuchumi huku familia ya kina Juma ikididimia na hivyo basi nafsi za familia hizi mbili zinaendelea kutofautiana. Japo Juma na Kitaru ni marafiki kwa kuwa wote walikuwa wakisomea vyuo vikuu, wana nafsi zinazopingana. Ingawa Juma aliwakilisha tabaka la chini, alikuwa na mawazo ya ubwana. Kitaru anang'ang'ania kupata kuuelewa ukweli wa jamii yake – anataka kuondoa nafsi ya ushetani na kuwa na nafsi ya binadamu. Juma kwa upande mwingine anawazia ubwana.

Vilevile Murithi (2002) anaelezea migongano inayopatikana katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki*. Kuna mivutano kati ya nafsi ya watawala na watawaliwa. Watawala wanawalinda wanyanyasaji kama vile Bwana Delamon kwa kutumia sheria mbovu na askari. Mgongano huu unatokea kwa sababu watawala hawatekelezi wajibu wao wa kuwalinda watawaliwa. Kwa mfano kuna msichana anayetafunwa na majibwa ya

Bwana Shamba lakini Bwana Shamba hachukuliwi hatua yoyote. Mvutano huu pia unaendelezwa baina ya waajiri na waajiriwa. Bwana Delamon amewaajiri watu wengi na kuwapa mishahara duni. Kwa upande wao, waajiriwa wanataka kazi lakini wanaona kwamba wanadhulumiwa na Delamon kwa kupewa mishahara midogo.

Uchanganuzi wa Murithi unaendeleza utafiti kuhusu migogoro ya kitabaka katika tamthilia na jinsi migogoro hiyo ilivyoathiri mahusiano ya wahusika mbalimbali. Utafiti wake ulitofautiana na huu wa kisaikolojia kwa kuwa; mbali na kuchunguza migogoro hii ya kitabaka katika riwaya, ulitafuta kubaini chanzo cha migogoro ya aina hii na iwapo inaweza kusababishwa na migongano ya kimawazo.

Kahara (2011) anapolinganisha tamthilia ya *Kinjeketile* na *Mzalendo Kimathi*, amebainisha migogoro kati ya Wakoloni na Waafrika. Anasema kwamba ukoloni uliwafanya Waafrika kuupoteza uhuru wao, mashamba yao na kuathiri mifumo yao kiuchumi. Mwishowe, Mwafrika anajikuta amejikita katika mfumo wa kibepari ambapo alijikuta kama skwota katika mashamba ya walowezi. Katika mfumo huo, alijikuta ni mzalishaji mali tu na hakuwa na udhibiti wowote wa njia za kuzalisha mali yenyewe. Vivyo hivyo anajikuta hana sauti katika ugavi wa mali aliyozalisha. Mfumo huu wa kibepari unazua mgogoro kati ya Waafrika na Wakoloni na kuwafanya Waafrika kuanza kupigania haki zao. Jambo lililomfanya Mwafrika kutofaulu kupigania haki zake katika tamthilia hizi ni migogoro kati ya jamii za kiafrika. Kahara ananukuu kutoka kwa *Kinjeketile* na kusema:

> Jua limetoka ... nuru yake itaondosha moshi na kiza, kiza kilichomficha Mrufiji asionekane na Mngoni. Moshi ulioziba macho ya Mrufiji yakawa hayamtazami Mmatumbi ... (Kahara, 2011:46)

Kinjeketile alipendekeza vita dhidi ya utawala wa kikoloni. Hata hivyo kulikuwa na kikwazo kingine hatari zaidi cha ukoloni mamboleo wa Mwarabu. Baada ya kugundua kwamba Hongo alimsaliti, Kinjeketile anasema: "Nimedanganywa. Wameniuwa, nimejiuwa mimi mwenyewe. Ilikuwa ndoto nikiota! Apana! Wamenidanganya" (Uk. 20). Kahara anasisitiza kwamba majuto ya Kinjeketile yanathibitisha mgogoro wa ndani kwa ndani kwa mhusika huyu na hata dhidi ya wahusika wengine. Mgogoro huu unachangiwa na mhusika kufahamu kwamba kuanzia hapo lazima athibiti athari ya matendo yake. Haya yalikuwa na mwingiliano na utafiti wa riwaya ya *Mkamandume* (2013) kwani yanatufanya kufahamu vyema zaidi mawazo yalitomtatiza Mkamandume na kumfanya afyeke vichwa vya watu.

Nanjala (2015) kwa upande wake anaangazia migongano ya kitamaduni katika mikusanyiko minne ya hadithi fupi za Kiswahili: *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* (2007), *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* pamoja na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007). Kulingana naye, migogoro ya kitamaduni imeletwa na ukale unaozidi kufifia kila uchao na usasa unaochomoza kwa mshindo mkuu. Ameangazia desturi mbalimbali zinazosababisha migongano ya kitamaduni miongoni mwa jamii mbalimbali. Anasema kwamba baadhi ya vipengele vya kitamaduni vinavyosababisha migogoro hii ni kama vile suala la urithi wa wajane, ulipaji wa mahari na kuozwa kwa watoto wadogo, tohara kwa wanawake, mfumo wa kuumeni miongoni mwa mengine. Anasisitiza kwamba fasihi ni kitambulisho cha jamii za binadamu. Fasihi huwa na mwingiliano mkubwa na tamaduni mbalimbali na kuwa namna ya maisha katika jamii hizo kiasi cha kwamba

inakuwa vigumu kuwabadilisha wanajamii na kuwafanya waache hali yao ya maisha waliyozoea tokea utotoni. Wanajamii wanapohitajika kuyabadilisha mawazo yao ya jadi, kunatokea mitafaruku na migongano kati ya tamaduni mbili zilizo tofauti. Nanjala akimnukuu Matei (2011) anasema kwamba, 'miongoni mwa masuala mbalimbali yanayoshughulikiwa na taaluma ya fasihi ya Kiswahili ni mgongano wa kitamaduni ambao umedhihirika katika jamii ya sasa.

Kwa mujibu wa utafiti wa Nanjala, kuna mambo mawili makuu yanayodhihirika. Jambo la kwanza ni kuwa utamaduni huchukua nafasi muhimu katika maisha ya wanajamii na utamaduni ndio huunda jamii yoyote ile. Pili, panaweza kutokea mitagusano kati ya tamaduni mbili zinaokinzana, na jambo hili litokeapo, panazuka migogoro ambayo inaweza kuendelea kwa muda mrefu. Kila mara panapotokea mabadiliko katika jamii, kuna sehemu ya wanajamii ambao hujaribu kuhifadhi utamaduni wao hivyo basi kuhitilafiana na wale wanaokumbatia mabadiliko.

Utafiti wa Nanjala (2015), umebainisha namna migogoro ya kimawazo inaweza kuzuka kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wanajamii wanaweza kuathirika na tamaduni za jamii zao kiasi cha kwamba wanapokumbwa na utamaduni mpya huchanganyikiwa na kushindwa kufanya uamuzi kuhusu utamaduni wanaostahili kuukumbatia. Kufikia sasa imedhihirika kwamba ni jambo rahisi zaidi kubainisha migogoro katika tamthilia kwani migogoro ndiyo mihimili mikuu katika utanzu wenyewe. Tafiti nyingi ambazo zimefanywa zimehusisha utanzu wa tamthilia kwa wingi kuliko riwaya. Hata hivyo migogoro inayoshughulikiwa ni ile ya kitabaka, kitamaduni, kidini na kadhalika. Utafiti wa *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?*

(2012) ulitoka nje kidogo ya migogoro iliyoshughulikiwa kwa wingi na kujishughulisha na namna migogoro hiyo yote inaweza kuzuka kutokana na mgogoro wa kimawazo katika riwaya husika.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Ndaharia ni dhana iliyopewa fasiri mbalimbali na wataalamu mbalimbali. Ogechi, Shitemi na Simala (2008) wanasema kwamba neno nadharia linabeba dhana nyingi kwa wakati mmoja. Hata hivyo, wanaeleza maana ya nadharia kama mzingiro unaozunguka mawazo fulani yanayotofautisha mawazo hayo na yanayozungukwa na mzingiro mwingine tofauti. Wanaongezea kusema kwamba nadharia ni dira ya kumwongoza mtafiti au kumwezesha kutalii na kuelezea vyema masuala yake kwa mtazamo unaotarajiwa kuwa imara zaidi kuliko ule wa nadharia nyingine. Nadharia huondoa '*uovyo'* wa mambo katika kutalii somo la lugha na fasihi.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kwamba nadharia ni "jumla ya maelezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum." TUKI (2004) nayo inasema kwamba nadharia ni "mawazo, maelezo au mwongozo unaosaidia kueleza, kutatua na kutekeleza jambo fulani. Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba nadharia humwezesha msomaji kufahamu mambo mengi zaidi kwa undani katika kazi yoyote ya fasihi.

Utafiti huu, ulitumia nadharia kwa maana ya "maelezo yanayofafanua mawazo mbalimbali katika fasihi kwa kuzingatia utaratibu fulani maalum." Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya upembuzi ya Mao Tse Tung (1937). Hii ni kwa sababu

nadharia ya Upembuzi ndiyo yenye mihiili inayoweza kuchanganua migogoro ya kimawazo kikamilifu.

Utafiti huu uliteua baaadhi ya mihimili ya nadharia ya Upembuzi ambayo iliingiliana vyema zaidi na migogoro ya kisaikolojia na kuitumia kama dira yake iliyotuelekeza kufafanua migogoro katika riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?*

### 1.8.1 Nadharia ya Upembuzi

Soo (1981) anasema kuwa nadharia ya Upebuzi ni nadharia ya kifalsafa iliyoasisiwa na mwanafalsafa wa Kijerumani kwa jina Hegel katika karne ya kumi na tisa. Hegel alisema kuwa sababu kuu ya upembuzi ni kuchanganua mambo jinsi yalivyo na kuyabainisha ili kuondoa utata kati ya mambo tofauti. Katika nadharia hii, Hegel alikuwa akiendeleza mawazo ya Plato ingawa anasema kwamba mawazo yake yanatofautiana na yale ya Plato kwa kuwa Plato alizungumzia tasnifu na tabaini katika migogoro na mikinzano ya kawaida bila kuzungumzia suluhu inayopatikana mwishoni. Kwa hivyo, yeye anatoa suluhu kwa kuonyesha kwamba upembuzi ni mchakato unaoendelea kila wakati na huhusisha kila kitu ulimwenguni. Kwamba mchakato huu hauwezi kukamilika mpaka unaposheheni mambo matatu: tasnifu, tabaini na kusanisi.

Wafula na Kimani (2007) wanasema kwamba mawazo ya Hegel yaliingiliana na yale ya Plato kwani wote wawili waliamini kwamba vitu vyote vipatikanavyo ulimwenguni ni picha hafifu ya vitu hivyo kama vinavopatikana katika ulimwengu wa kinjozi. Hegel aliamini kwamba vitu hivyo huendelea kukua na kubadilika hata vikaelekea kuwa vikamilifu. Wanasema kwamba Hegel alikiita kitu kisicho kikailifu tasnifu. Tasnifu ikiwa asili ya kitu au jambo na kwa kuwa tasnifu haijakamilika wala kujitosheleza, huzalisha

migogoro ya ndani kwa ndani ambayo huitwa tabaini. Tabaini ikigongana na tasnifu huzalisha kusanisi. Kusanisi nayo siyo kamilifu hivyo basi hujenga tasnifu mpya. Tasnifu hii vilevile haijitoshelezi hivyo basi kuibua migogoro mingine na mchakato wote kujirudia tena. Kwa hivyo, Hegel alisisitiza kwamba mchakato huu unaozua migogoro ya tasnifu na tabaini huendelea mpaka hali kamilifu ya kidhahania ya kitu inapofikiwa. Hali hiyo dhahanifu ndiyo kamilifu na timilifu kuliko zote. Hegel alifafanua kwamba masuala yanapaswa kufasiriwa kama michakato ya mambo changamano yanayoendelea kukua ili yafikie ukamilifu unaostahili bali yasifasiriwe kama matukio.

Mbali na matapo ya Hegel na Marx, matapo mengine yaliyoendeleza nadharia hii ni kama lile la, Mao Tse–Tung na Lenin. Kati ya matapo hayo yote, utafit huu ulitumia nadharia ya Upembuzi ya Mao Tse-Tung kwa kuwa ndiyo yenye mihimili iliyoweza kuchanganua data husika kwa kina.

### 1.8.2 Nadharia ya Upembuzi ya Mao Tse–Tung (1937)

Kwa mujibu wa Soo (1981), nadharia ya Upembuzi ya Mao Tse–Tung ni nadharia inayoshughulikia mikinzano katika jamii. Nadharia hii iliasisiwa na Mao Tse–Tung aliyekuwa kiongozi wa Uchina kati ya miaka ya 1949 – 1976. Aliasisi nadharia hii katika mwaka wa 1937. Mao aliishi kati ya 1893 – 1976. Ingawa babake alikuwa mkulima wa tabaka la chini katika maisha yake ya awali, alikuja kuwa tajiri hapo baadaye na hivyo basi Mao hakupitia ugumu walioupitia watoto wa watu wa tabaka la chini. Hata hivyo, jambo hilo halikumfanya kuepuka kufanya kazi kwenye mashamba ya matajiri akiwa angali na umri mdogo. Jambo hili lilimfanya afahamu ugumu uliowakumba maskini wa tabaka la chini. Kwa kuwa familia yake ilikuwa ya tabaka la juu, alipata elimu na

baadaye kujiunga na jeshi la mapinduzi nchini Uchina mnamo mwaka wa 1911. Baadaye alisomea taaluma ya ualimu kati ya mwaka wa 1913 – 1918. Kati ya mwaka wa 1919 – 1921, Mao alianza kufuata itikadi za ki-Marx na kuwa mwanzilishi wa Chama cha Kijamaa cha Uchina (*Chinese Communist Party*).

Soo (1981) anadhihirisha kwamba nadharia ya Upembuzi ya Mao Tse Tug ni nadharia inayoshughulikia mambo matatu ambayo ni: Ubia wa migogoro, Upekee wa Migogoro na upembuzi wa migogoro. Anasisitiza kwamba nguzo kuu ya nadharia hii ni migogoro. Mao anaeleza dhana ya migogoro kwa kutumia miktadha mitatu tofauti lakini iliyo na mahusiano ya namna fulani. Miktadha hii ni: muktadha wa kihalisia, muktadha wa kijamii na muktadha wa kibinafsi au kimawazo. Kwa mujibu wa Mao, migongano hupatikana katika michakato yote inayopatikana ulimwenguni. Migongano hupatikana kila mahali lakini hutofautiana kulingana na vitu vinayohusika. Ili kuelewa mambo au maumbile, Mao anasisitiza kwamba, lazima tuchukulie kila kitu kuwa mchakato na kwa kuwa mambo hayo ni michakato, hubeba sehemu mbili – sehemu ya ndani na sehemu ya nje. Migongano ya ndani kwa ndani ya vitu hutumiwa kubainisha mahusiano ya vitu hivyo na vingine vya nje. Ni migongano ndiyo huendesha kila kitu katika ulimwengu huu.

Kwa mujibu wa Soo (1981), lengo kuu la Mao Tse Tung katika nadharia hii ni kubainisha migogoro katika jamii na jinsi ya kuisuluhisha. Kwake, migongano hurejelea uhusiano wa makundi mawili au matabaka mawili yanayohitilafiana. Anasema kuwa tatizo pia huchukuliwa kama mgogoro kwa kuwa ina mahusiano ya namna fulani ambayo hayana uwiano. Ili kufafanua nadharia hii vyema zaidi, Mao anabainisha mambo yafuatayo:

a) Kila kitu ulimwenguni huwa na migongano. Hivyo basi, bila ya kuwepo kwa migogoro hakuna kitu kinachoweza kuwepo ulimwenguni
b) Maisha ni migongano. Migongano hiyo inapoisha, maisha pia hufikia mwisho.
c) Kukana kuwepo kwa migogoro ni sawa na kukana kila kitu.
d) Tofauti zozote zilizopo katika jamii ni migogoro.
e) Tatizo lolote katika jamii ni mgogoro.
f) Changaoto zote zinazokabili hatua za kimaendeleo ni migogoro.

Iwapo patakuwa na migongano yoyote katika mchakato wowote ambayo haiwezi kusuluhishwa, basi mchakato huo utaangamia. Mabadiliko katika jamii hutokea kwa sababu ya migongano ya ndani kwa ndani katika jamii husika na migongano yenyewe husababisha michakato ya uzalishaji mali, matabaka na upya na uzee katika jamii. Kitu kipya kinapojitokeza katika jamii hutokeza migogoro mipya kwani kujaribu kuangamiza kilichokuwepo katika jamii na kwa njia hiyo mchakato wa migogoro unakuwa jambo lisilokwisha. Mihimili inayojenga nadharia hii na ambayo ilisaidia katika uchanganuzi ni:

1. Mhimili wa ubia wa migogoro katika jamii unasisitiza kwamba kukana kuwepo kwa migogoro ni kukana kila kitu. Katika kila jamii kuna mabadiliko ambayo hutokea mara kwa mara. Mabadiliko yanapotokea mambo mapya huzuka na yanapozuka huchukua nafasi ya mambo yaliyokuwepo hapo awali. Haya mabadiliko yanayozua mambo mapya huwa na migogoro yake ya ndani kwa ndani na hivyo michakato ya kutafuta suluhisho huanza na kuendelea hadi jambo jingine jipya linapotokea. Jambo hili hutokea katika kila jamii na kwa kila kitu.

2. Mhimili wa upekee wa migogoro katika jamii. Hii ina maana kuwa kila mgogoro una upekee wake unaoutofautisha na mgogoro mwingine. Kwa mujibu wa Mao, kila kitu huwa na mgogoro wa ndani kwa ndani unaotofautiana na migogoro mingine na jambo hili ndilo hutofautisha vitu mbalimbali. Ili kusuluhisha mgogoro wowote ule katika jamii lazima jambo linaloutofautisha na migogoro mingine libainike wazi. Katika kila mgogoro, kuna migogoro mingine midogo midogo ya ndani kwa ndani ambayo huchangia mgogoro mkuu. Mgogoro mkuu hubainika wazi zaidi huku migogoro mingine midogo inayoijenga ikichukua nafasi ya pili hafifu (uk. 59). Hivyo basi, ili kutatua mgogoro wowote ambao una migogoro mingine midogo midogo, ni muhimu kufanya kila juhudi kutambua mgogoro mkuu kwa sababu ndio huathiri na kuelekeza migogoro mingine midogo. Jambo hili likisha kutambuliwa inakuwa rahisi kutatua kila mgogoro.

3. Mhimili wa upembuzi wa migogoro katika jamii. Mhimili huu una vipengele vitatu ambavyo ni:
    a. Muungano wa mikinzano – ni kipengele kinachosisitiza kwamba katika kila mgogoro kuna migogoro mingine midogo ambayo lazima iungane ili kufanikisha mgogoro mkuu
    b. Kipengele cha ukamilifu wa mikinzano – ni hali ya migogoro mbalimbali kutegemeana na kukamilishana kiasi cha kwamba lazima pawe na mtagusano na mwingiliano wa vipengele mbalimbali vya migogoro ili mgogoro huo uweze kusimama. Kila mgogoro mdogo unakuwa ni sehemu inayokamilisha mgogoro mkuu

c. Kipengele cha mabadiliko ya migogoro – ndicho kipengele muhimu zaidi katika nadharia hii kwa sababu kinabainisha mabadiliko yote yanayotokea katika migogoro. Kwa kuwa kuna mabadiliko ya mara kwa mara kwenye migogoro, migogoro mipya hutokea kila mara hata baada ya migogoro ya awali kutatuliwa.

Utafiti huu uliegemezwa kwenye mihimili hii ya nadharia ya Upembuzi, ambayo ilifanikisha uchanganuzi wa migogoro ya kimawazo katika riwaya za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012) kwa njia zifuatazo:

a) Mhimili wa ubia wa migogoro katika jamii ulitumiwa kuchanganua namna migogoro ya kimawazo inavyoweza kuibua dhamira zinazopingana katika kila kitu wanachofanya wanajamii.

b) Mhimili wa upekee wa migogoro ulitumiwa kuchanaganua namna migogoro ya kimawazo inavyoweza kusaidia kukuza wahusika kwani upekee wa migogoro inayowakumba ilizingatiwa ili kutofautisha hulka zao na za wahusika wengine

c) Mhimili wa upembuzi wa migogoro ulitumiwa kuchanganua namna migogoro ya kimawazo ilivyowawezesha waandishi kusuka ploti zenye mshikamano mwema katika riwaya teule ikizingatiwa kwamba migogoro inapobadilika huwawezesha waandishi kusuka ploti zao kwa kushughulikia masuala mengi.

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inafafanua: mahali pa utafiti huu, muundo wa utafiti, kudhihirisha namna sampuli ilivyoteuliwa, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake na hatimaye kueleza jinsi matokeo yalivyowasilishwa.

### 1.9.1 Mahali pa utafiti

Utafiti huu ulijikita katika maktaba. Usomaji mpana wa riwaya hizi mbili – *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012) ulifanywa maktabani. Mtafiti alisoma kwa kina makala mbalimbali, tasnifu, majarida na vitabu vilivyoandikwa kuhusu mada hii ili kumsaidia katika uchanganuzi wake na mambo muhimu kuhusu mada kunakiliwa. Aidha, nadharia ya Upembuzi ya Mao Tse Tung (1937) ilitumiwa kuchanganulia data.

### 1.9.2 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti huu ni wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Murray (2003) muundo wa utafiti wa kimaelezo ni ule ambao data yake haichanganuliwi kitakwimu bali huchunguza sifa zinazobainika katika jambo linalochunguzwa. Katika utafiti huu, maelezo yalitolewa kuhusu namna migogoro ya kimawazo huweza kuathiri mahusiano ya wahusika na namna tabaka la malezi huathiri maingiliano ya kijamii na kuzua migogoro miongoni mwao huku ikiwasaidia waandishi kukuza ploti.

### 1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ya utafiti huu ilietuliwa kimakusudi kutoka kwa riwaya mbili za Kiswahili – *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012) Riwaya hizi ziliteuliwa kwa sababu mbili kuu. Kwanza hizi ni riwaya za kisasa na ambazo zimeandikwa katika karne ya ishirini na moja na hivyo basi zinaangazia masuala na matatizo yanayoshuhudiwa katika jamii ya sasa. Pili, riwaya hizi zina data muhimu kuhusu mada teule.  Aidha, wahusika wake wanaonyesha sifa changamano zinazomwafiki mwanadamu halisi.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Njia kuu ya kukusanya data katika utafiti huu ilikuwa kusoma riwaya teule kwa kina. Katika kusoma huku, mtafiti alinukuu sehemu ambazo migogoro hii ya kimawazo ilipojitokeza. Migogoro mbalimbali kama ile inayojitokeza akilini mwa *Mkamandume* baada ya kufyeka shamba lake; ilichanganuliwa kwa njia ya moja kwa moja na kuiainisha kulingana na mihimili ya nadharia ya Upembuzi. Aidha, maandishi mengine yaliyowahi kuandikwa hapo awali yalijumuishwa katika uchanganuzi wenyewe.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Data zilizokusanywa zilichanganuliwa kwa kuteua na kuhakiki sehemu za riwaya teule huku malengo ya utafiti yakitiliwa maanani, maswali ya utafiti na nadharia ya Upembuzi. Katika uchanganuzi wenyewe, migogoro ya kimawazo ilichunguzwa kulingana na mihimili ya nadharia iliyochaguliwa ili kutimiza malengo ya utafiti.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Data zilizokusanywa ziliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia sura mbalimbali. Malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya Upembuzi ndiyo ilikuwa dira iliyoongoza uwasilishaji wenyewe.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii imewasilisha mambo ya kimsingi yaliyobainishwa katika utafiti huu. Mambo yaliyozungumziwa ni pamoja na: suala la utafiti, malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada. Vilevile, misingi ya nadharia pia imewasilishwa, yaliyoandikwa kuhusu mada teule na mipaka au upeo wa utafiti. Mbali na hayo, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli pamoja na namna ya uwasilishaji wa data zimeshughulikiwa ipasavyo. Sura

inayofuata ilishughulikia namna migogoro ya kimawazo ilivyoibua maudhui mbalimbali katika riwaya teule.

# SURA YA PILI

# MIGOGORO YA KIMAWAZO NA NAMNA INAVYOIBUA DHAMIRA NA MAUDHUI KATIKA RIWAYA TEULE

## 2.1 Utangulizi

Lengo la sura hii ni kubainisha namna migogoro ya kimawazo inavyoweza kuibua dhamira na maudhui mengi yanyokinzana katika riwaya. Sura hii imebainisha kuwa chanzo cha maudhui na dhamira zinazopingana katika riwaya ni migogoro ya kimawazo. Lengo hili lilitimizwa kwa kuchanganua riwaya mbili za Kiswahili: *Mkamandume* (2013) Said A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2012) Wamitila K. na vilevile kurejelea utafiti wa kitaalamu ambao umewahi kufanywa hapo awali. Kwa mujibu wa Morreti (2006), kama ilivyo na tamthilia za tanzia na mighani, riwaya huonyesha uhusiano uliopo baina ya binadamu na mazingira yake. Anaongeza kusema kwamba katika mighani mashujaa wa hadithi huhusishwa zaidi na miji au vijiji vyao huku katika tanzia majaliwa ya wahusika wakuu huweza kutabirika. Wahusika wakinzani katika riwaya hudhihirishwa vyema zaidi na mikinzano inayodhihirika kati ya wahusika hao na jamii zao.

Riwaya ndiyo utanzu wa fasihi unaobainisha uhusiano uliopo baina ya wahusika na maadili ya kijamii pamoja na mikinzano inayotokana na uhusiano huu. Swali kuu analouliza Morreti ni iwapo suala la maadili lina umuhimu wowote ulimwenguni na iwapo upo, mbona kuna tofauti kubwa kati ya maadili hayo na tabia za binadamu? Kwa kuzingatia maoni haya, sura hii ilitumia mhimili wa nadharia ya Upembuzi unaosisistiza ubia wa migogoro kufafanua dhamira zinazopingana katika riwaya hizi. Kwa mujibu wa mhimili huu, migogoro hujitokeza mara kwa mara katika kila jamii hata baada ya migogoro ya zamani kutatuliwa. Hivyo basi, kukana kuwepo kwa migogoro ni kukana

kila kitu. Ufatiti huu ulitumia mhimili huu kudhihirisha kwamba migogoro ya kimawazo ndiyo huibua maudhui yanayopingana ili kuleta migogoro ya aina nyingine yoyote katika jamii zote. Kabla ya kuchunguza namna migogoro ya kimawazo ilivyoibua dhamira na maudhui katika riwaya husika, sehemu mbili zifuatazo zinatoa muhtasari wa riwaya mbili teule.

### 2.2.0 Muhtasari wa *Mkamandume*

Kama anwani ya riwaya inavyoashiria, riwaya hii inahusu mhusika kwa jina Mkamandume. Mhusika huyu anapatwa na ukomo unaomziba kinywa na kupata ukimya wa milele. Anabakia kuwasiliana na jamii yake kwa ishara na minong'ono yake ya ndani kwa ndani. Familia ya Mkamandume ni familia ya watu wanane: Mkamandume mwenyewe; mkewe Tufaa na wanawe sita: Time, Viwe, Msimu, Mtumwa, ki-Katija na kaka yao Fikirini. Riwaya hii ina sura hamsini na nane ambazo zimetumiwa kuangazia maisha ya Mkamandume pamoja na familia yake. Mkamandume anavyozidi kuwazia namna maisha yake ya awali yalivyokuwa na namna yalivyo sasa anazidi kukereka ndani kwa ndani na kujilaumu mwenyewe huku akijutia maovu aliyoyatekeleza kwa kisingizio cha kutafuta uhuru wa kweli katika nchi yake ya Malelejimema. Anapowazia namna alivyowaua watu kwa kuwafyeka vichwa ilhali wengi wao hawakuwa na hatia hata kidogo, anajawa na simanzi na kutiririkwa na machozi. Mkamandume alikuwa na matumaini makubwa kuhusu nchi yake ya Malelejimema. Jambo hili lilimfanya apigane kufa kupona ili kuwaondoa wakoloni.

Mkamandume aliamini kwamba watu ambao hawakuwa wenyeji wa Malelejimema au wenyeji walioonyesha dalili zozote za kuwahurumia Wakoloni, walipaswa kuangamizwa. Hata hivyo baada ya Wakoloni kuondoka, hali ya unyanyasaji inaishia kuwa mbaya zaidi

kwani hata kazi alifanya kwa muda mrefu zaidi bila kupokea mshahara. Mazingira yaliharibiwa na mashamba hayakuzalisha mazao tena. Maisha yakawa magumu zaidi. Mkamandume anapogeuka nyuma na kutazama ni wapi atokako, haoni chochote ila tarihi ya nchi yake inayoendelea kufunikwa na giza. Tarihi hii ndiyo hadithi yake na watu wake. Mkamandume aliyekuwa buldoza, mtukutu, shujaa na mfyeka vichwa vya watu aliyepigania haki amebakia kuwa gofu la mtu. Kumetokea nini hata Mkamandume hawezi tena kukitegua kitendawili kinachomhusu na jamii yake?

Swali hili ndilo linalomsumbua sana Mkamandume kiasi cha kuzua migogoro katika mawazo yake. Migogoro hii ya kimawazo inaonekana kumwathiri kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, katika familia yake, anaonekana kuwa mtu mwenye ulimwengu wake kivyake. Haongei na yeyote tena, hawasaidiani tena na mkewe Tufaa kuchuma na kushauriana kuhusu mambo mbalimbali yanayoathiri jamii yao. Watoto wao nao wanaishia kupuuzwa na kudhulumiwa. Kwa mfano, Time anapomkabili babake kuhusu kufyeka shamba lao la mihogo, babake anamtumbulia macho tu. Vilevile, Time anahisi kaonewa kwa sababu babake alikataa posa ya mchumba wake; Soud. Mbali na famiilia yake, migogoro yake ya kimawazo iliharibu uhusiano kati yake na wanajamii wengine kama vile kijana Kombo ambaye alimheshimu na kumnunulia chai kila siku lakini yeye akachukulia kuwa huko kulikuwa kudhalilishwa.

Hatimaye inakuja kumbainikia kwamba wananchi aliowadhulumu kama vile Bwan Sleyyum, wazazi wake Soud na Mzee Mkasi hawakuwa maadui wa maendeleo na wasaliti kama alivyowafikiria hapo awali bali maadui wa maendeleo walikuwa viongozi kama Bosi wake ambao walitokea kupora mali ya umma na kuwadhulumu wananchi bila

huruma. Mkamandume anapogundua hivyo anaamua kujiunga na kundi la wanaharakati wa kupigania haki za wanyonge lililoongozwa na Soud Nadia na Viwe. Hata hivyo, anakuja kuuawa kwa kumiminiwa risasi wakati wa maandamano.

Haya yote yanathibitisha kwamba, migogoro yote inayojitokeza katika jamii ya Walelejimema, isingedhihirika endapo wahusika wakuu kama Mkamandume wasingekuwa na migogoro ya ndani kwa ndani ambayo ndiyo inakuja kuzalisha migogoro mingine mikuu katika jamii hii. Migogoro hii ilikuwa imetishia kuisambaratisha jamii ya Malelejimema kwani kila mwanajamii alitaka kupata utatuzi wake binafsi. Kwa mujibu wa Eldridge (2008) ni jambo la kawaida kwa binadamu kujitambua kabla ya kuwatambua wanajamii wengine walio katika mazingira yake. Aghalabu, binadamu huweka matakwa yake mbele bila kuwafikiria wengine. Jambo hili linapotokea jamii haiwezi kujiepusha na migogoro ya mara kwa mara kama ilivyoshuhudiwa katika jamii ya Walelejimema. Vivyo hivyo, McClinton-Temple (2011) akimnukuu Northrop Frye anasema kwamba migogoro katika mawazo ya mhusika hasa yale yanayotokea kupinga mawazo ya jamii, humfanya mhusika kama huyo kujitenga na jamii yake. Jambo hili linaonekana kutokea katika hadithi ya *Mkamandume* kwani baada ya kutekeleza maovu ya kuwafyeka watu vichwa, Mkamandume anajitenga na jamii katika kila kitu alichokifanya. Anatokea kuwa katika ulimwengu wake binafsi hasa anapopanda katika ule mti wake wa hadithini (uk. 460).

### 2.3.0 Muhtasari wa *Unaitwa Nani?*

Hii ni riwaya yenye wahusika wakuu wawili; mwanamke (Kasekesi) na mwanamume (Mumbo). Wahusika hawa wamesawiriwa kupitia kwa nafsi za watu mbalimbali wa kike

na kiume. Riwaya hii imegawanywa katika sehemu mbili zinazolingana; sehemu ya kwanza imeangazia nafsi ya kike na sehemu ya pili inazungumzia nafsi ya kiume. Wahusika hawa wamelazwa hospitalini wakiwa mahututi. Hawakumbuki jambo lolote kuhusu asili zao ila tu jinsia zao. Katika sehemu ya kwanza kuna visa vitano vya wanawake mbalimbali ambao madhila waliyoyapitia mikononi mwa wanaume yanaonyesha mgogoro uliopo baina ya mwanamume na mwanamke na ule uliopo baina ya mwanamke na utamaduni kwa jumla. Kisa cha kwanza kinamhusu msimulizi (Kasekesi). Anatanguliza masimulizi haya kwa kuonyesha namna alivyolazwa hospitalini akiwa mahututi. Hakuna analokumbuka ila jinsia yake. Anaendeleza kisa hiki kutueleza maisha yake ya awali. Kasekesi aliingizwa katika ndoa na mwanamume mmoja kwa jina Agusto akiwa angali na umri mdogo sana. Mambo yalimwendea sawasawa hadi Agusto alipofilisika na kuanza kunywa pombe kupindukia. Baadaye, Agusto anakufa na jamaa zake kumsingizia Kasekesi kuwa ndiye aliyemwibia mali yake na hatimaye kumuua.

Kisa cha pili ni cha Mwanamuka aliyeolewa na Kitonga. Aliolewa na Kitonga baada ya kukosa pesa za kulipia karo. Kitonga anamlipia mbuzi watatu tu kama mahari na Mwanamuka anapokosa kushika mimba mumewe anamwoa kijakazi wao. Kisa cha tatu kilikuwa cha Nyakor ambaye alisoma hadi kupata shahada ya uhandisi. Anapoolewa, mumewe anakuja kumtaliki kwa kuwa alihisi kwamba Nyakor alimdharau kwa sababu ya kisomo chake.

Kuna visa vingine viwili vya Zahra na Kamene ambao wote pia wanapitia dhuluma mikononi mwa wanaume kwa kushikilia mawazo yaliyokinzana na yale ya wanaume. Zahra alikuwa yatima aliyelelewa na babu na nyanya yake ambao walijitahidi kumlea

kwa maadili ya kijamii na kidini. Walimpeleka katika madrasa alikobakwa na mwalimu wake wa dini. Babu yake alipotafuta haki kwa kuripoti kisa hiki kwa chifu, hakuna hatua inayochukuliwa kwani aliyembaka Zahra alikuwa mwana wa kigogo mmoja mwenye uwezo mkubwa na chifu aliogopa kumchukulia hatua kwani angepoteza kazi yake huku akiwa amebakisha miezi michache tu kustaafu. Baadaye, Zahra, nyanyake na babu yake wanahamishiwa nchi nyingine kwa lazima kwa kisingizio cha kuwepo nchini bila kibali. Kamene naye alikataliwa na babake tangu alipozaliwa kwani babake alitarajia mtoto wa kiume lakini akatokea kuwa wa kike.

Sehemu ya pili ya riwaya hii inahusu namna jinsia ya kiume inavyonyanyaswa na jinsia ya kike. Sehemu hii inatangulizwa na mwanamume aliye mahututi. Hawezi kukumbuka chochote ila tu kuwa ni mwanamume. Anazomewa na kundi la wanawake ambao anaamini kwamba ni wauguzi na madaktari. Katika sehemu hii, mwandishi amewatumia wahusika mbalimbali wa kiume kuonyesha mgogoro uliopo baina ya wanaume na wanawake. Kwanza, msimulizi (Mumbo) anatueleza namna mke wa ami yake alivyomwendea mumewe kinyume na kula uroda nje ya ndoa na Kasu (mchimba vichuguu kijijini). Aidha, anatueleza namna mke wa mzee wa kanisa alivyofanya mapenzi kichakani na mhubiri usiku wa kuamkia mwaka mpya. Mumbo naye anapooa, anaishi kwa amani na mkewe hadi anapopoteza kazi. Hapo ndipo migogoro ya kila siku haikuisha nyumbani kwao. Hatimaye, wanaachana na mkewe ambaye anatoweka na watoto.

Kisa kingine kilimhusu Kaminda Mwana–a–Pasta. Yeye alikuwa mwadilifu hadi alipopata kazi na baadaye kulaghaiwa na mwanamke mmoja kwa jina Sasi na bila

kufahamu akajipata katika ndoa. Baadaye, anakuja kugundua kwamba, Sasi alikuwa na mtoto wa kike aliyemficha kwa nyanyake. Mzozo wao ukaanzia hapo na kuwa mbaya zaidi kiasi cha Sasi kutaka kumuua Kaminda alipokuwa akilala. Kwa bahati nzuri, Kaminda ananusurika na kutoroka asirudi kwake tena.

Kisa kingine ni cha Wamae aliyekuwa kijana maskini aliyeliwa na funza miguuni lakini kwa msaada wa madaktari wa *'M'edicins Sans Frontieres'* akapona. Baadaye alipopita mtihani, alikosa karo ya kuendea shule ya sekondari. Alitafuta msaada kutoka kwa mbunge wao Bwana Atiriri lakini akakosa. Baadaye, alianzisha biashara iliyonawiri vyema na kuwa tajiri. Alipomwajiri Betty kama msaidizi wake hakugundua kwamba huyu ndiye aliyekuwa katibu muhtasi wa Bwana Atiriri. Matatizo yake yakaanza alipoamua kumwoa Betty na kujiingiza katika siasa. Anakamatwa na kufungwa gerezani kwa tuhuma za kuwafadhili magaidi. Mkewe anatoweka na anapotoka jela anabakia kuwa maskini hohehahe kwa mara nyingine. Vivyo hivyo kuna visa vingine vya Sir Pipo na Purupesa ambao pia wanadhulumiwa na wanawake. Hatimaye msimulizi anamaliza kwa kisa cha Mheshimiwa Kasina Usina Sini. Kisa hiki kinathibitisha kuwa hakuna mwanamke hata mmoja aliye mwaminifu katika ndoa.

### 2.4.0 Migogoro ya Kimawazo, Dhamira ya Mwandishi na Maudhui Katika Riwaya ya *Mkamandume*

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), migogoro ni mivutano inayokuwa kati ya mhusika mmoja na mwingine katika kazi ya fasihi au katika akili ya mhusika mmoja na huchukua sehemu kubwa ya usimulizi wowote ule wa fasihi. Amebainisha namna migogoro mbalimbali inaweza kujitokeza katika kazi za fasihi. Kwanza, anasema kuwa panaweza

kuwa na migogoro kati ya mhusika fulani na nguvu au kani nyingine au mhusika mwingine. Pili, mivutano hiyo inaweza kuwa kati ya mhusika na jamii kwa jumla. Na tatu, migogoro inaweza kuwepo kati ya mhusika na nguvu nyingine za nje. Utafiti huu uliegemea zaidi sehemu ya fasiri hizi inayosisitiza kuwa migogoro ni mivutano inayojitokeza akilini mwa mhusika. Sura hii ilitumia nadharia ya Upembuzi ya Mao Tse-Tung (1937) kudhihirisha kwamba maudhui mengi katika riwaya ya Kiswahili huibuliwa na migogoro ya kisaikolojia.

Kwa mujibu wa Soo (1981), nadharia ya upembuzi ya Mao Tse-Tung ina mihimili mitatu: ubia wa migogoro, upekee wa migogoro na upembuzi wa migogoro. Sehemu hii ya utafiti iliegemezwa zaidi kwenye mhimili wa ubia wa migogoro ili kuchanganua namna migogoro ya kimawazo ilivyowawezesha waandishi kuibua maudhui mbalimbali na kufikia dhamira zao. Mhimili huu unasisitiza kwamba katika kila jamii kuna migogoro ambayo hutokea mara kwa mara. Migogoro itokeapo, mambo mapya huzuka na kuchukua nafasi ya mambo ya kale.

Mabadiliko haya yanayozaa mambo mapya, huwa na migogoro yake ya ndani kwa ndani na hivyo basi mchakato wa kutafuta suluhisho huanza na kuendelea hadi jambo jingine jipya linapotokea. Jambo hili hutokea katika kila jamii. Kwa kuegemea mhimili huu wa ubia wa migogoro, sehemu hii ilichunguza migogoro katika miktadha miwili. Muktadha wa kibinafsi na muktadha wa kijamii. Ukweli wa mhimili huu ulidhihirika katika jamii ya Walmaelejimema kwani palikuwa na migogoro kati ya Wakoloni na Wamalelejimema. Mgogoro wenyewe ulitokana na visa vya dhuluma dhidi ya Wamalelejimema kama vile unyakuzi wa mashamba, kunyimwa haki ya kumiliki mali na kunyimwa elimu

iliyowafaa. Haya yote yalitokea wakati wa ukoloni na Walelejimema wakaamua kwamba wasingekaa na kutazama unyanyasaji huo ukiendelezwa. Kwa hivyo waliamua kupigania haki zao.

Mgogoro huu ulisababisha umwagikaji wa damu ambao ulihusisha hata mauaji ya badhi ya Wamalelejimema waliofikiriwa kuwa watetezi wa utawala wa kidhalimu wa wakoloni. Baadhi ya Walelejimema waliouawa ni pamoja na wazazi wake Soud; Bw. na Bi. Aziz Kindy na nyanyake Nadia. Mgogoro huu unaendelea kwa muda mrefu na suluhisho lake linapatikana tu baada ya Wakoloni kuondoka na kuwapa Wamalelejimema uhuru wa kujitawala. Hata hivyo, kama mhimili wetu unavyosisitiza kwamba migogoro mipya huchipuza baada ya ile ya zamani kusuluhishwa, migogoro mipya inajitokeza katika jamii mpya ya Wamalelejimema. Migogoro hii kwanza inachipuza mawazoni mwa baadhi ya wahusika kama vile Mkamandume na kusababisha migogoro mbalimbali inayojitokeza katika riwaya. Kwa mfano, kuna migogoro inayojitokeza mawazoni mwa Mkamandume:

> "Kwa vyovyote vile, kila mtu siku hizi hubeba msalaba wake. Hakuna cha baba wala cha mama; cha mtoto wala kinying'nya … Aaa niseme nini? Labda mwanzo na mwisho ni moja." (uk. 1)
>
> "Nani kabadilika katika kiini cha maisha yetu? Yaani sisi. Mtindo ni ule ule wa waamba ngoma. Kila mtu huvutia kwake. Lakini waamba ngoma wa sasa ni wa rangi ya aina nyingine. Weusi. Wao wanavuta bila hisia wala imani. Wanavuta kwa nguvu mno mpaka ngoma inararukiana… Maisha ya Malelejimema sasa yanapangwa kwa maneno matupu. Ukikosa maneno kwa ombaombo" (uk. 6)

Migogoro hii yote imemsaidia mwandishi kukuza maudhui mbalimbali. Maudhui haya ni pamoja na: uharibifu wa mazingira, dhuluma dhidi ya raia, ukiukaji wa haki za watoto, tama na kadhalika.

### 2.4.1 Uharibifu wa Mazingira na Athari Zake

Kupitia kwa mawazo ya Mkamandume, mwandishi anakuza maudhui ya uharibifu wa mazingira. Uharibifu huu ndio ulifanya mashamba yasiwe na mazao ya kuridhisha. Mkamandume, alifahamu kwamba Malelejimema ilikuwa nchi nzuri ya kusetiri mahitaji ya kila mmoja. Hata hivyo, mambo yamebadilika na sasa kuna Wamalelejimema wanaolala na njaa kwa sababu mazingira yameharibiwa na mashamba hayatoi mazao tena (uk. 6). Anasema kwamba ingawa kulikuwa na maudhi kadhaa, Malelejimema haikufikia kiwango cha watu wenyewe au serikali yao kupita wakiombaomba lakini leo mazingira yameharibiwa na anaiita Malelejimema bahari kame. Ndiyo maana Mkamandume anawaza:

> "Itazame Malelejimema leo – bahari kame. Ndiyo ukame mkubwa ulikuwa jana. Leo haupo tu, umetawala." (uk. 6)

Jambo hili linamghadhabisha sana Mkamandume na kumfanya afyeke migomba na mihogo aliyokuwa nayo shambani. Jambo hili pia linazua mgogoro kati yake na bintiye; Time. Ingawa migomba hiyo haikuzalisha mazao mengi, palikuwa na angalau matumaini kidogo kwa familia ya Mkamandume. Ufyekaji huu unaotekelezwa na Mkamandume mwenyewe unakuwa dhuluma kubwa kwa familia yake kwani baada ya hapo familia yenyewe haikuwa na matumaini yoyote kuhusu namna ingeweza kupata chakula. Hii ndiyo sababu Time anamkabili Mkamandume na kumuuliza:

> "Umefanya nini ile konde ya muhogo na migomba? Hata … hata mavuno machache yangesaidia kusukuma siku mbele, enh baba enh!" (uk. 46)

Migogoro ya kimawazo inayojitokeza katika akili ya Mkamandume inamfanya afyeke shamba lake zima asibakishe chochote. Kulingana na Mkamandume, ni vigogo wa

kisiasa ndio wanapaswa kulaumiwa kwani ndio waliokata miti yote kiasi cha nchi yao kubakia bila mvua na kuwaacha watu wakiteseka wasijue la kufanya. Mambo haya yanatokea kuwa kinyume kabisa na waliyoyatarajia walipokuwa wakipigania uhuru. Hata hivyo, Mkamandume anazua mgogoro ndani ya mawazo yake baada ya kufyeka shamba lake. Dhamiri yake inamwadhibu na anaanza kujutia tendo lake punde tu anapomaliza kufyeka shamba hilo. Haya yanadhihirika anapowaza:

> "Ndiyo nini? Kitu gani umefanya Mkamandume? Umetatua tatizo kwa kulitatiza tatizo? Kumesaidia nini kufyeka kila kitu kondeni mwako? Umezidi kuikata tamaa yako. Umeongeza njaa na shida juu ya nafsi yako na nafsi za waliomo katika ukoo wako!" nayo sauti nyingine inamjibu "Si ndivyo ulivyoniamrisha nifanye – sasa?" (uk. 25)

Mbali na kwamba mgogoro huu wa kimawazo umemsaidia mwandishi kukamilisha maudhui haya ya uharibifu wa mazingira, mgogoro huo pia umemsaidia kukuza maudhui ya majuto kwa upande wa Mkamandume. Kukamilishana huku kwa maudhui kwa sababu ya migogoro ya kimawazo kuliwezekana tu kwa sababu kulikuwa na uhusiano kati ya mawazo ya wahusika wanaotumiwa na mazingira yao. Firth na Lindsay (2016) wakirejelea uchanganuzi wa Biblia kwa mujibu wa Polzin (1974) wanasema kwamba pana migogoro ya kimawazo inayoweza kujitokeza kwa sababu ya imani na tajriba ya mtu. Tajriba ya mtu kuhusu maisha inaweza kumpa imani fulani kuhusu mazingira yake na iwapo patakuwa na mabadiliko katika mazingira hayo ambayo yatapinga imani aliyoijenga hapo awali, mgogoro wa kimawazo unaweza kuzuka akilini mwake. Wanathibitisha haya kwa kumrejelea Ayubu alivyobadilikiwa na mambo kiasi cha kujawa na shauku akilini mwake kuhusu imani yake ya awali kumhusu Mungu. Haya ndiyo yanayompata Mkamandume kwani tajriba yake ya awali kuhusu Malelejimema ilimfanya kujenga imani kwamba Malelejimema ingekuwa nchi nzuri baada ya Wakoloni

kuondoka. Hata hivyo, Wakoloni wanapoondoka, imani yake haitimii; jambo linalomvuruga akili na kuzua mgogoro mkubwa zaidi akilini mwake hata asiweze kuukubali uhalisia unaojitokeza.

### 2.4.2 Dhuluma Dhidi ya Raia

Mwandishi amefaulu kukuza maudhui ya dhuluma dhidi ya raia kupitia kwa mawazo ya Mkamandume. Kuna aina mbalimbali za dhuluma zinazoendelezwa dhidi ya wananchi. Dhuluma hizi ni kama vile mauaji, unyanyasaji wa wafanyakazi, unyakuzi wa mali ya umma huku wananchi wakiachwa kujifia kwa njaa na ukosefu wa huduma muhimu kama matibabu na kadhalika. Kupitia kwa mawazo ya Mkamandume, tunapata kwamba viongozi hawatambui juhudi wanazozifanya wafanyakazi. Suala la kuwatambua na kuwatuza wafanyakazi linapojitokeza, wale wafanyakazi wafanyao kazi kwa bidii hawatambuliwi. Badala yake, tuzo hutolewa kwa mapendeleo na kuwazawadia wazembe wasiofanya kazi ipasavyo. Ni Mkamandume ndiye aliyefanya kazi kwa kujituma lakini wakati wa kutoa zawadi unapowadia, ni Bi. Zuhura Saleh ndiye anayetuzwa. Ingawa huyu alituzwa, alikuwa mzembe kazini ambaye alifika kazini kuchelewa (uk. 25).

Soud naye ana migogoro ya mawazo kuhusu namna unyanyasaji unavyoendelezwa katika nchi ya Malelejimema. Anasononeka kwa kuona namna watu walivyonyanyaswa. Kwa mujibu wa Soud, watu wote wana haki ya kupata elimu, haki ya kuchagua na kuchaguliwa, haki ya kufanya kazi na kuweza kuzitunza aila zao na kadhalika. Anasema kwamba maporomoko yanazuka katika jamii kwa sababu ya haki zisizo haki na uhuru usio uhuru. Ni uhuru wa magazeti tu, redio na televisheni. Uhuru wa kisiasa ambao hutumiwa na wanasiasa wa nchi kubwa kuhalalisha ubovu wa mfumo wao unaokwenda

kinyume na maumbile ya mwanamke na mwanaume (uk. 287). Soud anaghadhabishwa na namna ulafi na tamaa zilivyokithiri katika nchi ya Malelejimema. Kuna watu wanaonyakua kila kitu na kuvitumia kwa njia ya kibadhirifu. Kila mtu ana ubinafsi. Anataka kutumia kingi kuliko inavyostahili huku wengine hawapati hata kidogo. Haya yanawekwa wazi na mwandishi kupitia kwa mawazo ya Soud ifuatavyo:

> Alianza kufikiri. Kiu ya kutaka kuridhisha chagizo zisizoridhishika. Wingi wingi wingi. Chukua chukua chukua. Kusanya kusanya kusanya. Pika pika pika. Pakua pakua pakua. Tumia tumia tumia. Kila mtu anataka kuvuka mpaka kwa kupata ingawa wengine hawapati hata kidogo (uk. 289).

Mbali na hayo, kupitia kwa mawazo ya Mkamandume, tunapata kuona baadhi ya dhuluma walizotendewa Wamalelejimema wakati wa vita vya uhuru. Wengi wao walifyekwa vichwa na Mkamandume pamoja na rafiki yake Suguru. Mkamandume anapigana na nafsi yake ili asiyakumbuke waliyoyatenda na rafiki yake Suguru lakini kumbukumbu zake zinamrudisha nyuma na kumwonyesha namna Suguru alivyovunja milango na kuwatoa watu wote nje na kuanza kuwafyeka vichwa mmoja baada ya mwingine mpaka watoto wachanga akisema kwamba *Mtoto wa shetani ni shetani* (uk. 413)

Aidha, mawazo ya Mkamandume yanadhihirisha dhuluma alizotendewa Mzee Mkasi kupitia kwa uchochezi wake Mkamandume. Mzee Mkasi hakuwa na hatia ila Mkamandume alimwona kama msaliti kwa kuwa alikataa kushirikiana na Waafrika wenzake kutetea nchi yao (uk. 375). Hata ingawa Mkamandume na wenzake walipigana kufa na kupona kwa sababu ya uhuru wao, viongozi wa baada ya uhuru waliendeleza dhuluma za kijamii kwa kunyakua mashamba ya wachochole wasio na nguvu na hata

kuwanyima haki zao mbalimbali. Watu kama hao ndio waliowakilishwa na Soud mahakamani na kujaribu kupigania haki hizo walizonyimwa na wenye nguvu. Mwandishi anasema:

> Wengine walikuja chozi kifuani wakimwomba asimame nao kudai nao haki zao zilizofisidiwa na wakubwa wenye nguvu za kubadilisha haramu kuwa halali (uk. 134).

Mzee Mkasi anamsimulia Time namna binadamu ameweza kumdhulumu binadamu mwenzake kwa msingi wa rangi. Waafrika waliwachukia Wazungu nao Wazungu wakawachukia Waafrika. Palikuwa na shauku miongoni mwa Wahindi na Wazungu. Waarabu na Wayahudi hawakuaminiana. Mzee Mkasi anasikitika kwamba hata baada ya watu kupigana na kumwaga damu, kwa kisingizio cha kutafuta uhuru, bado unyanyasaji unaendelezwa na Waafrika wenyewe. Watu walidhulumiana na kuchukiana wao kwa wao wakisema ni utetezi wa haki. Kabla ya uhuru makundi yalijitokeza mawili. Kuna kundi la wale waliojiita wenyeji wa Malelejimema na wale walioonekana kama wageni ingawa nao walizaliwa Malelejimema kama vile babake Soud. Makundi haya mawili yalipambana na kuendeleza uovu miongoni mwao. Hata baada ya uhuru. Mkamandume amepoteza hisia zote kwa mkewe. Haya yalitokea kwa sababu alinyanyaswa kotekote. Mshahara anaoupata haumtoshelezi kitu.

Kudhulumiwa kwa wafanyakazi pia kunajitokeza katika shamba la babake Soud. Babake Soud aliwadhulumu wafanyakazi wake kwa kuwatishia kila mara. Hata hakutaka wawe na uhusiano wa aina yoyote na mtoto wake, Soud, ambaye aliwapenda wafanyakazi hao kwa dhati. Mauaji katika nchi hii ya Malelejimema yalikuwa mambo ya kawaida. Soud

naye anasononeka kwa sababu ya wazazi wake kuuawa. Haya yanadhihirika kwa uchungu alio nao:

> Haumii? Nani kasema haumii kwa kuuliwa babake na mamake? Kwa nini asiumie? … Lakini nani katika nchi hii asiyegegenwa moyo kwa sababu hii au ile kama si kwa hili jingine? Huyu kafanywa hili, yule kafanywa lile, huyu ana njaa, huyu ana kiu, huyu mgonjwa anaumwa wala hapana matibabu wala dawa (uk. 302).

Mambo haya yote yanadhihirika kupitia kwa mawazo ya wahusika mbalimbali kama vile Mkamandume, Soud, Mzee Mkasi, Sunguru na kadhalika. Ni dhahiri kwamba mwandishi ameweza kukuza maudhui ya dhuluma dhidi ya wananchi (ambayo ndiyo yaliyobeba ujumbe wake mkuu) kupitia kwa migogoro ya kimawazo. Maudhui ya dhuluma dhidi ya wananchi yamepewa nafasi kubwa zaidi katika riwaya hii. McClinton-Temple (2011) anasisistiza kwamba ni jambo la kawaida kwa binadamu kukwepa mateso. Watu hujaribu kukwepa matatizo ya wengine kwa sababu ya kuogopa kuteseka pia. Jambo hili linadhihirika kupitia kwa Soud ambaye anakwepa kuuawa baada ya kuarifiwa na wazee.

### 2.4.3 Ukiukaji wa Haki za Watoto

Maudhui mengine ambayo yanadhihirishwa kupitia kwa migogoro ya kimawazo ni ya ukiukaji wa haki za watoto. Watoto, hasa mabinti, hawapewi fursa ya kujiamulia wachumba wao. Mfano mzuri ni Time anapokatazwa na babake (Mkamandume), kuolewa na Soud. Mkamandume hakuwa na sababu yoyote ya kumkataza Time kuolewa na Soud ila tu kwamba Soud alikuwa mtoto wa adui yake wa jadi tokea enzi za ukoloni. Sababu nyingine iliyomfanya Mkamandume kupinga ndoa hiyo ilikuwa imani yake kwamba asili ya Soud haikuwa pale Malelejimema bali mababu zake walikuwa wageni katika nchi hiyo. Hilo tu ndilo lilimfanya ambague Soud.

Jamii ya Walelejimema iliwadhulumu watoto wasichana kwani ndio tu waliotarajiwa kujitunza na kuhakikisha kwamba hawakujiingiza katika mapenzi nje ya ndoa. Iwapo jambo hili lingetokea na mimba ipatikane, ni mtoto wa kike ndiye tu aliyelaumiwa na kuachiwa mzigo wote wa kupambana na utamaduni uliomkandamiza bila huruma. Haya yanadhihirika kupitia kwa Viwe. Viwe anapopata mimba, yule mvulana (Bete) aliyemringa mimba hiyo haonekani popote. Ni Viwe tu anaachiwa mzigo huo kuubeba mwenyewe. Utamaduni haukumruhusu msichana asiye katika ndoa kupata mimba na hata mamake msichana anayepata mimba nje ya ndoa pia hubebeshwa mzigo ambao haumhusu hata kidogo. Haya yanadhihirika mamake Viwe anaposema:

> Aaa, umeshaharibu maisha yako na yangu … nyumba nzima itaripuka akijua babako asiyejua kuambizika wala kusemezeka – hasa kwa jambo hili (uk. 99).

Kupitia kwa mawazo ya Soud pia tunabaini kwamba babake alikiuka haki za watoto kwa kuwaajiri na kuwatesa sana. Aliwafanyisha kazi kama punda. Mwandishi anasisitiza hili kupitia kwa mawazo ya Soud yanayoturudisha nyuma na kusema:

> Mara Kinda kaokote kuni. Kachote maji kisimani. Kachume mashelisheli shambani. Kang'oe muhogo, Kinda osha vyombo. Kafue Kinda. Kachume mafenesi uuze. Halafu kaanike karafuu uwanjani. Mradi Kinda, Kinda, Kinda … Na aliposita kofi, alipozubaa kibao, alipokosea fimbo (uk. 221).

Soud alitofautiana na wazazi wake kimawazo kuhusu utabaka na namna walivyomtesa Kinda. Anamkabili mamake na kumwambia kwamba Kinda si mnyama; ni binadamu kama wao. Mamake anamjibu kwa kumweleza kuwa binadamu wote hawakuumbwa sawasawa na kwamba ni wazi kwamba kuna tofauti kubwa baina yao na akina Kinda. Wao walikuwa Waungwana na Kinda ni Mswahili. Na hiyo ilikuwa tofauti kubwa. Hiyo ndiyo maana wazee wake walimleta kwa akina Sound kwa kuwa walishindwa kumlea.

Vilevile, maudhui haya yanaendelezwa kupitia kwa mawazo ya Mkanandume anapokumbuka wakati walipopigana vita vya uhuru walivyowafyeka watu vichwa. Anakumbuka namna rafiki yake Sunguru alivyovunja milango ya watu na kuwatoa walimojificha pamoja na watoto wao. Aliwafyeka vichwa bila ya kuwajali hata watoto kwani aliamini kwamba mtoto wa shetani ni shetani.

**2.3.4 Unyanyasaji wa Kijinsia**

Katika jamii ya Wamalelejimema, wanawake wanadhulumiwa na kunyanyaswa kwa msingi wa kijinsia. Unyanyasaji huu unadhihirika kwa kuzingatia mawazo ya Bi. Tufaa ambaye anaingiwa na wasiwasi bintiye Viwe anapopata mimba nje ya ndoa. Siri ya Viwe kuwa mjamzito inapofichuka, Tufaa anaingiwa na wasiwasi na kuzua mgogoro nafsini mwake kuhusu namna mumewe angemchukulia baada ya kugundua kwamba Viwe alikuwa mjamzito lakini Tufaa akaificha siri hiyo. Ni unyanyasaji huo wa kijinsia ndio unamfanya Bi. Tufaa kutafuta njia za kutumia kuavya mimba ile ili wasiweze kutambulika na Mkamandume ambaye angewameza wazimawazima. Anapanga njama na Bi. Reja kujaribu kuuficha ukweli lakini kabla ya mpango huo kufaulu, Mkamandume anagundua yaliyokuwa yamejiri.

Dhuluma hizi zinaendelezwa na Mkamandume anapogundua kwamba mwanawe (Viwe) alikuwa mjamzito. Anamshambulia na kumkaba koo akitaka kumuua. Jambo hili linazua rabsha wakati huo wa usiku kwani Time na mamake walipojaribu kumsihi Mkamandume asimuue Viwe, aliwashambulia na wao pia. Walijaribu kupigana naye na alipowazidi nguvu, waliamua kupiga usiahi ili majirani waje kuwasaidia. Maudhui haya yanakamilisha kazi hii kwani ndiyo yanayoonyesha namna utamaduni ulivyompendelea

mwanamume huku mwanamke akiachwa kupambana na hali yoyote ngumu ambayo aghalabu huwa imechangiwa na mwanamume pia.

### 2.4.5 Tamaa

Kupitia kwa migogoro mawazoni mwa Mkamandume, inabainika kwamba Wamalelejimema walikuwa na tamaa. Wamalelejimema walikuwa na tamaa iliyokithiri mpaka kwani hata pale sokoni kila mtu aling’ang’ana kuuza bidhaa zake atakavyo. Katika akili yake, Mkamandume hakuweza kujizuia kulinganisha maisha ya sasa na ya zamani. Nafsi yake inazua mgogoro kuhusu ni wakati gani ulikuwa na nafuu ya maisha kati ya zamani na sasa. Wafanyabiashara wengi waliwapunja wananchi wa kawaida kwa kuwauzia bidhaa hizo kwa bei ya juu sana. Haya yanabainika Mkamandume anapowaza:

> Biashara siku hizi ilikuwa kama kutiana adabu na kulipizana visasi. Kila mtu aliyeuza chochote kilichohitajika, alijaribu kuuza kwa bei kubwa kama inavyowezekana ili awakomoe wengine, ili aweze kuingia kwenye mzunguko wa kuishi (uk. 311)

Wafanyakazi wananyanyaswa na viongozi na wenye mamlaka makuu. Kwa mfano, baada ya Mkamandume kuacha kazi tangu alipopewa likizo bila marupurupu, alifukuzwa kazini na hakuna malipo yoyote aliyopata kutokana na kazi aliyokuwa ameifanya kwa miaka mingi. Kombo naye aliyekuwa mlinzi kule alikofanya kazi Mkamandume, alipigwa risasi na majambazi alipojaribu kuwazuia wasiingie ndani ya ofisi kuiba. Hii ni kwa sababu ya tamaa waliyokuwa nayo ya kutaka vitu visivyo vyao. Hakufa lakini alikuwa kitandani hajiwezi wala hakuwa na malipo yoyote ya bima wala ya serikali aliyojitolea kuihudumia kwa nguvu na roho yake. Haya yote yanazua mgogoro mawazoni mwa Mkamandume anapowaza:

> Siku hizi. Siku hizi. Zamani. Zamani. Mkamandume alikuwa hawezi kujizuia siku hizi kulinganisha zamani na sasa … Kwa nini sasa anahisi kwamba zamani ilikuwa nafuu kiliko sasa? Sasa aliyotazamia kuwa na furaha. Sasa imekuwa kama miiba kwa Mkamandume (uk. 311).

Mkamandume anazua mgogoro wa kimawazo ambao unaturudisha nyuma na kuangazia mzozo uliokuwepo wakati wa ukoloni na baadhi ya mambo yaliyowafanya wapiganie uhuru wao. Hata hivyo, anashindwa kubainisha unafuu wa maisha kwani anaona kuwa maisha ya sasa yametokea kuwa magumu zaidi.

### 2.4.6 Kukata Tamaa

Maudhui ya kukata tamaa yanajitokeza kupitia kwa migogoro ya kimawazo ya Mkamandume anapokumbuka namna watu walivyokumbwa na njaa baada ya vita vya ukombozi ilhali walichokipigania na kuwafanya wawafukuze wakoloni ni kujitegemea. Jambo hili linatokea kuwa kinyume kwani baada ya wale wakoloni kufukuzwa kutoka Malelejimema, wananchi wamebakia watu wasioweza kujitegemea na iliwabidi kutegemea chakula cha resheni na hata kupigania vitunguu vibovu. Haya yote yalitokana na uongozi mbaya wa Waafrika. Mkamandume anakumbuka kisa kimoja:

> Kisa kimoja hatakisahau kamwe Mkamandume. Katika msongamano wa kuwania vitunguu vibovu bimkubwa mmoja wa miaka sabini hivi alibanwa mbavu katika kibiru akapinduka chini na kupoteza fahamu. Alipochukuliwa hospitali hakuchukua siku nyingi; aliaga dunia … mpaka leo tukio lile la kifo kwa vitunguu vibovu lilimrusha roho Mkamandume (uk. 392).

Wamalelejimema wametamaushwa kabisa na maisha. Mkamandume anawaona wenzake ambao kulingana naye walikuwa wadogo wake mara mia ingawa walionekana wabovu zaidi kuliko yeye. Wamegeuka wakongwe wa miaka tisini na saba. Hivi ndivyo watu hawa walivyobaki kwa mateso ya makusudi. Alipomwangalia Vuai waliyesoma naye amebaki mfupa tu. Mussa aliyesuhubiana naye zamani uvuvini alikuwa mweupe kwa

safura. Haya yote yalitokana na uongozi mbaya uliochukuliwa na Waafrika baada ya kuwafurusha wakoloni.

### 2.4.7 Umaskini

Mawazo ya Mkamandume yanatupa taswira ya umaskini anapomtembelea Suguru. Familia ya Suguru ni mfano mzuri sana wa umaskini ulioikumba Malelejimema. Mkewe Suguru Bi. Mbunjaki alikereka sana na ile hali ya watoto kufunzwa mafunzo ya kijeshi na kuthamini sana kuua. Kwa mujibu wa mawazo ya Mkamandume, Bi. Mbunjaki kakonda kakondeana, kabakia macho tu. Na macho yenyewe meupe kama yaliyopakwa rojo la chokaa. Suguru naye anapotoka nje kumsalimia Mkamandume aliyekuja kumtembelea anasema kwamba dunia waliiharibu wenyewe na hivyo basi, Mungu alikuwa akiwaadhibu. Hawakuwa na maji, chakula, umeme, nguo za kuvaa, na matibabu wakiwa wagonjwa; hawangeweza kuwaelimisha watoto wao. Suguru anasema kwamba ingawa haya yote yanatokea, wamefumbwa macho na hawaoni (uk. 420).

Mawazo ya Mkamandume yanazidi kutudhihirishia umaskini anapokabiliana na mwanawe (Time) baada ya kufyeka shamba lao. Tunapata taswira ya umasikini kupitia kwa suruali ya Mkamandume ambayo ilikuwa mararu yenye maraka elfu (uk. 40). Kupitia kwa migogoro ya mawazo, tunapata kuona kwamba Mkamandume amebaki na kikata kidogo tu ambacho hakiwezi kulinganishwa na ardhi kubwa aliyoirithi kutoka kwa mababu zake (uk. 23). Ardhi hiyo kubwa aliiwekea rehani kushibisha matumbo yake na jamaa zake hadi akabaki bila ardhi. Mkamandume anakuja kujuta baada ya kufyeka kile kijishamba kidogo kilichokuwa tegemeo lao. Time anapomkabili Mkamandume, babake anawaza:

> Je hiyo haikuwa ishara ya machofu Time anayoyazungumzia? Je si sehemu ya umaskini … Si sehemu ya kushindwa kwake? (uk. 40)

Aidha, maudhui ya umaskini yanaendelezwa kupitia kwa mawazo ya Soud anapowazia hali ya Wamalelejimema pale ki-Mwajuma kinapokuja kumwomba sukari na kumweleza kwamba wao hawakuwa wamekunywa chai kwa miezi mitatu (uk 126). Jambo la kuja kuombwa sukari na ki-Mwajuma lilimtatiza Soud sana. Kitendawili cha kuwepo kwa maskini wengi na matajiri wachache kilimsumbua na kumshinda kukitegua. Jambo hilo linarudisha fikra zake katika enzi za wazazi wake walipokuwa hai. Kwao, walipata kila kitu walichokihitaji lakini kuna baadhi ya watu kama vile Msafiri, Mpikachai, Maliyatabu na Kinda waliokosa mahitaji yao muhimu. Soud anasononeshwa na hali kwamba umaskini umezidi kuwaathiri Wamalelejimema zaidi kuliko ilivyokuwa wakati wa ukoloni. Wengi walifikiri kwamba mambo yangetengenea baada ya Wakoloni kuondoshwa lakini mambo yanatokea kuwa kinyume kabisa. Haya yanadhihirika vyema mawazoni mwa Soud:

> Na sasa kinatokea nini katika dunia ya waamba ngoma wapya? Vilevile au zaidi ya vile, majumba yana utoshelevu na vibanda ni vitupu zaidi ya vilivyokuwa wakati ule (uk. 129).

Mbali na kusikitikia umaskini uliowakumba watu binafsi, Soud anasononeshwa na umasikini ulioikumba nchi ya Malelejimema. Haya tunayathibitisha kupitia kwa mawazo yake. Fikra zake zinakinzana kuhusu hali ya zamani na ile iliyoko sasa. Anasema kwamba hapo awali, mapato ya bandari na viwanja vya ndege vilikuwa tele. Nafasi za kazi na za elimu ya juu zilikuwa nyingi. Miliki ya nguvu za kibenki pia ilikuwapo lakini kwa sasa mambo hayo yote hayapo.

> Hapo tena Soud vilimjia vipande vya mawazo vilivyomwenda akilini harakaharaka. Tazama mapato ya forodha sasa, bandari na viwanja vya ndege …

> tazama misaada na mikopo, tazama nafasi za elimu ya juu … Zamani Malelejimema iliongoza kwa wingi wa yote hayo na sasa imekuwa ukurutu mtupu (uk. 240)

Suala la umaskini pia linamsumbua Time. Anashangaa ni kwa nini katika kijiji chao kumekuwa na umaskini uliokithiri. Anaangalia vibanda vilivyoinamiana vinavyoitwa makazi na wenyeji na kusikitika. Katika kijiji kizima kulikuwa na nyumba mbili tatu hivi ambazo zilistahili kuitwa nyumba. Anashangaa kwa nini vile vibanda vilisalia pale kijijini kwa karne nyingi. Mawazo ya Time yanatudhihirishia haya vema zaidi yanapojitokeza:

> Kwa nini kijiji kile kimekuwa na vibanda na vijumba vile karne zote zile? Kwa nini nyumba mbili tatu tu ndizo zilizochukua maana ya nyumba? Kwa nini… Time alijikataza kwenda zaidi upande huo katika fikra zake (uk. 196).

Kwa mujibu wa mifano hii, inabainika kwamba maudhui ya umaskini yamekuzwa vyema zaidi na kufanikishwa katika riwaya hii kupitia kwa migogoro ya kimawazo.

### 2.4.8 Usaliti

Kupitia kwa migogoro ya kimawazo ya wahusika mbalimbali, tunatambua kwamba viongozi wa Malelejimema wamewasaliti wananchi kwa kuendeleza ukoloni, miaka thelathini na saba baada ya wakoloni kutimuliwa. Ni miaka thelathini na saba baada ya ushindi wao dhidi ya wakoloni, lakini bado kuna unyanyasaji dhidi ya watu weusi. Unyanyasaji huu unaendelezwa na Waafrika wenyewe (uk. 200). Mkamandume anasononeka sana. Nafsi yake inamzomea kutokana na matarajio ambayo hayakutimizwa. Waliahidiwa kwamba kila mtu angepiga hatua nchini kimaendeleo baada ya uhuru lakini haya hayatokei. Jitihada anazoonyesha Mkamandume hazizai matunda yoyote na badala yake zinazidisha uchungu wake. Ameshindwa kabisa kumudu mahitaji

ya aina yoyote ya familia yake. Si chakula, si mavazi, si makazi; kila kitu alishindwa kukigharamia. Usaliti huu unadhihirika Mkamandume anapowaza:

> Anakwenda kakatwa uume wake na kurudi na butu la uume. Keshafikia daraja hili? Tayari ameshakuwa baradhuli kiasi hiki? Kama huko si kuporomoka ni nini? Kama hiyo si fedheha ni kitu gani? Hebu nambie Mkamandume (uk. 203).

Vivyo hivyo, kupitia kwa mikinzano ya kimawazo ya Mkamandume, tunatambua kwamba viongozi wamewasaliti wafanyakazi ambao walitarajia kuwepo kwa usawa katika ugavi wa nafasi za kazi na vilevile kupewa mshahara ambao ungeyakimu mahitaji yao baada ya uhuru. Matarajio ya wafanyakazi hayatimii kwani unyanyasaji unatokea kuwa mbaya kuliko ule uliokuwepo wakati wa ukoloni. Tuzo zinazotolewa kwa wafanyakazi bora waliojitolea kazini zinatolewa kwa ufisadi na mapendeleo kwa wavivu na wazembe kazini kama alivyokuwa mpwawe Bosi; Zuhura Saleh Mcheshi. Mkamandume anawaza:

> Lakini kama yeye alikasirika (Mkamandume), vicheko vya wafanyakazi wake wengi havikuwa vicheko vya furaha hata chembe. Vilikuwa vicheko vya maumivu. Au tuseme vilikuwa namna fulani ya kutoa dukuduku lao (uk. 26).

Aidh, kuna usaliti wa kimapenzi. Kupitia kwa migogoro ya kimawazo ya Nadia, tunafahamu kwamba alisalitiwa kimapenzi na Soud. Walipokutana kule Uingereza, walisuhubiana na Soud akafahamu kwamba Nadia alimpenda kwa dhati. Soud hakuwahi kumwambia Nadia kwamba alikuwa na mpenzi kwa jina Time ambaye walipendana naye tangu utotoni. Jambo hili linakuja kumsumbua Nadia kimawazo anapokuja kujigundulia na kukutana na Time kule Malelejimema. Mawazo ya Nadia yanadhihirika:

> Toba! Nani huyo Mungu wangu! Moyo Nadia ulimgutuka. Sadfa gani hii? Kweli au uongo? Au dhana yake mwenyewe Nadia? … Kwa hakika, Nadia alitaka iwe uwongo? (uk. 360)

Vivyo hivyo, Time naye anaona kwamba amesalitiwa na Soud kwa kutopigania penzi lao baada ya posa yake kukataliwa na babake, Mkamandume. Time haelewi ni kwa nini Soud ameamua kumpuuza kwa sababu Mkamandume alikataa ndoa kati yao. Wasiwasi unamwingia zaidi anapofikiria kwamba Nadia na Soud walikuwa wakiishi katika nyumba moja. Wasiwasi huu hata unamfanya kumchukia Nadia hata ingawa alijua vema kwamba Nadia hakufahamu uhusiano uliokuwepo baina yao na Soud. Mawazo ya Time yanadhihirika anapowaza:

> Kwa nini analalamika basi? Kwa nini kajaa wivu wote huo? Kwa nini anatokotwa na chuki? Kwa nini anamchukia mtu asiye na hatia wala madaraka kama yeye? Kitu gani wivu? Kitu gani chuki? … vipi atavifikia ili avitoe na kuvitokomeza? (uk. 196)

Haya yote yanathibitisha kwamba migogoro ya kimawazo imetuwezesha kukuza na kutambua maudhui ya usaliti katika riwaya hii.

### 2.4.9 Utabaka

Mgogoro unaobainika mawazoni mwa Mkamandume unatujengea maudhui ya utabaka. Katika pitapita zake pale mjini, anajipata mbele ya hoteli moja kubwa iliyomilikiwa na bosi wake wa zamani. Nafsi yake inamkanya kwamba angeingia katika hoteli hiyo, angefukuzwa kwani alivyovalia haikuafiki kiwango cha hoteli yenyewe. Hii inadhihirisha kwamba watu waliotarajiwa kwenda katika hoteli hiyo walikuwa wa tabaka la juu kwani hata mavazi yao yalitofautiana na ya akina yakhe kama Mkamandume. Mgogoro unajitokeza mawazoni mwa Mkamandume akiwa na shauku ikiwa angeruhusiwa kuingia katika hoteli hiyo ya watu wa tabaka la juu au la.

> Watakufukuza pindi uingiapo ndani tu.
> Kwa nini?
> Kwa sababu wewe hukuelekea kuwa mtu wa kuingia mkahawa kama huo.

> Kwa nini?
> Sura yako, kivazi chako, mchukuo wako, nafsi yako nzima (uk. 438).

Kupitia kwa mgogoro huu unaojitokeza mawazoni mwa Mkamandume, inabainika kwamba kuna taasisi na huduma mbalimbali zinazopatikana katika jamii ambazo zimetengwa kwa matumizi ya watu wa matabaka mbalimbali. Aidha, kupitia kwa mgogoro wa mawazo ya Time, utabaka huu unadhihirishwa anapowaza:

> Kwa nini kijiji kile kimekuwa na vibanda na vijumba vile karne zote zile? Kwa nini nyumba mbili tatu tu ndizo zilizochukua maana ya nyumba? Kwa nini … Time alijikataza kwenda zaidi upande huo katika fikra zake (Uk. 196).

Kwa kuzingatia haya yote tunaweza kuhitimisha kwamba migogoro ya kimawazo ndiyo kwa kiwango kikubwa imekuza maudhui mengi katika riwaya hii. Kwa mujibu wa McClinton Temple (2011), mgogoro kati ya mtu na jamii ni jambo la kawaida katika jamii. Anasisitiza kwamba mambo ambayo yanazua ukinzani huu ni nguvu fulani katika jamii na historia, ambayo hayaingiliani na ubinafsi na matakwa ya mtu. Jambo hili ndilo linamfanya Mkamandume kuwa katika hali ngumu na jamii yake kwani anataka Malelejimema iliyotengenea na patulivu. Hata hivyo, jambo hili haliingiliani kabisa na hali halisi katika Malelejimema. Nchi ya Malelejimema imejaa unyanyasaji, mauaji, na ukiukaji haki za binadamu wa aina mbalimbali.

Sehemu inayofuata ilichanganua namna migogoro ya mawazo ya kimawazo ilivyoibua dhamira na maudhui ya mwandishi katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2012)

### 2.5.1 Migogoro ya Kimawazo, Dhamira ya Mwandishi na Maudhui Katika Riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2012) K.W. Wamitila

Kwa mujibu wa Soo (1981) Migogoro ni misuguano, mikinzano au kutoelewana kati ya pande mbili au zaidi katika jamii. Anaainisha migogoro katika makundi manne ambayo

ni: mgogoro wa kimawazo, mgogoro kati ya mtu na mtu, mgogoro kati ya mtu na jamii na mgogoro kati ya jamii na jamii. Utafiti wetu umejikita katika mgogoro wa kimawazo. Soo anafafanua migogoro ya kimawazo kama mivutano inayoweza kujitokeza akilini mwa mtu mmoja au watu wawili au makundi mawili yenye mawazo yanayokinzana. Anasisitiza kwamba suala la migogoro ni muhimu sana katika jamii yoyote ile kwani ndio msingi wa mabadiliko yote na maendeleo ya binadamu.

Katika utafiti huu, riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2012) ya Wamitila K. imechanganuliwa kwa kuzingatia mhimili wa ubia wa migogoro. Mhimili huu unasisitiza kwamba migogoro hutokea katika kila jamii na kwa kila kitu. Mwandishi wa riwaya hii ameibua migogoro na maudhui katika jamii mbalimbali na kuonyesha uhasama na mzozo uliopo baina ya jinsia ya kike na jinsia ya kiume. Kupitia kwa mawazo ya wahusika wawili mahututi, mmoja wa kike na mwingine wa kiume, mwandishi huyu ametusimulia visa mbalimbali kutoka kwa jamii mbalimbali. Visa hivi vinathibitisha kwamba migogoro kati ya mwanamume na mwanamke hujitokeza katika jamii zote. Riwaya hii imegawanywa katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza inayotangulizwa kwa mwanamke mgonjwa mahututi ambaye kupitia kwa mawazo yake tunasimuliwa visa mbalimbali vya migogoro kati ya mwanamke na mwanamume. Sehemu ya pili nayo inasheheni visa vinavyodhihirisha mzozo uliopo baina ya mwanamke na mwanamume kwa mtazamo wa kiume. Visa hivi vinasimuliwa kupitia kwa mawazo ya Mumbo ambaye pia ni mgonjwa mahututi na hakumbuki jambo lolote ila jinsia yake. Maudhui yaliyoibuliwa na migogoro ya mawazo ni pamoja na:

### 2.5.2 Ndoa

Kitangulizi cha sehemu ya kwanza ni cha mwanamke aliyelazwa hospitalini na hana uwezo wa kukumbuka chochote ila jinsia yake kuwa ni mwanamke. Anapoulizwa na wanaomuuguza kwamba anaitwa nani? anawajibu kwa neno moja tu “mwanamke”. Wanapomdadisi zaidi anashikilia tu kwamba ni mwanamke. Baadaye, wanamkejeli kwamba jambo lililomfanya ajipate katika hali hiyo ni kumdharau mumewe. Mazungumzo haya yanaelekea kuashiria kwamba ndoa  kati ya mume na mke huongozwa na mzozo tu bila ya kuwepo kwa amani. Mizozo hii huonekana kuwa mibaya kiasi cha wanawake kupigwa na kujeruhiwa vibaya. Hii ndiyo maaana mmoja wa wanaume wale anamwuliza:

> Au ulimwotea mumeo pembe. Je, ulitaka kuyatwaa mamlaka yasiyokuwa yako? (uk. 30).

Kwa mujibu wa maneno haya, inadhhirika kwamba mume hutwaa mamlaka makuu katika ndoa na iwapo mke atatishia kuyatwaa mamlaka hayo basi migogoro hutokea na hata mke kuishia kujeruhiwa vibaya. Aidha, katika kisa cha Kasekesi, mawazo ya mama kuhusu ndoa yanatofautiana kabisa na yale ya baba. Wazazi wote wawili wanamshauri Kasekesi namna ya kuishi katika ndoa yenye furaha. Mama anamshauri Kasekesi kwamba atakapotaka kuolewa amtafute mume atakayemheshimu, asiye mtamaduni na ambaye atamthamini kama kiumbe. Asitafute mume mtamaduni atakayemmiliki kama chombo. Mama anamshauri Kasekesi asitafute mwanamume wa huko kwao anayemchukulia mwanamke kama shamba linalostahili kulimwa kila mara. Aidha, mama anamshauri Kasekesi kwamba asinyamaze kimya anapodhulumiwa katika ndoa. Atoe

sauti na kupinga unyanyasaji unaotoka kwa jinsia ya kiume. Anamshauri kwamba iwapo hatapata mume anayemheshimu mwanamke basi ni heri asiolewe.

Mawazo ya baba kuhusu ndoa nayo yanakinzana kabisa na yale ya mama. Anamwambia Kasekesi kwamba heri ndoa mbaya kuliko ujane mwema. Anamsisitizia kwamba mwanamume ni kichwa cha nyumba na anastahili kuheshimiwa hata akiwa gumegume. Anamshauri atafute mwanamume wa kwao kwani ni wanaume wazuri. Wanaume hao wanafuata utamaduni wao ambao umekuwako tangu jadi. Anamwelekeza kwamba asitafute gumegume asiyefuata utamaduni. Baba anamhimiza Kasekesi amnyenyekee mumewe na kumtii kwa vyovyote. Anashauriwa asifuate mwanamume anayekimbilia usasa na kuacha utamaduni wake. Kasekesi anapokuja kuolewa baadaye na tajiri mmoja kwa jina Agusto, wanaishi katika ndoa bila visa vyovyote vya kikatili hadi mumewe anapofilisika na kuanza kunywa pombe. Hatimaye, mumewe anaaga dunia. Hapo ndipo jamaa za mumewe wanamsingizia kwamba alimuua mumewe na wanaamua kumtesa sana.

Ndoa ya pili ni ile ya Mwanamuka na Kitonga na inatokea baada ya Mwanamuka kukosa karo ya kuendeleza masomo yake. Mwanamuka anakaa bila kupata mtoto na hatimaye wanaanza kuzozana na mumewe anamwoa kijakazi wao. Nyakor pia anatofautiana kimawazo na mumewe. Mawazo ya Nyakor na mumewe kuhusu ndoa na utamaduni yanatofautiana. Mumewe Nyakor anaamini kwamba mke anastahili kumheshimu mumewe na anaona kwamba Nyakor ameacha utamaduni wao na kumdharau kama mume. Nyakor naye anaamini kwamba mume hastahili kumdhulumu mke katika ndoa kwa sababu ya utamaduni. Anaukataa unyanyasaji wa mumewe na ndoa yao inakuwa ya

misukosuko mingi na migogoro ya kila mara. Mumewe anapokufa, mawazo ya Nyakor yanatofautiana kabisa na yale ya wazee wanaoshikilia utamaduni kwamba lazima arithiwe. Nyakor anakataa kabisa kurithiwa baada ya mumewe kufa.

Kamene naye anatoswa kwenye ndoa ya lazima baada ya babake kukataa kumlipia karo kwamba elimu ndogo ya shule ya msingi ilimtosha kama mtoto wa kike. Kamene anatoroka kutoka kwenye ndoa hiyo na kutafuta msaada kutoka kwa mwalimu Zipporah Mosha ambaye anamsaidia kuendelea na masomo yake hadi chuo kikuu na kufuzu na shahada mbili. Kamene anafanikiwa kuwa mwalimu wa chuo cha walimu. Baadaye, wanakutana na Ceddy Lusweti ambaye anamvutia kwa uchesi wake. Hata hivyo, Kamene bado anajikanya dhidi ya mahusiano ya ndoa kwani anakumbuka mateso aliyoyapitia katika ndoa yake ya kwanza. Mgogoro wa mawazo unajitokeza pale nafsi yake inamkanya dhidi ya kuingia katika ndoa ambayo ingeweza kumkumbusha machungu aliyoyapitia. Kwa upande mwingine, sauti akilini mwake inamshawishi akubali kuolewa na Ceddy kwani hayo mengine yalitokea akiwa angali mchanga. Mgogoro ufuatao unatokea mawazoni mwake:

> Sauti ya nafsi yake ikawa inamkumbusha kiapo alichoapa zamani: kuwa ikiwa mara ya kwanza alizongomezewa kwenye ndoa kama ng'ombe wanaosagwasagwa na kutoswa kwenye josho, akiwa na satua na uamuzi wake, hatofanya kosa la kujiingiza kwenye ngome hiyo tena. Lakini akilaani sauti yake hiyo na hata kuikosoa kwa kutokumbuka kuwa huo ulikuwa uamuzi uliofanywa kwa hasira na kwamba binadamu haishi kubadilisha msimamo wake kadri wakati unavyosonga (uk. 85).

Hatimaye, Kamene anapofanya uamuzi wa kufunga ndoa na Ceddy, ndoa yao inakuja kuwa ya mashaka matupu kwani kila mara wanazozana na mumewe. Chanzo kikuu kikiwa ni migogoro ya mawazo. Mavyaa anaingilia ndoa yao na kumfanyia Ceddy kila

kitu kama mtoto mchanga. Ndoa hiyo inasambaratika na Kamene anapodai haki na ufadhili wa mtoto wao kutoka kwa Ceddy, anavamiwa na kupoteza fahamu.

Ndoa nyingine iliyojaa hila na udanganyfu ni ndoa kati ya Kaminda na Sasi. Sasi alimhadaa Kaminda wakafunga ndoa kanisani huku akifahamu vyema kwamba alikuwa na mtoto msichana aliyempata nje ya ndoa. Kaminda alipogundua jambo hili, ndoa yao inaishia kuwa ya migogoro  na manung'uniko kila wakati. Hatimaye ndoa hiyo pia ilikuja kuvunjika.

Ndoa nyingine inayodhihirisha migogoro ya kimawazo ni ile kati ya Sir Pipo na Lulu. Kwanza, wanatofautiana kuhusu watoto katika ndoa. Lulu anaamini kwamba katika ndoa watoto wanastahili kuzaliwa hata katika umri mkubwa lakini Sir Pipo anaamini kwamba watoto wanastahili kuzaliwa mapema katika ndoa. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kati ya wanandoa hao. Vivyo hivyo, Sir Pipo anaamini kwamba mume ndiye anastahili kuwa na usemi mkubwa katika ndoa. Lulu naye anaamini kinyume chake kwani anaona kwamba mke na mume wanastahili kuwa na usemi sawa katika ndoa. Kwake Lulu, mke si chombo cha kudhibitiwa nyumbani na kuamrishwa na mume atakavyo. Jambo hili lilimfanya ajiingize katika harakati za kuwatetea wanawake. Hatimaye, ndoa yao pia inakuja kusambaratika.

Ndoa kati ya Purupesa na Truvessa nayo inadhihirisha migogoro ya kimawazo kati ya wanandoa. Purupesa anaamini kwamba mke katika ndoa anapaswa kumtii mumewe, kujihesimu, kuuheshimu na kufuata utamaduni wa Kiafrika. Truvessa naye anaamini kwamba uhuru kamili unastahili kuwepo katika ndoa ili mke apewe fursa ya kufanya atakavyo. Mgogoro huu unadhihirika zaidi Truvessa anaposema:

> Uhuru hauna aibu. Kwa nini niyabane mawazo yangu ndani yachipukizie kwenye ndoto tu kwa kuwa jamii iliyotiwa pingu na mila imeyakataza? (Uk. 212).

Purupesa naye anajibu:

> Truvessa … hizo ni tabia za Ulaya na Marekani … watu ambao wamekosa mwelekeo na kuyachoma maghala ya utamaduni zamani kama kijana ambaye ameshiba na kuamua kuchoma ghala la chakula." (uk. 213)

Kwa kuwa mawazo ya wanandoa hawa yalikinzana, ndoa yao ilisambaratika na Truvessa kuishia kupata maradhi yaliyomlaza hospitalini. Hatimaye, wanandoa hawa wawili waliishia kuangamia. Haya yote yanadhihirisha kwamba chanzo cha matatizo katika ndoa ni migongano ya kimawazo ambayo inasababisha ndoa nyingi kuvunjika. Hivyo basi, ni sahihi kuhitimisha kwamba migogoro ya kimawazo ilimwezesha mwandishi huyu kukuza vyema maudhui ya matatizo katika ndoa.

### 2.5.3 Elimu ya Mtoto wa Kike.

Maudhui mengine ambayo mwandishi ameyaangazia ni elimu ya mtoto wa kike. Migogoro ya kimawazo inamfanya kushughulikia maudhui haya kikamilifu kwani anadhihirisha wazi namna jamii mbalimbali zilivyo na mawazo yanayokinzana kuhusu elimu kwa mtoto wa kike. Baadhi ya wanawake wanakosa elimu na kuingizwa katika ndoa za mapema. Mwanamuka anakosa kuendelea na masomo yake kwa sababu anakosa karo. Mawazo ya wazazi wa Mwanamuka kuhusu elimu kwa wanawake yanatofautiana na yale ya wanakijiji. Wazazi wa Mwanamuka wanaona kuwa kumwelimisha mtoto wa kike ni jambo la busara hata wanahangaika kumtafutia karo na kuomba msaada kutoka kwa wanakijiji. Wanakijiji na jamaa zao wanawacheka na kutofautiana nao kimawazo kwani wanaamini kwamba kumwelimisha mtoto wa kike ni kujisumbua bure, kupoteza

wakati na kuharibu pesa kwani ataishia kuolewa tu. Haya yanajitokeza katika mawazo yafuatayo:

> Ya nini kujisumbua bure? … mtoto wa kike unamwelimisha nini na ataishia kuolewa? ... umesikia wapi mtu anatafuna nyama inayomezwa na mwingine… Huko ni kutia maji kwenye mashimo ya kichuguu (uk. 57)

Maneno haya ya wanakijiji hayakumfisha moyo mamake Mwanamuka ingawa babake alikata tamaa na kuanza kunywa pombe. Mamake Mwanamuka aling'ang'ana kumtafutia karo kutoka kwa mhubiri wa pale kijijini lakini akakosa. Badala yake, mhubiri alimtuma kwa mkuu wa wilaya kwani huko kulikuwa na hazina ya kuwaelimisha watoto maskini. Huko nako aliambulia patupu. Miaka miwili baadaye Kitonga akajitokeza na kumwoa Mwanamuka. Wanakijiji wakajitokeza na kusema kwamba utabiri wao kuhusu elimu ya mtoto wa kike ulikuwa umetimia. Mgogoro huu wa kimawazo unamsaidia mwandishi kujenga maudhui matatu kwa pamoja:

Kwanza, mgogoro huu unamwezesha mwandishi kukamilisha maudhui ya elimu kwa watoto wa kike. Katika jamii hii mtoto wa kike alinyimwa haki ya kuelimishwa kwa sababu angeolewa na kuishia kusaidia jamii nyingine tofauti. Hivyo basi, hakukuwa na haja ya kupoteza pesa bure. Aidha, mgogoro huu ulimwezesha mwandishi kuangazia utamaduni mbaya unaomdhalilisha mwanamke na kumchukulia kama chombo cha kutekea mali. Mwanamuka analazimishwa kuolewa na Kitonga akiwa angali na umri mdogo sana. Anaolewa na mtu asiye wa rika lake ambaye alikuwa ameachana na mkewe. Mamake Mwanamuka anapewa pesa kidogo za kuelimisha wadogo wa Mwanamuka. Mgogoro huu pia unamsaidia mwandishi kuibua maudhui ya matatizo yanayomkumba Mwanamke katika asasi ya ndoa. Baada ya Mwanamuka kuolewa na Kitonga, ilitokea

kwamba Kitonga alimnyanyasa, kumtesa na alipokosa kupata mtoto, Kitonga alimwoa mke mwingine.

Katika hadithi ya Nyakor mambo yanaonekana kuwa tofauti kiasi kwani Nyakor alisoma hadi chuo kikuu na kufuzu kuwa mhandisi. Hata hivyo, mwandishi alitumia kisa cha Nyakor kuendeleza mgogoro huu wa kimawazo kati yake na mumewe. Katika ndoa hii, mume wa Nyakor alitaka kuwa wa pekee wa kusikilizwa huku Nyakor akinyenyekea na kukaa kimya hata aliponyanyaswa. Anaamini kwamba ni jukumu la mke kumridhisha mumewe kwa vyovyote vile katika hali nzuri na mbaya. Alichukulia mwanamke kama kiumbe asiye na hisia. Nyakor kwa upande wake alikuwa na msimamo kwamba wanandoa wote wawili wana haki sawa. Mgogoro wao katika ndoa uliendelea hadi mumewe alipoaga dunia. Baada ya mumewe kuaga dunia, Nyakor alijiingiza katika mgogoro mwingine na utamaduni wake. Wazee walimlazimisha arithiwe baada ya mumewe kufa ili asiiletee jamii bahati mbaya au kuvutia hasira za mizimu. Nyakor alikataa katakata kufuata utamaduni ambao hakuona umuhimu wake.

Mgogoro huu umetumiwa na mwandishi kufanikisha mambo mawili. Kwanza, mwandishi ameonyesha kwamba mwanamke anapopata elimu kikamilifu huweza kusimama kidete na kukataa unyanyasaji dhidi yake katika ndoa. Pili, mzozo huo unaonyesha kwamba elimu ni chombo muhimu cha kumwezesha mwanamke kupinga utamaduni unaodhamiria kumnyanyasa na kumdhalilisha huku ukimtukuza mwanamume.

Suala la elimu kwa mtoto wa kike pia linajitokeza katika kisa cha Kamene ambaye alichukiwa na babake tangu alipozaliwa kwani babake alitarajia mtoto wa kiume akampata wa kike. Kwa hivyo, tokea hapo mahitaji yake yote yalishughulikiwa na

mamake. Kamene hakumaliza shule kama ndugu zake bali babake alisema kwamba elimu ndogo ya shule ya msingi ilimtosha. Walimu wa Kamene walimshauri babake amwache aendelee na masomo lakini akakataa. Hapa pia tunapata mawazo ya babake Kamene na yale ya wanakijiji yakitofautiana. Babake Kamene anaona kwamba wanakijiji ni wanafiki. Kwa mfano, yule mhubiri aliyejifanya anamshauri alikuwa mwovu aliyegombana na jirani yake kutokana na kuku wake kuharibu maua ya mimea. Baadaye, Kamene anatekwa nyara na kulazimishwa kuolewa. Hata hivyo, anaokolewa na Bi. Ziporrah Mosha ambaye hakuwa mwenyeji wa kijiji chao. Huko Kamene anapata fursa ya kuendeleza masomo yake hadi chuo kikuu.

### 2.5.4 Dhuluma Dhidi ya Wanawake

Maudhui mengine yanayojitokeza katika riwaya hii ni ukiukaji wa haki za wanawake. Migogoro ya kimawazo inamwezesha mwandishi kukuza maudhui haya kwani kuna visa vingi vinavyojitokeza katika jamii mbalimbali anazozizungumzia katika riwaya. Katika sehemu ya kwanza mwandhishi anatanguliza riwaya yake kwa kutupa taswira ya mwanamke mahututi aliyelazwa hospitalini ambaye anachofahamu tu ni kuwa yeye ni mwanamke. Kuna mvutano wa kimawazo kati yake na wanaume wanaomhudumia pale hospitalini. Wale wauguzi na madaktari wa kiume wanaamini kwamba ni uovu wake ndio ulimfanya ajipate katika hali hiyo. Wanaamini kwamba lazima alimfanyia mumewe ujeuri, aliongoza wizi wa benki, alishikwa ugani na mume wa mtu au alipatikana akifanya biashara haramu. Aidha, wanasema kwamba mwanamke hawezi kuongoza na katika historia hakuna mwanamke aliyewahi kuongoza na kufaulu.

Hata hivyo, msimulizi ana mawazo tofauti kwani anajua kwamba mwanamke hana unyonge anaosingiziwa. Aidha, anafahamu kwamba mwanamke anaweza kuwa kiongozi kama alivyokuwa Yule mwanamke wa kichina Wu Zeitan. Alijitokeza na kuwatetea wanawake katika enzi hizo za wanawake kunyanyaswa bila kutarajiwa kulalamika. Kasekesi naye anapitia mateso baada ya wazazi wake kufa. Ilibidi aende kuishi na mjomba wake ambaye baada ya muda fulani alimwoza kwa Agusto Muridhania. Kabla ya mamake Kasekesi kufa mashauri aliyompa yanaonyesha kwamba wanaume katika jamii yake hawawathamini wanawake hata kidogo. Wanashikilia utamaduni unaowadhulumu wanawake. Wanaume hao huchukulia wanawake kama kitu cha kuliwa. Babake naye anamshauri kwamba amtafute mume kutoka katika jamii yao kwani wao ndio wanaojua kufuata utamaduni wao.

Baada ya Kasekesi kuolewa wanaishi kwa amani na mumewe hadi anapofilisika na kuanza kunywa pombe kupindukia na hatimaye kufariki. Jamaa za mume wake wanakuja juujuu na kumsingizia Kasekesi kwamba ndiye aliyemuua mumewe. Wanamtesa sana na kumlazimisha kulala katika chumba kimoja na maiti ya mumewe. Wanampa mchanganyiko wa dawa za kienyeji zinazomfanya kutapika sana na hata kuishiwa nguvu. Wanararua nguo zake na kumpaka matope huku wakimtembeza katika kijiji kizima. Kasekesi anapokosa kufa kama walivyotarajia wanamfukuza. Anaenda kwa shangazi yake ambaye hapendezwi na kuja kwake. Anapokosa kupata amani huko, anaamua kwenda kwa mjomba wake lakini hafiki kule. Hakumbuki chochote baada ya hapo kwani anajipata kalazwa hospitalini bila fahamu.

Mawazo ya msimulizi (Kasekesi) yanampa msomaji kisa cha Mwanamuka. Jamii ya Mwanamuka inatofautiana kimawazo na wazazi wa Mwanamuka kuhusu elimu ya mtoto msichana. Wazazi wa Mwanamuka wanapoomba msaada kutoka kwao, wanakataa na kuwadhihaki kwamba mtoto wa kike hapaswi kuelimishwa kwani ataishia tu kuolewa. Hata hivyo, kikwazo hicho hakimzuilii mamake Mwanamuka kutafuta msaada kwingineko. Kwanza anamwendea mhubiri ambaye anakataa kumpa msaada kutoka katika hazina ya kanisa ya kusaidia watoto maskini na badala yake anamwelekeza kwa mkuu wa wilaya ambaye anakuja kumwona tu baada ya kuhangaishwa sana. Hata vivyo, anaishia kukosa msaada aliotarajia. Baadaye, Mwanamuka anaishia kuolewa na Kitonga. Ndoa yao inapokosa mtoto, wa kulaumiwa na kudharauliwa anakuwa ni Mwanamuka lakini mumewe anakataa kwenda naye hospitalini ili wafanyiwe uchunguzi wa kiafya. Hatimaye mumewe anaishia kuoa kijakazi wake kama mke wa pili. Mwanamuka anaachana na mumewe na kufanya juu chini kujiendeleza kimasomo. Anapata kazi kama mhariri mkuu katika shirika moja la uchapishaji vitabu. Huko nako anafukuzwa kwa kukataa au kupuuza miswada mingi ya wanaume.

Aidha, kisa cha Nyakor kinadhihirisha migogoro ya kimawazo inayojitokeza kati ya mwanamke aliyepata elimu ya kimagharibi na wazee wanaoshikilia utamaduni wao wa jadi. Nyakor alipata elimu ya kimagharibi hadi akafuzu kwenda chuo kikuu. Huko anafuzu kwa kupata shahada ya uhandisi. Ndoa yao inaingiliwa na migogoro kwani mawazo yake yanatofautiana na ya mumewe anayeamini kwamba mkewe anamdharau kwa sababu amesoma na kupata shahada. Baada ya mumewe kufa anazozana na wazee wanaosisitiza kwamba Nyakor lazima arithiwe na mume mwingine. Nyakor anakataa

katakata kwamba hawezi kufuata utamaduni usio na maana kwake. Wazee wanatishia kumlaani na kuomba mizimu imwadhibu.

Zahra pia anayanyaswa na jamii yake. Anabakwa na mwalimu wake wa madrasa lakini babu yake anaporipoti kisa hicho kwa chifu, kiongozi huyo hachukui hatua yoyote kwani aliogopa kuwa kijana aliyehusika alikuwa binamuye waziri. Babu anaposukuma zaidi haki itendeke wanakamatwa wote na kuondolewa nje ya nchi kwa kisingizio kwamba hawakuwa wenyeji bali wahamiaji walioingia nchini bila kibali. Kamene naye alichukiwa na babake tangu alipozaliwa. Babake anakataa kumwelimisha na kusema kwamba elimu kidogo ya shule ya msingi ilimtosha kwani angeishia kuolewa. Baadaye anatekwa nyara na kuingizwa katika ndoa ya lazima. Anatoroka na kwenda kuomba msaada kwa Bi. Ziporah Mosha anayekubali kumsaidia kuendeleza masomo yake. Baadaye anakutana na Ceddy anayemwoa lakini maisha yake ya ndoa yanakuwa magumu. Ndoa yao ilijaa mzozo wa mara kwa mara. Kamene anapojifungua kwa njia ya upasuaji, mumewe anampuuza na kukataa kumsaidia au hata kumtafutia kijakazi. Wanakuja kutengana na mumewe Ceddy ambaye anakataa kuotoa pesa za kugharamia mahitaji ya mtoto wao. Kamene anapoamua kutafuta msaada wa kisheria, anavamiwa na kupoteza fahamu.

### 2.5.5 Uwajibikaji na Malezi

Migogoro ya mawazo pia imemsaidia mwandishi wa riwaya ya *Unaitwa Nani?* kukuza maudhui ya uwajibikaji na malezi. Kupitia kwa masimulizi ya Kasekesi, tunapata kuwa malezi yake yanakuwa na changamoto baada ya wazazi wake kufa. Kasekesi anaturudisha nyuma kupitia kwa mbinu rejeshi ambapo anatusimulia ushauri wa mama na vilevile ushauri wa baba. Mtoto huyo anajikuta katikati ya mawazo ya baba na yale ya

mama ambayo yote yanakinzana. Hivyo basi, anaachwa amechanganyikiwa kuhusu ndoa kwani anashindwa afuate ushauri wa baba au wa mama. Mama anaamini kwamba wanaume kutoka jamii yao ni watu wanaowadhulumu wanawake na hivyo basi Kasekesi anastahili kujihadhari nao. Baba naye anamshauri kwamba amtafute mwanamume kutoka katika jamii yao kwani ndio wanaojua kufuata utamaduni wao na wana weledi wa kuishi na mke.

Malezi ya Kasekesi yanaachiwa mjombake ambaye anakuja kumwoza kwa tajiri mmoja kwa jina Agusto. Kasekesi anaingia katika ndoa hii akiwa na umri mdogo sana. Wanawake wengi ndio wanaoachiwa majukumu ya kuwalea watoto hasa wale wa kike huku wanaume wakipuuza majukuu yao kama walezi. Mamake Mwanamuka ndiye anayehangaika kumtafutia karo huku babake akizama kwenye ulevi. Zahra naye analelewa na babu na nyanyake baada ya mamake kufa wakati wa kumzaa. Hawa wawili wanaonyesha kuwajibika kwani wanajitahidi kuhakikisha kwamba alipata hekima ya kilimwengu na ya kidini. Wanapompeleka Zahra kwenye madrasa anabakwa na mwalimu wake wa dini. Babu yake anatafuta haki kwa udi na uvumba kutoka kwa chifu lakini haipati. Chifu anachelea kumchukulia mhusika huyu hatua kwa sababu angefukuzwa kazi na kupoteza marupurupu yake ya ustaafu. Mwishowe Zahra anaishia kukosa haki.

Kamene alizaliwa na kukataliwa na babake tangu alipozaliwa. Babake alitarajia mtoto wa kiume. Kamene anapotokea kuwa msichana, babake anakataa kabisa kumwajibikia kama mzazi. Kamene anashughulikiwa tu na mamake na hata anapofika katika shule ya msingi, babake anasema kwamba elimu hiyo ilimtosha. Baadaye anatekwa nyara na kulazimishwa kuolewa. Anatoroka kutoka kwa ndoa yake na kwenda kupata msaada kutoka kwa mwalimu Zipporah Mosha. Mwalimu huyo anamsaidia kuendelea na

masomo yake hadi chuo kikuu. Baadaye anaolewa na Ceddy Lusweti ambaye anampuuza na kumsikiliza mamake sana kuliko mke wake. Kunatokea mawazo yanayokinzana kati ya mama mkwe na Kamene. Ceddy anaamini kwamba ni haki yake kufanyiwa kila kitu na mamake hata kufuliwa nguo zake za ndani. Mawazo haya yanatofautiana na yale ya Kamene ambaye anaamini kwamba Ceddy anastahili kujitoa katika minyororo ya kumtegemea mamake. Wanapopata mtoto wao wa kwanza, Ceddy anamtelekeza na kumpuuza mkewe asitake kujua masilahi yao. Kutowajibika huku ndiko kunamfanya Kamene kumshitaki Ceddy kwa kumpuuza mtoto wake. Hata hivyo anavamiwa na hatima yake haijulikani ilipofikia.

**2.5.6 Utamaduni.**

Mwandishi pia amekuza maudhui ya utamaduni kwa kuangazia migogoro ya kimawazo. Katika jamii mbalimbali anazozungumzia mwandishi, inabainika kwamba tamaduni nyingi za Kiafrika zinamkandamiza mwanamke kupitia kwa mila zisizo na umuhimu wowote katika jamii. Migongano ya kimawazo inajitokeza hasa miongoni mwa wanawake waliopata elimu na wale wanaume wanaoshikilia utamaduni. Mfano mzuri ni ule wa Nyakor anayepata shahada chuoni na kukataa unyanyasaji wa kijinsia kutoka kwa mumewe. Baada ya mumewe kufa, anakabiliana na wazee na kuwakataza peupe kwamba asingekubali kurithiwa na mwanamume mwingine kama utamaduni wao ulivyosisitza. Wanamtisha kwamba mizimu ingemwadhibu iwapo angekataa utamaduni huo wa jadi. Nyakor anawajibu kwamba anangoja hiyo mizimu akabiliane nayo.

Purupesa na mkewe Truvessa nao wanashikilia mawazo yanayopingana kuhusu utamaduni. Kwa Purupesa, utamaduni wa Kiafrika ni utamaduni mzuri unaostahili

kufuatwa kwani unazingatia maadili. Sio kama utamaduni wa kigeni usiojali ustaarabu. Kwa mkewe Truvessa aliyepata elimu ya Kimagharibi, Utamaduni wa Kiafrika ni kama minyororo iliyowafunga Waafrika na hawana uhuru tena ingawa wanadai kuwa huru

**2.5.7 Hitimisho**

Kwa mujibu wa utafiti huu, imedhihirika kwamba migogoro ya kimawazo kati ya wahusika mbalimbali ni kipengele muhimu ambacho kiliwasaidia waandishi kujenga maudhui yao mbalimbali. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mkamandume* dhamira ya mwandishi ilikuwa kuonyesha kwamba chanzo cha matatizo yote katika jamii ni uongozi mbaya na ubinafsi. Mwandishi ameweza kufikia dhamira hii kwa kuwa alijumuisha migogoro mbalimbali ya kimawazo katika kazi yake ambayo ilimwezesha kuzua maudhui kama vile tamaa, unyanyasaji, dhuluma dhidi ya wananchi miongoni mwa mengine. Sura hii imedhihirisha kwa kutoa mifano mbalimbali kutoka riwayani kwamba maudhui haya yalijitokeza vyema zaidi kwa kuwa yaliegemezwa kwenye migogoro ya kimawazo.

Aidha, ukweli wa mhimili wa nadharia ya upembuzi unaosisitiza ubia wa migogoro katika jamii umebainika kwani kuna jamii mbalimbali zilizoangaziwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* na masuala mbalimbali kushughulikiwa vilivyo hasa katika ndoa na dhuluma dhidi ya wanawake. Haya yote yamefaulu vizuri kwa kuegemezwa kwenye migogoro ya kimawazo inayojitokeza katika masimulizi yenyewe. Sura inayofuata (ya

tatu) imeshughulikia namna migogoro ya kimawazo ilivyowawezesha waanddishi wa riwaya teule kuwakuza wahusika wao.

# SURA YA TATU

# MIGOGORO YA KIMAWAZO NA UKUZAJI WA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA ZA *MKAMANDUME* NA *UNAITWA NANI?*

## 3.1.0 Utangulizi

Sura hii imechanganua suala la wahusika na migogoro ya kimawazo na jinsi migogoro hiyo ilivyowawezesha waandishi wa riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?* kuwakuza wahusika wao. Sura hii imedhihirisha namna migogoro ya kisaikolojia miongoni mwa wahusika mbalimbali inavyoweza kuathiri mahusiano yaliomo baina ya wahusika wenyewe na jamii zao. Hakuna mhusika anayeweza kuendelezwa katika ombwe tupu. Woloch (2003) anasisitiza kwamba nafasi ya mhusika yeyote katika fasihi hudhihirika tu miongoni mwa wahusika wengine. Kwa sababu hii, ni vizuri kuchunguza masuala yanayoweza kuathiri uhusiano miongoni mwao ili kuweza kuelewa ujumbe wanaoubeba. Migogoro ya ndani kwa ndani ya mhusika inapaswa kuchunguzwa ili tuweze kuelewa nafasi ya mhusika huyo na kubainisha namna inavyomwathiri na wahusika wengine wanaomzunguka.

Uchanganuzi wa wahusika katika sura hii uliongozwa na mhimili wa pili wa nadharia ya upembuzi ambao unasisitiza upekee wa migogoro katika kazi ya fasihi. Mhimili huu unasisitiza kuwa kila mgogoro una upekee wake unaoutofautisha na migogoro mingine. Kila kitu huwa na mgogoro wa ndani kwa ndani unaotofautiana na migogoro mingine. Jambo hili ndilo hutofautisha vitu mbalimbali. Ili kusuluhisha mgogoro wowote ule katika jamii lazima jambo linaloutofautisha na migogoro mingine libainike wazi. Katika kila mgogoro, kuna migogoro mingine midogo midogo ya ndani kwa ndani ambayo huchangia mgogoro mkuu. Mgogoro mkuu hubainika wazi zaidi huku migogoro mingine

midogo inayoijenga ikichukua nafasi ya pili hafifu Soo (1981). Anasema kwamba, ili kutatua mgogoro wowote ambao una migogoro mingine midogo midogo, ni muhimu kufanya kila juhudi kutambua mgogoro mkuu kwa sababu ndio huathiri na kuelekeza migogoro mingine midogo. Jambo hili likitambuliwa inakuwa rahisi kutatua kila mgogoro. Sura ya pili ilichanganua namna migogoro ya kimawazo ilivyowawezesha waandishi wa riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?* kukamilisha maudhui yao mbalimbali. Maudhui hayo yalidhihirisha ubia wa migogoro katika jamii kwani yalishughulikia matatizo yaliyojitokeza na kuathiri jamii nzima. Sura  hii inabainisha kuwa ubia huo wa migogoro huweza tu kutokea pale ambapo pana upekee wa migogoro kwani maudhui hayo yanakamilika tu kupitia kwa wahusika mbalimbali. Kwa kuegemea mhimili huu, sura hii imebainisha kwamba kupitia kwa wahusika hao migogoro mbalimbali ilitegemea migogoro ya kimawazo ya wahusika mbalimbali.

### 3.2.0 Namna Migogoro ya Kisaikolojia Ilivyomwezesha Mwandishi wa *Mkamandume* Kuwakuza Wahusika Wake.

Riwaya ya *Mkamandume* ina wahusika wengi. Kuna wahusika wakuu kama vile Mkamandume mwenyewe, Time ambaye ni mwanambee wa Mkamandume, Soud (mchumba wake Time), Tufaa (mkwewe Mkamandume) miongoni mwa wengine. Aidha, kuna wahusika wengine wadogo ambao ni wajenzi wa wahusika wakuu. Hawa wametumiwa kuwakamilisha wahusika wakuu. Wahusika hawa ni kama Mzee Mkasi, Kombo, Suguru, Bilal, Tukaije, Bwan Sleyyum, Viwe na kadhalika. Kwa kuwa kuna wahusika wengi waliotumiwa kuwakamilisha wahusika wengine katika kazi hii, ni wachache tu ndio waliochanganuliwa ili kuwawakilisha waliosalia. Kwa mujibu wa Woloch (2003), wahusika wote katika kazi ya fasihi ni muhimu ingawa kuna baadhi ya

wahusika wajenzi ambao majukumu yao huingiliana katika kazi hizo kiasi cha kwamba kuwachanganua wachache tu kunaweza kuwawakilisha waliosalia. Kwa msingi huu wahusika wakuu, waliochanganuliwa ni wanne. Wahusika hawa waliteuliwa kulingana na umuhimu wao katika riwaya hii. Hii ni kwa sababu, riwaya hii haingeweza kukamilika iwapo mmoja wao angeondolewa. Wahusika wakuu waliochanganuliwa ni: Mkamandume, Time, Soud, na Nadia. Wahusika wadogo waliochanganuliwa ni: Viwe, Mzee Mkasi, Bwan Sleyyum, na Tufaa. Hawa waliteuliwa kwa sababu ndio waliotoa mchango mkubwa zaidi kuwajenga wahusika wakuu. Aidha, sifa zao zinadhihirika wazi kupitia migogoro ya kimawazo inayotokea akilini mwao au mawazo yanayokinzana moja kwa moja na yale ya wahusika wakuu.

### 3.2.1 Mkamandume

Mkamandue ndiye mhusika mkuu katika riwaya hii kwani ndiye matukio yote yanamzunguka na ujumbe mkuu wa mwandishi unawasilishwa kupitia kwake. Migogoro ya mawazo inamsawiri mhusika huyu kama mtu katili. Kupitia kwa migogoro ya kimawazo, tunapata mustakabali wake kuhusiana na uhuru wa nchi yake. Dhamiri yake inamwadhibu kwa matendo ya zamani aliyowatendea wananchi wenzake kwa kisingizio cha kupigania uhuru. Mkamandume alifyeka vichwa vya watu wote waliodhaniwa kupinga harakati zao za kupigania uhuru. Mkamandume na marafiki zake kama vile Suguru na Silimia walikubali kuwa Valantia (vibaraka waliojitolea kulinda maslahi ya viongozi) na kuwacharaza viboko watu wasiokuwa na hatia mradi tu watu hao walishukiwa kutokuwa na nidhamu dhidi ya utawala mpya. Aidha, anamfyeka Bwana Shombo kichwa kwa kushambulia familia yake. Nafsi yake inazua mgogoro mawazoni mwake. Tunamwona akijisemea:

> Udhaifu wa ndani na nje; alijiambia. Mwele, mgonjwa, mbovu hapo ulipo na mbovu unakokwenda – utaweza? Aliisimanga nafsi yake. "Aaaa! Ulichimbuka ule unyama wake. Yule Mkamandume wa zamani akamwambia Mkamandume wa sasa. 'Sikiliza!' Mkamandume akasikiliza. "Wewe ni Mkamandume mwendelezaji ushujaa wa ukoo wako (uk. 481).

Hapa tunaona mawazo ya Mkamandume yakizozana iwapo ataweza kumuua Shombo au la kwani siye Mkamandume wa zamani. Hatimaye, sauti inayomhimiza kwenda kumuua Shombo inashinda. Baadaye, Mkamandume anafaulu kumfyeka kichwa Bwana Shombo.

> Kama kufumba na kufumbua, Mkamandume aliruka kwa nguvu za ajabu na kwa dhoruba moja la panga alimkata kichwa Bwana Shombo. Bwana Shombo hakuwahi hata kutoa ukwenzi wa maumivu au kutetea roho yake (Uk. 482).

Mbali na hayo, tukio la kumfyeka Mtemi kichwa pia lilidhihirisha ukatili wa Mkamandume. Aidha, tunabaini kupitia kwa mawazo ya Mkamandume kwamba ni mwoga. Mkamandume alipoingia pale kisimani bila kupiga hodi na kumwona Tukaije mkewe jirani akioga, alijilaumu kwa kutopiga hodi. Tukaije alimfanyia mzaha na kumwita aje amtwike hando. Mkamandume alipomaliza kumtwika, Tukaije aliangua kicheko na kumdhihaki Mkamandume. Punde anatokea Bwan Rajab aliyemsalimia Mkamandume lakini hakumjibu. Baadaye, Mkamandume aliingiwa na hofu kwamba Bwan Rajab angeenda kumwambia mumewe Tukaije kwamba Mkamandume alimnyemelea mkewe.

> "Mungu wangu we!" alitamka Mkamandume kimoyomoyo. "Atafikiri nini mumewe Tukaije, jirani yangu? Atasema nini fitina hii ikimfikia? Kafanya mambo makubwa mwanamke yule, Tukaije. Hata unyamavu wangu hautasaidia kitu. Utapalilia tu kadhia nzima, hasa kwa vile Bwan Rajab katoa salamu sikuitikia – maana yake nini?" (uk. 370)

Migogoro ya mawazo pia inadhihirisha sifa nyingine ya Mkamandume kama mwenye kisasi. Baada ya Soud kukutana naye kwenye hoteli na kumlipia chakula, anampandisha gari lake na kuanza kumweleza kadhia iliyoipata familia yake wakati alipoondoka kijijini.

Soud anamweleza Mkamandume kwamba kuondoka kwake kijijini kulifasiriwa kama kukimbia kwa kuogopa kushambuliwa na Bwana Shombo kwa kumnyemelea mkewe Tukaije. Hivyo, basi Bwana Shombo alipanga njama ya kuchoma familia ya Mkamandume ndani ya nyumba pamoja na Nadia aliyechukuliwa kuwa mtetezi wa Mkamandume dhidi ya shutuma alizolimbikiziwa. Jamaa yote ya Mkamandume iliokoka isipokuwa mgeni wao Nadia aliyeathirika vibaya kwa moshi uliomwingia mapafuni. Kupitia kwa mawazo ya Mkamandume mle garini wakiwa na Soud, mwandishi anatudokezea kwamba Mkamandume alikuwa amenuia kulipiza kisasi. Mgogoro huo unajitokeza Mkamandume anapowaza:

> Wanataka kumuua yeye na ukoo wake lakini watamuua mara ngapi mtu aliyekwisha kufa? … La, hataingia jitimai Mkamandume. Atakwenda na umaitihai pasi na kujali. Atakwenda hivyo hadi siku ya siku… siku ya siku… siku ya siku… Alijisikia akipiga kelele mle garini lakini hakuna aliyemsikia (uk. 448).

Wazo hili lilikuja kutimia Mkamandume alipomfyeka kichwa Bwan Shombo kulipiza kisasi kwa kuchomewa vibanda vyake. Aidha, kisasi chake kinadhihirika anapomfyeka bosi wake kichwa kwa kumwachisha kazi bila ya mshahara wowote hata baada ya kufanya kazi kwa miezi kadhaa. Hata marupurupu ya likizo hakupewa.

Migogoro iyo hiyo ya mawazo pia ilimbainisha Mkamandume kama mwenye ubinafsi. Jambo hili linatokea anapomchukua ng’ombe wao wa pekee na kumuuzia Soud. Anaondoka na pesa hizo zote pasi kujali ni yapi yangetokea au familia yake ingekidhi vipi mahitaji yake. Mkamandume alifahamu vyema kwamba kila mwaka familia yake ilistahili kumwaga damu kama kafara kwa pepo wa mababu zake aliyeilinda jamii yao. Alifahamu vyema kwamba ni huyo ng’ombe mmoja tu ndiye angetumiwa kukamilisha tambiko hilo. Hata hivyo, mbali na nafsi yake kumkanya asimuuze ng’ombe huyo,

anaghairi na kumuuzia Soud. Anachukua pesa zote – laki moja. Anatoweka nazo bila kujali Tufaa angefanyaje na watoto. Hakujali familia yake ingekidhi vipi mahitaji yake. (UK. 384 – 385).

Aidha, mawazo kinzani ya Mkamandume yalitudhihirishia kwamba Mkamandume alikuwa mwenye majuto. Alijutia maovu yote aliyoyatenda kwa kisingizio cha kutafuta uhuru huku akifyeka vichwa vya watu kwa kisasi tu alichokuwa nacho dhidi yao bali siyo kwa ushahidi wowote kwamba watu hao walikuwa wasaliti kama alivyowaita. Anapigana na dhamiri yake inapomkumbusha aliyoyatenda hapo zamani.

> Mara nyingi alizisikia zile sauti zake mbili…ile iliyopenda kumsimulia hadithi au historia ya Malelejimema. Hiyo hakupenda kuisikia tena siku hizi. Aliikemea waziwazi ilipomjia. 'Kwenda uko!' Bado hujatambua kwamba historia ya nchi hii imekwama pahala fulani na kwamba huwezi wewe kuiendeleza (uk. 382)

Mkamandume pia anajutia maovu aliyomtendea Mzee Mkasi. Nafsi yake inazua mjadala wa kumsuta na matendo ya kidhuluma aliyomtendea Mzee Mkasi huku wakati huu alikuwa ameshika njia kwenda kumkopesha pesa za kukidhi mahitaji yake. Hulka hii ya majuto pia inasisitizwa na mawazo ya majuto yanayomjia baada ya kufyeka shamba lao la mihogo. Nafsi yake inamsuta na anajutia tendo lake:

> Kitu gani umefanya Mkamandume? Umetatua tatizo kwa kulitatiza tatizo? Kumesaidia nini kufyeka kila kitu kondeni mwako? Umezidi kuikata tamaa yako (uk. 21).

### 3.2.2 Time

Time ni bintiye Mkamandume. Kupitia kwa migogoro mbalimbali ya mawazo tunapata kufahamu mojawapo ya sifa zake kama binti anayewajibika. Time alipotofautiana na babake kimawazo, sifa yake iliyodhihirika ni kwamba aliwajibika. Babake alikuwa na wazo kwamba shamba lao halikuwa na manufaa yoyote hivyo basi alifyeka mihogo yote na migomba iliyokuwamo. Hapo ndipo Time alimkabili na kumuuliza kwa ujasiri kwa

nini kafanya hivyo. Aliuliza hivyo kwa kuwa alijua kwamba shamba hilo ndilo lilikuwa tegemeo lao la pekee. Mbali na hayo, babake alipokataa posa ya mchumba wake Soud, Time alisononeka kwa muda mrefu sana. Hata hivyo, alibakia kujiheshimu kinyume na mtazamo wa wazazi wake waliomchukulia kuwa mtundu. Hata Viwe alipotungwa mimba, mama alishangaa sana kwani hakutarajia Viwe ashike mimba ila Time. Ingawa Time alikuwa na mchumba wake waliyependana naye sana wote wanaonyesha uwajibikaji wanapojiepusha na ngono kabla ya ndoa (uk. 98 na 160).

Vilevile, Time alionyesha sifa ya kuwa na mawazo mapevu. Haya yalidhihirika migogoro ya mawazo ilipotokea akilini mwake. Walikuwa wameenda kutembea na Nadia kwenye msitu na wakiwa pamoja, mawazo yake yalikimbia huku na kule. Hapo ndipo alipozozana na nafsi yake na kujiuliza kwa nini alimchukia na kumwonea wivu Nadia. Baadaye, alikuja kuikanya nafsi yake alipotanabahi kwamba Nadia hakuwa na hatia wala kutambua kwamba Time alikuwa mchumba wa Soud. Aidha, migogoro mawazoni mwa Time ilimfanya kubaini kwamba Malelejimema kulikuwa na matabaka mawili makuu – ya walalahoi na walalaheri. Ndiyo maana anajiuliza.

> Kwa nini kijiji kile kimekuwa na vibanda na vijumba vile karne zote zile? Kwa nini nyumba mbili tatu tu ndizo zilizokuwa na maana ya nyumba? (uk. 196)

Aidha, Time alikuwa mwenye mapenzi ya dhati. Alidhihirisha mapenzi haya kwa Soud aliposononeka baada ya kupitiwa na mawazo akilini kuhusu mustakabali wake na Soud huku akifahamu vyema kwamba Soud na Nadia waliishi pamoja. Time alishangaa kwa nini alimmwagia Soud mapenzi tele lakini Soud hakuweza kuyaona. Alijiuliza kwa nini Soud aliitikia mapenzi yake kwa unyamavu na mapuuza. Alighadhabika kwamba Soud alimpuuza na juhudi zake zote za kumwonyesha mapenzi kwa sababu babake

(Mkamandume) alikataa posa ya Soud. Alijua kwamba Soud alikuwa anampenda lakini kavunjwa moyo na mzee wa Time. Alishangaa kwa nini Soud hakungojea kuvunjwa moyo na yeye Time ndipo afanye hasira. Alishangaa ni vipi mapenzi ya kweli yanaweza kuisha (uk. 334)

Migogoro ya kimawazo pia ilimdhihirisha Time kama mhusika jasiri. Mawazoni mwa Mkamandume, alishangaa kwa nini Time na ng'ang'anizi zake alitaka kuolewa na hasimu wake (uk. 205). Mawazo ya Time na ya babake yalipogongana kuhusu tendo la babake la kukata mihogo shambani, Time alimkabili babake kwa ujasiri na kumuuliza bila ya woga. Aidha, hapo ndipo alipata fursa ya kumkabili babake kuhusu penzi lake kwa Soud. Hata babake alipomjongea kwa hasira kwa sababu ya kumtaja Soud, hakushtuka hata kidogo, alimtazama tu.

### 3.2.3 Soud

Soud ni mmojawapo wa wahusika wakuu ambao sifa zao zimedhihirishwa vyema zaidi kupitia kwa migogoro ya kimawazo inayojitokeza akilini mwake na katika akili ya wahusika wengine. Soud alikuwa mtu mwenye msimamo imara. Katika mazungumzo yake na Bwan Sleyyum, Bwan Sleyyum alitaka Soud amwoe bintiye Shafiqa kwa kuwa huo ulikuwa mpango uliowekwa wakati wazazi wa Soud walipokuwa hai. Hata hivyo, Soud hakumpenda Shafiqa na alimwambia Bwan Sleyyum waziwazi kwamba asingeridhia ndoa hiyo. Ingawa Soud alimheshimu sana Bwan Sleyyum, hakukubali kushawishiwa naye kujiingiza katika ndoa pasi na mapenzi. Sifa hii ya Soud ilidhihirika kupitia kwa migogoro ya mawazo akilini alipowaza:

> Kinyume cha mambo! Kuikimbia ndoa ya kulazimishwa kwa kufuata ndoa ya kulazimishwa maana kama hii anayoiita Bwan Sleyyum na Bi. Mwana si ndoa ya kulazimishwa ni nini? (uk. 270).

Mawazo ya Soud yalikinzana na yale ya wazazi wake kuhusu utabaka. Alishangaa ni kwa nini mamake alimweleza kwamba kunao binadamu walio bora kuliko wengine huku mafunzo ya kidini yakimwelekeza kwamba hakuna binadamu bora kuliko mwingine. Ukinzani huu wa mawazo unamdhihirisha Soud kama mwenye utu. Soud alijiuliza maswali mengi kuhusu msimamo wa wazazi wake na hakuamini kwamba Mungu mwenye uwezo na huruma na mhimiza haki awe na mkono wa ubaguzi. Alibaki tu kulaumu kwa nini wanadamu walikuwa na mazoea ya kumzulia Mungu uongo kiasi hicho (uk. 220). Tofauti na wazazi wake, Soud alitambua kwamba damu ni damu tu na ni nyekundu kwa kila mtu. Mwandishi anazidisha mgogoro huu kwa kutuonyesha taswira ya wazazi wa Soud walivyowakandamiza wanyonge kama vile Kinda na wafanyakazi wao wengine. Ukinzani mwingine wa kimawazo ambao ulimdhihirisha Soud kama mwenye utu ni ule uliojitokeza alipowaza na kujiuliza kwa nini maisha yawe nusura kwa binadamu fulani na yawe angamizo kwa binadamu mwingine. Aliona kuwa maisha yalikuwa kinyang’anyiro na hivyo basi wanjanja na wenye nguvu ndio walioshinda. Haya yote yalimpitia akilini kwa sababu ya taswira ya ki-Mwajuma kilichokuja kumwomba sukari (uk. 127-128).

Tukio hili pia lilidhihirisha sifa nyingine ya Soud kama mtu karimu. Alimpa Mwajuma sukari yote iliyobaki bila kujali maslahi yake kwanza. Aliwazia chanzo cha hali ile katika nchi yake ya Malelejimema. Aliwaza kwa nini mambo yalikuwa yamebadilika ghafla na kuwa mabaya. Hapo awali, Malelejimema iliongoza kwa wingi wa mapato, nafasi za elimu ya juu, milki na nguvu za benki. Mabadiliko haya yalimsononesha kwa kuwa

hakutaka kuwaona watu wakihangaika. Aligharamia kesi zao kwa kujitolea na pesa zake mwenyewe.

Soud pia alikuwa kijana mwadilifu na aliyeheshimu watu wakubwa kwa umri. Hii ndiyo maana anapendwa na Bwan Sleyyum ambaye alisisitiza ndoa kati yake na bintiye Shafiqa itokee. Ni heshima yake kwa Bwan Sleyyum ndiyo ilimfanya asimkabili moja kwa moja kwamba ndoa kama hiyo haikuwa haki bali kulazimisha vijana waoane pasi na mapenzi. Ndiyo maana mwandishi anasema:

> Soud alitaka kumfunulia Bwan Sleyyum utata huu, lakini hakudhubutu. Yeye Soud haungi mkono ndoa yoyote ya kulazimishana kwa sababu zozote zile zilizopo. Alijiasa kukataa ndoa zote hizo (uk. 270)

Vilevile uadilifu wake ulidhihirika kupitia kwa migogoro ya mawazo iliyojitokeza akilini mwa Nadia. Ingawa Soud aliishi na Nadia katika nyumba moja hakuwahi kuzini naye hata ingawa Nadia alikuwa amemwonyesha ishara za wazi kwamba alimpenda.

Mbali na hayo, Soud alikuwa na utu. Haya yalidhihirika mawazo yake yalipokinzana na mawazo ya babake. Hakupendezwa na jinsi wazazi wake walivyowakandamiza wafanyakazi wao. Soud aliwachukulia akina Msafiri, Mpikachai na Maliyatabu kama binadamu waliostahili kutendewa wema na kuheshimiwa. Mawazo yake yalitofautiana kabisa na yale ya babake aliyeamini kwamba hakukuwa na tofauti yoyote kati ya wafanyakazi hao na hayawani. Hivyo basi, hawakustahili heshima zozote. Haya yote yanadhihirika mwandishi anaposema:

> Lakini Soud aliyapuuza yote hayo. Alihisi hiyo ilkuwa njia ya pekee kugomea kitu kisicho halali kinachotendwa na ukoo wake (uk. 219).

Utu wake Soud pia ulidhihirika katika mgogoro wa kimawazo alipofikiria kwamba wazazi wake walikiuka mafundisho ya kidini walipowanyanyasa na kuwatesa wanyonge kama Kinda. Kwa mujibu wa mafundisho ya kidini aliyoyapata alifundishwa kwamba

Mungu hana ubaguzi na hivyo basi hakuna binadamu bora kuliko binadamu mwingine. Soud alitambua damu ni damu –nyekundu kwa kila mja (uk. 222 – 223).

Soud pia alikuwa na msimamo imara. Hakutetereka katika msimamo wake kuhusu masuala fulani. Migogoro katika mawazo yake ilitudhihirishia haya alipoitwa na Bwan Sleyyum na kujaribu kumshinikiza amwoe bintiye – Shafiqa. Mawazoni mwake alijua kwamba alimpenda Time na hivyo basi kubadilika na kuanza kumpenda Shafiqa kulikuwa kugumu. Hivyo basi, hata vishawishi vya Bwan Sleyyum havikumfanya kubadili msimamo wake. (uk 266)

Migogoro ya mawazo iliyompitia akilini Nadia, inadhihirika kwamba Soud alikuwa msaliti. Usaliti wa Soud ulidhihirika mawazoni mwa Nadia ambaye alionyesha dalili zote za kumpenda na hata kumfuata kwao Malelejimema baada ya Soud kumaliza elimu yake kule ng'ambo. Mwandishi alitudhihirishia kwamba Nadia alisalitika kimapenzi na Soud. Ingawa hakuwa amemwambia Soud alivyohisi kumhusu, ishara zote alizomwonyesha Soud zilikuwa ithibati tosha kuhusu penzi lake kwa Soud. Mawazoni mwa Nadia, alijiuliza kwa nini alitoka London kuja Malelejimema. Alishangaa ni kitu gani kilichomleta huku kusiko hata na chembe ya tamaa. Mawazo katika akili yake yalikinzana kuhusu furaha au maana ya furaha kwani nafsini mwake alifahamu fika kwamba kilichomleta huku kilikuwa penzi lake kwa Soud. Hata hivyo, alisononeka kwa sababu Soud hakuonyesha dalili zozote za kumpenda hata ingawa alikuwa ameashiria hilo walipokuwa kule Uingereza. Haya yanadhihirika wazi zaidi pale mwandishi anapotuonyesha mawazo ya Nadia akisema:

> Mpaka sasa Soud amekubali kumpa Nadia suhuba na urafiki lakini amemnyima kile anachokitaka yeye Nadia; yaani mapenzi. Au tuseme Soud anajifanya kipofu ingawa macho anayo (uk. 116).

Vilevile, usaliti huu wa Soud ulijitokeza kupitia kwa mawazo ya Time. Penzi la Soud na Time lilichipuka wakiwa wangali wachanga na Soud alifahamu vyema namna Time alivyompenda kwa dhati. Hata hivyo, Soud aliamua kukata tamaa kabisa posa yake ilipokataliwa na Mkamandume. Alimpuuza Time kabisa hata ingawa moyo wake ulikuwa ungali unampenda. Haya yote tuliyabaini kupitia kwa mikinzano ya mawazo akilini mwa Soud. Soud alijaribu kujifanya kwamba hisia za mapenzi kumhusu Time ziliisha ilhali angali anaumia ndani kwa ndani.

Time pia alisononeka kwa sababu ya penzi lake kwa Soud kukataliwa na babake. Alihisi kwamba alikuwa amevunja miiko ya Wamalelejimema kuhusu namna msichana alivyostahili kuonyesha penzi lake. Hata hivyo, jambo hilo halikumtia machungu kuliko alivyojiona kapuuzwa na Soud. Mawazo haya yote yanatudhihirishia kwamba kweli Soud kamsaliti Time kwa kumwacha kupigania penzi lao peke yake (uk. 160)

### 3.2.4 Nadia

Nadia alikuwa msichana Mwingereza aliyependana na Soud alipoenda kusomea Uingereza. Mhusika huyu alitokea kuwa muhimu kwa sababu ndiye alikuwa chanzo cha migogoro ya kimawazo akilini mwa wahusika wawili wakuu – Soud na Time. Kupitia kwa Nadia mwandishi alifaulu kuzua migogoro akilini mwa Soud na Time kuhusu penzi lao. Migogoro iyo hiyo ndiyo iliyotulibainishia sifa za Nadia kama mtetezi wa haki, msiri, msamehevu, karimu na jasiri. Nadia alijitokeza kama mtetezi wa haki. Mojawapo ya sababu zilizomleta Malelejimema ni kutafuta haki dhidi ya mauaji ya nyanyake na kutafuta penzi la Soud (uk. 352). Mkamandume aliposingiziwa kuwa na uhusiano wa

kimapenzi na Tukaije mke wa jirani yake, Nadia alimtetea kwa kueleza ukweli kwamba Mkamandume hakuwa na hatia kwani alikuwapo katika kisima kile Tukaije alipomwomba Mkamandume amtwike lile hando.

Mbali na sifa hiyo ya utetezi wa haki, Nadia alidhihirika kama mtu msiri. Sifa hii ilijitokeza kupitia kwa migogoro ya mawazo iliyomjia walipokuwa na Time. Hakuwa na hakika iwapo ilikuwa salama kumwamini Time na kumfichulia penzi lake kwa Soud au la. Time na Nadia walisimuliana hadithi za maisha yao ya mapenzi. Nadia ndiye aliyetangulia na hakuweza kumfichulia Time kwamba kijana aliyeiteka bakunja nafsi yake alikuwa ni Soud. Anafaulu kuficha siri hiyo kwa kuwa alishuku kwamba Time pia alimpenda Soud kwa hivyo halikuwa jambo la busara kumfichulia mpezi wake alikuwa nani. Sifa hii ya usiri kwa Nadia inadhihirika kwa kupitia mawazo yake anapowaza:

> Toba! Nani huyo Mungu wangu! Moyo wa Nadia ulimgutuka … kweli au uongo … vipi miaka yote aliyoishi hapa asijue kwamba Time anampenda kijana mwenyeji wa pale? (uk. 360 &131)

Kupitia kwa mawazo hayo kinzani ndipo pia mwandishi anazidi kumjenga Nadia kama msiri anapoonekana amesononeka kuhusu penzi lake lisilojibiwa na Soud. Nadia na Soud walikuwa wakiishi katika nyumba moja na alikuwa amemwonyesha Soud dalili zote kwamba alikuwa akimpenda. Hata hivyo siri ya penzi lake kwa Soud ilibakia moyoni mwake bila kumtamkia hata siku moja mpaka wakati Nadia alipoamua kurudi kwao Uingereza kwa sababu ya matibabu. Alimtamkia tu pendo hilo katika uwanja wa ndege aliposema:

> Niwie radhi kwa mapenzi yangu ya kitoto niliyokuonyesha kwa ishara siku zote pasi na kukutamkia. (uk. 455)

Migogoro ya mawazo pia ilituwezesha kubaini kwamba Nadia alikuwa msamehevu. Nadia alifanya uchunguzi wake Malelejimema na kuwafahamu watu waliowaua wazee wake. Watu hawa walikuwa: Silimia, Suguru na Mkamandume. Alitaka Mkamandume amwombe msamaha na Mkamandume alipogugumka na kuanza kulia, Nadia alifasiri hilo kuwa toba ya Mkamandume na akamweleza kwamba alikuwa amemsamehea (uk. 459).

Kisa cha ki-Mwaju kinaonyesha kwamba Nadia ni karimu. Mawazo ya Nadia yanatuthibitishia kwamba alikuwa TX yaani bingwa wa kigeni na hivyo basi aliruhusiwa kununua bidhaa zake katika duka hilo lililosheheni kila kitu ili wageni wasihisi usumbufu wowote. Nadia alimfadhili Soud kwa mambo mengi. Hii ni kwa sababu Soud alishindwa kupata kazi tangu afuzu. Mbali na kumfadhili Soud, ukarimu wa Soud wa kuwapa majirani walichokosa kila mara walipokuja kuomba kwake hakukumuudhi Nadia. Mwandhishi anaeleza:

> Nadia hakuwa na kizuizi naye Soud seuze kuwa na kizuizi katika kumpa alichotaka na alipopenda (uk. 127).

Mawazoni mwake Nadia aliwazia kuhusu maana ya ushenzi na uungwana. Aliona kwamba neno ushenzi ni neno la kiburi tu ambalo hutumika maksudi kuwadhalilisha watu ili kuwatawala kwa urahisi. Hakukubaliana na maoni yaliyoshikiliwa na upande mmoja wa nafsi yake kwamba uungwana ni maendeleo ya sayansi, teknolojia na mashini. Upande kinzani wa nafsi yake nayo ilisisitiza kwamba uungwa ni kumjali binadamu na utu wake. Imani hii ya pili ndiyo iliyompa motisha ya kuijenga hulka yake kama mtu jasiri kwani alipigania haki za Wamalelejimema huku akijua fika kwamba watu alioshindana nao walikuwa na mamlaka makuu serikalini na walikuwa na uwezo wa kumfanyia chochote, hata kumwangamiza. Ujasiri huu wa Nadia ulijitokeza katika

mawazo ya Soud (Uk. 445). Mashambulizi aliyokumbana nayo Nadia yalitokana na ujasiri wake wa kukabiliana na viongozi na kupinga dhuluma zao dhidi ya Wamalelejimema.

Mbali na wahusika hawa wakuu, kulikuwa na wahusika wengine wadogo ambao waliwajenga na kuwakamilisha wahusika wakuu. Wahusika hawa walikuwa: Mzee Mkasi, Bwan Sleyyum, Viwe, Tufaa miongoni mwa wengine. Migogoro ya mawazo ya wahusika hawa iliwakuza kwa njia zifuatazo:

### 3.2.5. Mzee Mkasi

Mzee Mkasi ni mmojawapo wa wazee wa Malelejimema waliodhulumiwa wakati wa kupigania uhuru wa Malelejimema. Kupitia kwa mawazo yake, inabainika kwamba mzee huyu ni mwenye busara. Aidha, kwa mawazo ya Time, tunatambua kwamba Mzee Mkasi kama mwenye busara. Time anashangaa kwa nini Mzee Mkasi aliogopa kuchinja kuku na jibu alilopewa na mzee huyo halikuridhisha. Mzee Mkasi alimwambia kwamba ameshaona damu nyingi ikimwagika na hivyo basi asingependa kuona ikimwagika tena – siyo hata ya kuku. Hata hivyo, Time hakufahamu kwamba ni busara ya Mzee Mkasi ilimfanya amwachie kuku amchinje. Kwa mujibu wa tamaduni za kimalelejimema, mwanamke hakuruhusiwa kumchinja kuku. Hata hivyo hekima ya Mzee Mkasi inamfanya kutambua kwamba ulimwengu ulikuwa umeanza kubadilika na hivyo ingekuwa bora kubadilika nao hasa kwa kuacha mila zisizo na msingi wowote ila kuwanyanyasa wanawake.

Aidha, mawazo ya Mzee Mkasi yanaonyesha kwamba ni hekima iliyomwezesha kung’amua kwamba nyakati hizo hazikufanana na zile za zamani ambapo wazee

waliwachagulia watoto wao wachumba nao watoto wakakubali kufuata matakwa ya wazazi bila ya maswali. Anatambua bila kuelezwa kwamba jambo hilo ndilo lilimnyima raha Time (uk. 177). Aidha, mawazo ya Mkamandume yanabainisha kwamba Mzee Mkasi alikuwa msamehevu. Mawazo hayo yalionyesha madhila yote aliyotendewa Mzee Mkasi na Mkamandume yakiwemo kumsingizia kuwa msaliti aliyeipinga serikali ya baada ya uhuru. Jambo hili lilimfanya Mzee Mkasi kufungiwa ndani na kuteswa sana (uk. 379). Hata hivyo, mawazo ya Mkamandume yanadhihirisha kwamba Mzee Mkasi alimsamehe. Hata namna Mzee Mkasi anavyomkaribisha Time kwake na kumpa chakula kulionyesha kwamba hakuwa na kinyongo na babake – Mkamandume.

Mzee Mkasi pia alijitokeza kama mshauri mwema. Baada ya kuulizwa swali na Time ni kwa nini wazee huwachagulia watoto wao wachumba badala ya kuwaachia uhuru wao wajichagulie, Mzee Mkasi anamjibu kwamba hakuna mzazi anayemtakia mtoto wake mabaya hivyo ni vizuri kuwasikiliza hata ingawa wazazi nao wanastahili kuwaachia vijana nafasi ya kujichangulia wachumba kwani nyakati hizo zilikuwa za mabadiliko. Aidha, alimshauri Time dhidi ya kuchukua msimamo katika hali yoyote ile bila kuwa na sababu ya kutosha au kuthibitisha msimano huo. Alimweleza Time kwamba hiyo ndiyo sababu iliyomfanya kutounga mkono upande wowote wakati wa vita vya uhuru kwani hakuwa na sababu yoyote ya kuunga mkono upande wa Wakoloni au wenyeji. Alifahamu kwamba pande zote hazikuwa na haki ya kushambulia upande pinzani kwa kuwa wote walipaswa kulaumiwa na hakuna upande uliosimamia haki (uk 181).

Mawazo ya Soud pia yalionyesha kwamba Mzee Mkasi alikuwa mtu mwenye bidii. Aliwaza namna alimpata kondeni mwake kila mara alipomtembelea. Hata siku walipoenda kumtembelea na Nadia, Soud alishangaa kwamba kwa mara ya kwanza Mzee

Mkasi hakuwa shambani mwake wakati huo. Kuku wengi aliowafuga pia ilikuwa ishara ya bidii yake.

### 3.2.6 Bwan Sleyyum

Mawazo kinzani ya Soud yalikumkuza Bwan Sleyyum kama mwajibikaji. Mawazo hayo yaliturudisha nyuma na kutuonyesha namna wakati mmoja Soud na Bwan Sleyyum walikuwa na misimamo tofauti kuhusu ndoa iliyopangwa na wazazi wa Soud na familia ya Bwan Sleyyum. Uwajibikaji wake ulionekana alipochukua fursa ya kumwelekeza Soud kuhusu ndoa baada ya wazazi wake Soud kuaga dunia. Aliwajibika kama mzazi kwa sababu hakutaka bintiye Shafiqa alazimishiwe ndoa kama ilivyokuwa imeshuhudiwa hapo Malelejimema baada ya uhuru. Soud alikataa mpango wa wazazi wake kumpangia ndoa. Alifahamu kwamba hakumpenda Shafiqa bali Time. Hata baada ya ombi la Bwan Sleyyum kukataliwa na Soud, hakufa moyo. Alihakikisha kwamba Shafiqa kaolewa kule Uarabuni ili amwepushie dhiki ya kulazimishiwa ndoa pale Malelejimema. Uwajibikaji wa Bwan Sleyyum pia ulionekana pale alipomshauri Soud aache kujihusisha na masuala ya siasa za Malelejimema. Hata ingawa Soud alimkataa bintiye Shafiqa, Bwan Sleyyum bado alimtakia mema na hakutaka mabaya yoyote yamfike.

Bwan Sleyyum pia alijitokeza kama mwoga. Alipomwalika Soud kwake alimwonya kwamba kupigania haki za Wamalelejimema kulikuwa ni kuhatarisha maisha yake hivyo basi alipaswa kufikiria tena mustakabali wake ili asihatarishe maisha yake. Sleyyum aliamini kwamba Soud alikosa ajira kwa sababu ya msimamo wake kisiasa. Jambo lililomtia wasiwasi zaidi ni kwamba Soud alikuwa akiandikia habari vyombo vya kimataifa kama vile BBC na VOA na habari alizoziandika zilihusu uozo nchini

Malelejimema. Jambo hili linamwogofya sana Bwan Sleyyum kwani alifahamu kwamba maisha ya Soud yalikuwa hatarini na angeyapoteza wakati wowote kwa kuwa vigogo wa Malelejimema hawakutaka maovu hayo yaanikwe hadharani. Hii ndiyo maana alimuuliza Soud kama haogopi. Soud alikiri kwamba aliogopa lakini kila mtu alistahili kupigania haki licha ya woga kwani woga ndio uliwatia nguvu zaidi viongozi dhalimu. Woga wa Bwan Sleyyum ulidhihirishwa vema zaidi kwa mawazo yake aliposema:

> Usiwasaidie Soud Waswahili. Epukana nao. Usijijishughulishe na mambo yao. Ni watu wabaya. Mara wanaweza kukupotezea maisha yako (uk. 303).

Sifa nyingine ya Bwan Sleyyum inayojitokeza mawazoni mwa Soud ni kwamba alikuwa mwenye utu. Kwa mujibu wa mawazo hayo, Bwan Sleyyum alikuwa mweledi wa dunia na akhera na mtiifu wa Mola wake. Alijua kwamba alifaa kula na kunywa lakini asifanye isirafu kwani Mungu amekataza isirafu katika kitabu chake. Mbali na hayo, utu wake unazidi kujitokeza wakati Soud alikataa kumwoa bintiye Shafiqa lakini hamwekei kinyongo bali anazidi kumtakia mema na kumwonya aachane na siasa kwani ingehatarisha maisha yake (uk. 273).

### 3.2.7 Viwe

Viwe alikuwa binti wa pili wa Mkamandume. Migogoro ya mawazo ya Viwe yanamkuza kama mtu mzinifu au mtovu wa maadili. Mawazo yaliyompitia akilini, yalidhihirisha kwamba alikuwa na mimba ingawa hakuwa ameolewa. Jambo hili lilimwingiza wasiwasi hasa alipokumbuka kwamba Mkamandume alikuwa babake. Katika jamii hii ya Malelejimema utamaduni haukumruhusu msichana kushika mimba nje ya ndoa. Inakuwa kioja binti yeyote anapopata mimba nje ya ndoa. Jambo hili ndilo lilimtisha zaidi Viwe kwani alifahamu vituko vya babake. Mkamandume aliogopwa siyo tu na jamaa yake bali

hata na wanakijiji wote. Haya yalitokana na ukali wake na ubaradhuli aliouonyesha umma wakati wa kupigania uhuru wa Malelejimema kwa kuwafyeka watu vichwa. Viwe alipokumbuka hayo yote, alijutia usherati wake kwani hakujua ni jambo lipi lingetokea iwapo babake angengundua kwamba bintiye Viwe ambaye alimwamini kuliko Time ndiye alikuwa na mimba. Sifa hii ya Viwe inajitokeza tu kwa sababu ya migogoro hiyo ya mawazo inayompitia akilini (uk. 97). Mkamandume alipokuja kugundua baadaye kwamba Viwe alikuwa mjamzito, alimpiga nusura amuue na kumfukuza nyumbani.

Mbali na kuwa Viwe ni msherati, pia alikuwa msamehevu. Sifa hii ilidhihirika alipowazia namna alivyofukuzwa na babake kutoka nyumbani miaka mingi iliyopita akatorokea Makao Makuu na kuanza kuhangaika. Alipoingia mjini alikuwa mjamzito na jiji likamkaribisha kwa uzito mkubwa kuliko ule wa tumboni. Alipita huku na kule mpaka hatimaye akafanikiwa kupata kazi ambayo aliifanya kwa bidii na kujiendeleza kimasomo. Baadaye anafanikiwa maishani na kuanzisha kundi la vijana lililopigania haki za wanyonge kupitia kwa uigizaji. Viwe alipokutana na babake baada ya miaka mingi, wanakumbatiana na kutiririkwa na machozi. Vivyo hivyo, hata mtotowe Viwe aliitwa Mkamandume – jina la babake, kuonyesha kwamba hakuwa na kinyongo na babake kwa kumfukuza nyumbani. Yote alikuwa amemsamehe babake (uk. 467)

Viwe pia anajitokeza kama msiri. Aliweza kuuweka ujauzito wake kuwa siri yake bila ya kumwambia yeyote. Kupitia kwa mawazo ya Viwe, tunapata kuwa mbali na kumwambia mamake tu, hakuna mtu mwingine aliyefahamu kuhusu ujauzito wake mpaka siri hiyo inapokuja kujifichua yenyewe Time anapompata Viwe akitapika usiku huku mama yao akimhimiza afanye hima siri yao isifichuke. Aidha mawazo yayo hayo, yanamkuza kama

mnafiki. Taswira aliyowapa wazazi wake ni kwamba alikuwa msichana mpole, mtulivu na mwenye kuzingatia maadili. Kwa sababu hii, wazazi wake walimpenda na kumtumia kama kielelzo bora kwa Time ambaye kwa upande wake alichukuliwa kama mtovu wa nidhamu asiyetulia hata kidogo. Sifa hii ya unafiki inadhihirika vyema Viwe anapowaza:

> Mimba yake ndiyo kioja na ndiyo ukorofi. Ndiyo aibu na fedheha. Hata Mkamandume babake anayejionyesha na kumsifu Viwe kijuujuu tu kila siku kwa upole na utulivu wake atamwonaje sasa? (uk. 98).

### 3.2.8 Tufaa

Tufaa ni mkewe Mkamandume. Yeye pia anakuzwa kitabia kupitia kwa migogoro ya mawazo. Sifa yake iliyokuzwa kutokana na migogoro ya mawazo ni ustahimilivu. Ustahimilivu wake unajitokeza kupitia kwa mawazo yake mwenyewe. Mwandishi anatuonyesha kwamba Tufaa alipigana na nafsi yake dhidi ya kumchukia mwanawe ki-Katija kwa kupata penzi la Mkamandume na kudekezwa:

> Kwa nini anakichukia ki-Katija siku hizi? La, la la … alikataa Tufaa kulipisha wazo la chuki kwa kitoto chake chenyewe alichokizaa (uk. 15).

Chanzo cha chuki ya Tufaa dhidi ya kitoto chake ni kupuuzwa na mumewe kimapenzi na kuhamishia mapenzi hayo kwa kitoto hicho ki-Katija. Mbali na hayo, inadhihirika kwamba Mkamandume alikuwa kabadilika kweli. Ucheshi na uchangamfu wa mumewe ulikuwa umepotea kabisa badala yake amekuwa moto unaorindima bila kuzimika. Siku hizi ilibidi Tufaa kumridhi Mkamandume zaidi kuliko alivyomridhi tokea awali. Umaskini uliwaandama kotekote na hata Mkamandume aliposhindwa kabisa kuikimu familia yake na kutorokea mjini baada ya kumuuza ndama wao mmoja tu aliyebakia, Tufaa bado alivumilia tu na kuendelea na maisha. Ingawa kaachiwa mzigo mzito

uliomshinda mume wake. Haya yanadhihirisha kwamba mhusika huyu ni mvumilivu na sifa hii ilidhihirishwa kutokana na migogoro yake ya kimawazo (uk. 13).

Tufaa pia anajitokeza kama msaliti. Alimsaliti mumewe kwa kuficha siri kwamba binti yao Viwe alikuwa mjamzito. Hata alimkanya Bi. Reja kuweka jambo hilo siri na Time vilevile alikanywa asimtajie Mkamandume jambo lolote. Mbali na kwamba alikuwa msaliti, jambo hili lili fungamana na sifa yake nyingine kama mtu msiri. Anaweka siri ya Viwe kuwa mjamzito mpaka inapofichuka yenyewe.

### 3.3.0 Migogoro ya Kisaikolojia na Ukuzaji wa Wahusika Katika Riwaya ya *Unaitwa Nani?*

Tofauti na riwaya ya *Mkamandume*, riwaya ya *Unaitwa Nani* (2012) yake Wamitila K. ina wahusika wakuu wawili tu, yaani Mwanamke na Mwanamume. Wahusika hawa wamekuzwa kupitia kwa hadithi mbalimbali zinazowahusu wahusika mbalimbali ambao lengo lao kuu kutumiwa ni kukuza hulka za wahusika hawa wawili wakuu. Hii ndiyo maana riwaya hii imegawanywa katika sehemu mbili kuu – sehemu ya kwanza inayosheheni hadithi mbalimbali zinazokuza hulka mbalimbali za mwanamke na sehemu ya pili ambayo pia inahusu hadithi mbalimbali zilizotumiwa kukuza hulka za mhusika mwanamume. Sehemu hizi mbili za riwaya hii zinahusu masimulizi ya mawazoni ya wahusika hawa wawili; Mwanamke na Mwanamume. Wahusika wote wawili wamelazwa hospitalini wakiwa mahututi.

Temmerman (2014) anasema kwamba waandishi wa riwaya katika karne hii wametambua namna ya kuwasawiri wahusika wao wakuu na kuwawezesha kuthibiti mamlaka juu ya mazingira yao. Anasisitiza kwamba usawiri wa namna hii unamwalika msomaji wa riwaya kuwachanganua wahusika hao kwa kuzingatia kiini au kisababishi cha tabia zao. Kwa kuzingatia maoni haya uchanganuzi huu ulijikita katika kuchunguza kiini cha tabia za wahusika mbalimbali na kubainisha namna hali zao kiakili zilivyoathiri uhusiano wao na wahusika wengine na mazingira yao. Kupitia masimulizi ya Mwanamke (Kasekesi) tunapata hulka mbalimbali za Mwanamke. Kwa mujibu wa sehemu ya kwanza, mwanamke anaoneka mwenye hulka zifuatazo:

### 3.3.1 Mwanamke

Sifa zote za mwanamke zilizoangaziwa katika sehemu hii zilitokana na mikinzano ya kimawazo inayojitokeza akilini mwa Mwanamke aliyelazwa hospitalini akiwa mahututi. Masimulizi mbalimbali yanayotokea akilini mwa mwanamke yanatudokezea hulka zake. Katika sehemu ya kwanza, sifa nyingi za Mwanamke zilizoangaziwa ni chanya huku sifa nyingi zinazojitokeza katika sehemu ya pili zikiwa hasi. Ibainike kwamba sehemu ya kwanza ya riwaya hii imekuza sifa hizi kwa mtazamo wa kike huku sehemu ya pili ikikuza sifa za mwanamke kwa mtazamo wa kiume. Kwa mujibu wa DiBattista (2010), mhusika katika kazi ya fasihi anastahili kupewa uwezo wa kukua kutoka pande zote kwa kumwachia nafasi ya kuonyesha uwezo wake unaotoka ndani kwa ndani na jambo hili linawezekana tu iwapo atapewa fursa ya kuibua mawazo yake kwa njia ya moja kwa moja. Jambo hili limejitokeza katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2012) kwani wahusika wake wamepewa fursa ya kuonyesha mawazo yao kwa njia wazi zaidi. Kupitia kwa masimulizi yanayotokea mawazoni mwa Mwanamke, sifa zake zinazojitokeza kama:

### 3.3.2 Mwanamke ni Mvumilivu

Msimulizi (Kasekesi) ambaye amelazwa hospitalini akiwa mahututi anaanzisha masimulizi yake kwa kusimulia kisa cha maisha yake binafsi. Maisha ya Kasekesi yalikuwa ya masumbuko mengi. Kwanza, alipoteza wazazi wake wote wawili katika ajali mbaya ya barabarani. Pili, anaozwa kwa Agusto Muridhania aliyekuwa tajiri kupindukia. Baadaye, mumewe alifilisika na kuwa mlevi sana. Hapo ndipo matatizo ya Kasekesi yalipoanza. Mumewe alikunywa pombe hadi akaaga dunia. Jamaa za mumewe wakamsingizia kwamba ndiye aliyemuua mumewe. Walimpa mkorogo wa dawa za kienyeji ili akiri kumuua mumewe lakini alikataa katakata. Mwishowe, walimvua nguo na kumvisha matawi wakimtembeza katika kijiji kizima. Walimtesa sana wakitarajia kwamba angekufa au mizimu ingemwadhibu kwa kumuua mumewe lakini hakufa. Alipokosa kufa, walimfukuza. Hapo ndipo anaamua kwenda kwa shangazi yake. Anavumilia mateso hayo na hata alipoenda kwa shangazi yake; huko nako alifukuzwa baada ya siku chache shangazi yake akiamini kwamba angemletea bahati mbaya.

Mbali na hayo, mashauri aliyopewa Kasekesi na mamake yanadhihirisha kwamba mwanamke ni mtu mvumilivu. Utamaduni wa jamii yao ni ule wa kumdhalilisha mwanamke. Mawazo ya mama (anapomshauri Kasekesi) yanakinzana na yale ya baba. Mawazo haya yote yanadhihirisha kwamba mwanamke ni mtu mvumilivu hasa ikizingatiwa kwamba utamaduni wa jamii hii ni ule wa kumdhalilisha mwanamke. Mamake Kasekesi anavumilia maonevu ya kijinsia na kuishi na mumewe hadi wanapopata ajali barabarani na kuangamia. Kutokana na mashauri ya mama kwa Kasekesi, inadhihirika kwamba mke alistahili kukaa jikoni. Mama alimshauri Kasekesi

kwamba amtafute mume ambaye angemthamini kama binadamu na wala siye ambaye angemmiliki kama chombo.

Kisa cha Mwanamuka nacho kinadhihirisha uvumilivu wa mwanamke. Mamake Mwanamuka alikuwa na mawazo yaliyokinzana na yale ya wanakijiji walioshikilia kwamba mtoto msichama hakustahili kuelimishwa. Hata mumewe alimwachia mzigo wa kuhangaika kumtafutia Mwanamuka karo. Vivyo hivyo, mawazo ya Nyakor yalitofautiana na ya mumewe kuhusu majukumu ya mke nyumbani. Mumewe aliamini kwamba mume ndiye alipaswa kuwa na usemi pale nyumbani lakini Nyakor anakataa jambo hili. Tofauti hizi za kimawazo zinafanya ndoa yao kuwa na misukosuko mingi lakini Nyakor anavumilia. Baada ya mumewe kuaga dunia, wazee walitaka kumlazimisha arithiwe lakini akakataa kabisa. Aidha, kupitia kwa hadithi ya Kamene, uvumilivu wa mwanamke unajitokeza. Kamene walipendana na Cedric ambaye alimalizia kumwoa lakini ndoa hiyo nayo ilijaa vituko vya mume. Kamene alipopata mimba alijifungua kupitia kwa njia ya upasuaji na kumsihi mumewe amtafutie kijakazi lakini akakataa. Kamene aliishia kufanya kazi zote za nyumba licha ya hali yake kuwa mbaya kiafya. Mwanamke wa Ziwa naye aliteswa na Nyalgondho licha ya kumpa mumewe utajiri mkubwa. Mumewe aliishia kuoa wake wengine na kuanza kunywa pombe huku akimpuuza. Alivumilia madhila hayo mpaka yalipozidi uvumilivu wake. Hatimaye, aliondoka na kurudi ziwani alikotoka pamoja na mifugo wote aliokuja nao. Kwa kuwa masimulizi haya yote yanatoka mawazoni mwa Kasekesi, yanatudhihirishia kwamba kwa kweli migogoro ya kimawazo ilimwezesha mwandishi wa riwaya hii kumkuza mhusika huyu kama mwenye stahamala.

### 3.3.3 Mwanamke ni Jasiri

Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*, mwanamke amekuzwa kama mtu jasiri. Kuna mambo mengi yanayohusu maonevu na tamaduni zinazomkandamiza lakini anatokea kukabiliana na changamoto mbalimbali na hata wakati mwingine hutokea anapolazimika kukabiliana na jamii nzima akiwa amesimama peke yake. Wakati mwingine mwanamke amelazimika kukabiliana na wanawake wenzake wanaomsaliti na hata wengine kumdhihaki. Hata hivyo mwanamke anakabiliana na changamoto hizi kwa ujasiri wa kupigiwa mfano. Kasekesi alipofiwa na mumewe Agusto, jamaa ya mumewe ilimgeuka na kumtesa sana kwa kisingizio kwamba ndiye aliyemuua Agusto. Walimvua nguo zote, kumpa mchanganyiko wa majani mbalimbali na kumlazimisha kulala katika chumba kimoja na maiti ya mumewe. Ujasiri wake ulijitokeza alipokabiliana na changamoto hizi zote na hatimaye hakufa kama jamaa hiyo ilivyotarajia.

Katika sehemu ya kwanza inabainika namna mwanamke anavyokabiliana na wale madaktari na wauguzi wa kiume wanaomdhihaki kwa sababu alikuwa mwanamke, hata hivyo anasimama kidete na kuwaonyesha kwamba yeye ni mwanamke na anaionea fahari jinsia yake licha ya maumivu makali aliyokuwa nayo. Mwanamuka alionyesha ujasiri pale alipoteswa na kuonyeshwa madharau na mumewe kiasi cha kumwoa kijakazi wao. Alipoona mambo yamezidi, alijinasua kutoka katika ndoa hiyo na kujiendeleza kimasomo. Hatimaye alikuwa mhariri mkuu katika shirika moja la uchapishaji wa vitabu. Nyakor pia alionyesha ujasiri kwa kupigania haki zake bila kumruhusu yeyote kumdhalilisha. Licha ya kwamba elimu ya mwanamke haikutiliwa maanani wakati huo aling’ang’ana na vikwazo vyote vilivyokuwa mbele yake na kuhakikisha kwamba alielimika hadi kiwango cha juu na kuwa mhandhisi. Ujasiri wa Nyakor ulimwezesha

kusimama kidete na kukataa unyanyasaji katika ndoa yake. Baadaye, mumewe aliaga dunia na wazee wa jamii yake wakasisitiza kwamba Nyakor lazima arithiwe kuambatana na mila za jamii hiyo. Nyakor kwa ujasiri alikataa na kusimama imara kiasi cha kutofuata utamaduni huo.

### 3.3.4 Mwanamke ni Mtiifu

Kupitia kwa kisa cha Kasekesi tunabaini kwamba mwanamke ni mtiifu. Kwa mujibu wa mashauri aliyoyapata Kasekesi kutoka kwa mama, inajitokeza kwamba kuna mengi ambayo yalimkera kuhusu utamaduni wao uliomdhalilisha mwanamke. Hata hivyo, alikuwa mtiifu kwa kufuata yale yote aliyohitajika kuyatimiza kulingana na utamaduni. Hii ndio maana aliweza kuishi na mumewe aliyekuwa mtamaduni ingawa mamake Kasekesi hakukubaliana na utamaduni huo. Kasekesi alitokea kuwa mtiifu baada ya kuolewa na Agusto. Aliikimu jamaa kubwa ya Agusto waliomtegemea kwa msaada wa vitu vingi. Baada ya Agusto kufa alitii masharti aliyopewa na wazee ya kunywa mikorogo ya namna fulani ili kuthibitisha kwamba hakuhusika katika kifo cha Agusto. Baba alipomshauri Kasekesi (uk. 43), alimhimiza anyeyekee mumewe na kumtii kama alivyoagiza mshairi Mwanakupona katika utenzi wake kwa mwanawe.

### 3.3.5 Mwanamke ni Mwenye Utu

Baada ya Kamene kuozwa kwa lazima, alitoroka na kumkimbilia mwalimu wake wa zamani Bi. Zipporah Mosha ambaye kwa utu wake alimfadhili kwendelea na masomo yake. Hatimaye, alifuzu na shahada ya kwanza na ya pili ya chuo kikuu na kuishia kuwa mwalimu wa chuo cha ualimu. Haya yote yalitokea kwa sababu ya utu wa mwalimu Mosha. Mbali na sifa hizi chanya za mwanamke zinazojitokeza katika sehemu hii ya

kwanza, kuna sifa hasi za mwanamke ambazo mwandishi amezitokeza kupitia kwa mtazamo wa kiume katika sehemu ya pili. Sifa hizi ni kama vile unafiki, ukatili, utovu wa shukrani, usaliti, uongo, miongoni mwa sifa nyinginezo. Mawazo ya mwanamume aliyelazwa hospitalini akiwa mahututi yanatudhihirishia sifa hizi za mwanamke kupitia kwa masimulizi ya watu mbalimbali.

### 3.3.6 Mwanamke ni Mnafiki

Msimulizi (Mumbo) anatuthibitishia sifa ya mwanamke kuwa mnafiki kupitia kwa Daphina – mke wa ami yake ambaye siku zote alikuwa mkali na hakuchelea kumgota kwa mwiko kila mara alipopika. Ukali wake uliyeyuka na kugeuka upendo kwa Mumbo pale Mumbo alipowapata wakifanya ngono na Kasu kichakani. Alipopika jioni alimpa Mumbo nyama za kukaanga na kujifanya mzuri kwake. Aidha, machoni pa kila mtu alijifanya mwadilifu na mwaminifu kwa mumewe lakini alimwendea kinyume kwa kufanya ngono na Kasu kichakani. Unafiki mwingine wa mwanamke ulijitokeza kwa mke wa Kaminda aliyemwingiza katika mtego wa ndoa bila yeye kufahamu. Sasi alijifanya kwamba alitaka tu msaada wa mahali pa kujisitiri baada ya kufungiwa nyumba kwa kukosa kodi. Baadaye, alijiingiza kabisa maishani mwa Kaminda na kumwacha na uchaguzi mmoja tu ambao uliku kumwoa. Alijifanya mcha Mungu na mke mwema kwa Kaminda hadi Kaminda alipomwoa ndipo alipata kujua hulka yake halisi.

Baadaye, Kaminda alitambua kwamba Sasi alikuwa na mtoto aliyempata nje ya ndoa na kumwachia babu na nyanyake asije akawa kikwazo katika ndoa yake. Baada ya Kaminda kugundua hila ya Sasi, maisha yao ya ndoa yalizorota kiasi cha Sasi kutaka kumuua kwa kisu. Kaminda aliponea na kuchomoka mbio. Alitoweka asionekane tena kwake. Lulu

naye alijifanya mke mwema kwa Sir Pipo wakati wa uchumba wao. Alionekana mnyeyekevu, mtiifu na mwenye kuenzi mumewe. Sir Pipo alipumbazwa na kumwendeleza Lulu kimasomo hadi alipopata shahada ya uzamili. Baada ya kuolewa, Lulu alibadilika na kuanza kumkaidi mumewe kwa kila kitu. Hata alijiunga na kundi la wanawake waliojifanya kutetea haki za wanawake. Katika kundi hilo, wote walikuwa wametalikiwa na waume zao ila Lulu tu. Baadaye, Lulu waliachana na mumewe Sir Pipo. Haya yote yanadhihirisha kwamba kweli mwanamke amekuzwa kama mhusika mnafiki.

### 3.3.7 Mwanamke ni Katili

Nyanyake Mumbo anamkaba koo na kumzaba makofi akidai kwamba alimchungulia wakati alipokuwa akienda haja, ingawa hilo halikuwa kweli. Mbali na hayo Sasi anajifanya kumpenda Kaminda ili amwoe lakini baada ya kuolewa na Kaminda anaanza kumwonyesha mumewe madharau. Alianza kumshuku kila mara alipochelewa kurudi nyumbani. Kaminda anapogundua siri ya mkewe kwamba alikuwa na binti aliyemwacha kwa nyanyake, anapanga kumwangamiza Kaminda kwa kisu. Kaminda anaponyoka tu kwa bahati nzuri na kutoweka asirudi tena.

Ukatili wa mwanamke unajitokeza pia pale wahudumu wa afya wanapomdhihaki mwanamume (Mumbo) aliyelazwa hospitalini akiwa mahututi badala ya kumhudumia na kumtibu wanamdhihaki na kumlazimisha ajitambulishe ingawa ilibainika kwamba hata hakuweza kuzungumza vizuri. Wanamkejeli kwamba ainuke kutoka kitandani iwapo ni mwanamume kweli. Anaposhindwa kuinuka wanaangua kicheko. Hata wanavyomzungumzia mwanamume huyo kunaonyesha kwamba wana chuki dhidi yake (uk. 128). Mamake Cedric Lusweti naye anaonyesha ukatili kwa kuzidisha mateso ya

mkaza mwanawe – Kamene. Mavyaa ndiye anayechangia pakubwa kuvunjika kwa ndoa kati ya Cedric na Kamene. Anamdekeza Cedric kama mtoto mdogo hata kumwoshea chupi, jambo ambalo Kamene hakulikubali hata kidogo. Cedric alipompiga Kamene na kumuumiza, mamake hakuingilia kati. Kila mara alimwona Kamene kama ndiye mwenye makosa na wa kuja kuingilia penzi lake kwa mwanawe.

### 3.3.8 Mwanake ni Msaliti

Usaliti wa mwanamke unajitokeza katika visa mbalimbali vinavyosimuliwa katika riwaya hii. Kuna visa vya wanawake kuwasaliti wanawake wenazo na wanawake kuwasaliti wanaume. Katika kisa cha Kasekesi baada ya mumewe kufa, kuna wanawake wanaojiunga na wanaume kumtesa badala ya kuwa mtetezi wake. Kasekesi anasema:

> Palikuwa na wanawake kadha huko mbali waliokuwa wakinisubu kwa mafumbo. Wanawake kama mimi wanaoshikilia kwamba lazima nipambane na hali kama hii? Ulimwengu umebiruka biru! (uk. 52)

Vivyo hivyo, shangazi yake Kasekesi (Selina) hamtetei na kumhifadhi. Badala yake anafurahia vijana wanapokuja kumfurusha kwa kisingizio kwamba angefanya kijiji chao kuchomwa kwa kuasi ukoo. Mwanamuka naye anasalitiwa na mke mwenzake ambaye alimwajiri kama kijakazi wake. Siku zote Mwanamuka alimhifadhi na hata kufadhili safari zake za kwenda kutembelea wazazi wake mara kwa mara kumbe safari zile zilimhusisha mumewe Mwanamuka pia. Kila mara alimnyemelea kijakazi wao. Kijakazi huyu anaishia kuwa mke mwenza wa Mwanamuka na kuchangia ndoa yake kusambaratika.

Wake wenza wa Mwanamke wa Ziwa pia wanamsaliti mwanamke mwenzao kwa kukubali kuolewa na Nyalgondho ingawa walijua kwamba Nyalgondho alikuwa na mke.

Kuwepo kwao pia kunachangia kusambaratika kwa ndoa ya Mwanamke wa Ziwa na Nyalgondho kwani uwepo wao ulimpa Nyalgondho kiburi cha kuanza kumwona Mwanamke wa Ziwa kama asiye na umuhimu wowote. Mbali na hayo, kuna wanawake wanaowasaliti waume zao. Mumbo anasalitiwa na mkewe. Baada ya kupoteza kazi yake mkewe anamdharau na mambo yanapokuwa magumu zaidi anawatwaa watoto na kutoroka nao akimwacha mumewe na mawazo mengi. Mumbo pia anahadithia namna alivyoamkuta mkewe ami yake Bi. Daphnia akila uroda na Kasu msituni. Aidha, anaeleza namna mkewe mzee wa kanisa na pasta walivyotoroka kanisani mkesha wa mwaka mpya na kwenda kula uroda kwenye mikonge wakati watu walipokuwa wakiabudu kanisani. Kaminda naye anasalitiwa na mkewe kwa kumdanganya kwamba alikuwa msichana asiye na mtoto. Baada ya kuingia katika ndoa ndipo kaminda anagundua kwamba alichezewa shere. Alidanganywa akafunga harusi na msichana aliyekuwa na binti mkubwa ambaye aliwaachia nyanya na babu yake awatunze. Jambo hili ndilo linakuwa chanzo cha ndoa yao kuvunjika.

Sir Pipo naye alimpenda mkewe Lulu kwa dhati. Hata kabla ya ndoa, anahakikisha kwamba anamwelimisha hadi anapata shahada ya uzamili. Hata hivyo, Lulu anamsaliti Sir Pipo kwa kuungana na jamaa zake na kumpunja mali kupitia kwa mahari. Sir pipo anapojizatiti na kulipa kiasi kikubwa cha mahari, wanaishi na Lulu kwa muda mfupi tu kabla ya migongano kuingia

katika ndoa yao. Hatimaye, Lulu anakosa kumtii mumewe. Alitaka chochote asemacho ndicho kitumike katika nyumba yao. Hatimaye ndoa hiyo inasambaratika.

Purupesa pia anadaganywa na mkewe kwamba alikuwa akihudhuria mkutano wao wa wanawake kumbe alikuwa akienda katika klabu ya *Avocadowasp* hapo jijini alipokuwa akisakata densi uchi. Hayo yote yanathibitisha kwamba mwanamke si msaliti tu wa mwanamume bali pia husaliti mwanamke mwanzake mradi tu anufaike yeye binafsi jambo ambalo pia linathibitisha kwamba mwanamke ni mwenye ubinafsi

### 3.3.9 Mwanamke ni Mwongo

Sifa ya mwanamke kuwa mwongo imedhihirishwa kupitia kwa wahusika mbalimbali. Katika hadithi ya Kaminda Mwana-a Pasta, Sasi mkewe, anahamia kwake kwa njia ya udanganyifu kabla hata hawajaoana. Sasi alimdanganya Kaminda kwamba alikuwa amepewa ilani ya kuhama kwa kuwa alishindwa kulipa kodi ambayo ilikuwa imeongezwa. Kwa hivyo, Sasi anatumia uongo kupata makao katika nyumba ya Kaminda. Vilevile, baada ya Sasi na kaminda kuoana kirasmi, Kaminda anakuja kugundua kwamba alidanganywa na Sasi kwamba alikuwa msichana asiye na mtoto ilhali alikuwa na binti mkubwa ambaye alimwacha kwa babu na nyanya yake. Hili ndilo jambo linalosambaratisha ndoa yao.

Truvessa naye alimdanganya Purupesa kwamba kila mara alipoondoka nyumbani alikuwa akienda katika chama cha wanawake kumbe alikuwa akienda kuwaburudisha walevi katika klabu ya *Avocado Wasp* kwa kucheza muziki akiwa uchi. Uongo huu unavunja ndoa yao na kumwacha Purupesa akisononeka kwa ugonjwa usioisha na hatimaye kufa.

### 3.3.10 Mwanamume

Mhusika wa pili katika riwaya hii ni Mwanamume. Hulka yake imesawiriwa vizuri katika sehemu ya pili ya riwaya hii. Sehemu ya pili ya riwaya hii inatangulizwa kwa kutupa

taswira ya mwanamume aliyelazwa hospitalini akiwa mahututi. Anakejeliwa na wahudumu wa kike wanaomshinikiza ataje jina lake. Mwanamume huyo kwa jina Mumbo anakataa kutaja jina lake na kuwasisitizia kwamba yeye anaitwa Mwanamume. Jambo hili linawakera na wanatishia kuachana naye kabisa wasimhudumie. Wanawake hao wanachukulia jibu lake kuwa jibu la kiburi. Kupitia kwa mawazo ya mhusika huyu, tunapata sifa mbalimbali za Mwanamume. Visa mbalimbali anavyosimulia akilini mwake vinadhihirisha sifa mbalimbali za Mwanamume. Katika sehemu hii sifa nyingi za mwanamume ni chanya  na zimetolewa kwa mtazamo wa kiume.

### 3.3.11 Mwanamume ni Mvumilivu

Uvumilivu wa Mwanamume unajitokeza katika hadithi ya Kaminda Mwana-a-Pasta. Sasi anapomjia na ombi la kuhifadhiwa akitafuta mahali pa kwenda, Kaminda anakubali kwa kuwa alikuwa amefundishwa kanisani kwamba binadamu anastahili kumsaidia mwenzake. Hata hivyo, ufadhili huo unazidi pale Sasi anapoendelea tu kuishi bila kuonyesha dalili zozote za kuondoka. Kaminda anaamua kumvumilia tu na kufa kikondoo bila kulalamika. Mambo yanaharibika Kaminda anapomwoa Sasi na tabia zake kuwa mbaya. Baada ya harusi yao Sasi alianza kumshukushuku Kaminda kila mara alipofika nyumbani akiwa amechelewa. Kadri wanavyozidi kuishi ndipo uhusiano wao unazidi kuzorota. Ikafika wakati ambapo hawakusemezana. Mwandishi naye anatusisitizia uvumilivu wa mwanamume anaposema:

> Kaminda Mwana-a Pasta ni mndani, anayemeza mrututu wake polepole kama mtu anayemeza utomvu wa msubili kuyatibu maradhi ya tumbo. Anayekereka kisha akaumeza uchungu wake ndani kwa ndani (uk. 153)

Mbali na Kaminda Sir Pipo naye anapendana na Lulu ambaye anajifanya anampenda kumbe alinyeyekea tu apate kuelimishwa. Baada ya Sir Pipo kujitolea kumwelimisha hadi chuo kikuu na kumwoa, anadhihirisha tabia zake halisi. Mara nyingi, alibishana na mumewe huku akimwonyesha dharau moja baada ya lingine. Ndoa yao inavurugika zaidi wakati Lulu anapojiunga na kundi la marafiki zake waliloliita chama. Maisha ya Lulu yalichukuliwa na kundi lenyewe akampuuza na kumdharau mumewe kabisa. Sir Pipo alivumilia haya yote kwa muda mrefu mpaka hatimaye wanakuja kuachana na Lulu.

Kisa cha Kasina Usina Sini pia kinathibitisha uvumilivu wa wanaume. Kasina Usina Sini anapomshuku mkewe kutokuwa mwaminifu katika ndoa na kutaka kumfukuza, babake anamkataza na badala yake anaandaa sherehe na kuwaita wanawake wote akiwemo mamake Kasina. Beberu anachinjwa kisha utumbo unapikwa vizuri. Mzee Usina anatangaza kwamba utumbo huo uliwe tu na wanawake ambao hawajawahi kwenda nje ya ndoa yao kwa sababu utumbo huo uliandaliwa na dawa maalum. Hakuna hata mwanamke mmoja aliyegusa utumbo huo. Hili lilikuwa funzo kwa Kasina kwamba wanaume wote wanaishi na wanawake kwa kuwavumilia.

### 3.3.12 Mwnamume ni Mwenye Bidii

Masimulizi ya Mumbo yanadhihirisha kwamba Mwanamume ni mtu mwenye bidii. Kisa cha Wamae kinatupa taswira halisi ya bidii. Wamae alikuwa kijana aliyetoka katika jamii maskini aliyekuwa na funza miguuni. Masomo yake yanasitishwa kwa kukosa karo anapotafuta misaada kutoka kwa watu mbalimbali akiwemo mbunge wao na kuukosa mpaka anaposaidiwa na madaktari wa kigeni. Anatolewa funza miguuni na madatari wa *“M’edicens san Frontieres.”* Wamae anaamua kuanzisha biashara ya kuuza mboga mjini.

Anatia bidii na baadaye kuanzisha biashara ya viazi, vitunguu na kabeji kwa bei ya jumla. Hatimaye, Wamae anafanikiwa na kuwa tajiri aliyeagiza mali ya thamani kubwa kutoka Dubai. Hili linathibitisha kwamba Mwanamume ni mwenye bidii. Mbali na sifa hizi zinazojitokeza katika mtazamo wa kiume, tunapata sifa zingine ambazo zinawasilishwa kupitia kwa mtazamo wa kike ambazo ni hasi. Kwa mujibu wa mtazamo wa kike:

**3.3.13 Mwanamume ni Katili**

Ukatili wa Mwanamume unajitokeza katika kisa cha Zahra ambaye alinajisiwa na mwalimu wake wa dini. Babu yake anapotafuta haki kutoka kwa chifu, hakuna hatua yoyote inayochukuliwa kwani aliyemtendea Zahra unyama ule alikuwa na uhusiano na kigogo mmoja pale kijijini na chifu aliogopa kuchukua hatua asimwage unga wakati alikuwa karibu kustaafu. Aidha tunaelezwa kwamba mamake Zahra alijifungua kizuizini kwa sababu alikamatwa kwa kuwa nduguye mdogo alishukiwa kuwa gaidi. Aidha, katika hadithi ya Kamene, mumewe anaonyesha ukatili kwa kumtesa moja kwa moja kisaikolojia kwa njia ya matusi. Kamene anapojifungua kupitia kwa njia ya upasuaji mumewe anakataa kumtafutia kijakazi na kumpuuza pamoja na mtoto wao. Badala yake anaondoka na kurudi nyumbamni akiwa amelewa na kumnyamazia mkewe. Hali hii inafikia kiwango cha Lusweti kumwonea wivu mwanawe kwa kuchukua muda mwingi wa mkewe Kamene na hivyo basi akamchukia mtoto wao pia. Hatimaye ndoa hii inapovunjika, Lusweti anakataa kutoa pesa za kumtunza mtoto wao. Kamene anapomchukulia hatua kisheria, Lusweti anapanga njama na Kamene anashambuliwa na watu asiowajua na kupoteza ufahamu. Kasekesi naye anateswa sana na wazee wa jamii ya mumewe kwa kisingizio kwamba ndiye aliyemuua Getonga. Wazee wanamlazimisha Kasekesi kulala katika chumba kimoja kidogo sana na maiti. Walimpaka matope na

kuzirarua nguo zake huku wakimzungusha kwenye soko la karibu akiwa nusu uchi na kumzomea.

### 3.3.14 Mwanamume ni Msaliti

Mwanamume anajitokeza kama msaliti kwa kumwendea kinyume mwenzake. Katika hadithi ya Mumbo, anatusimuliwa namna Mwanamume mmoja kwa jina Kasu alivyomnyemelea mke wa ami yake – Bi. Daphina na kufanya naye ngono msituni. Mbali na hayo katika hadithi iyo hiyo, Mumbo anaelezea namna pasta (babake Kaminda) alivyomsaliti mzee wa kanisa lake kwa kumnyemelea mkewe. Ulikuwa usiku wa mkesha wa kuamkia mwaka mpya ambapo kila mtu aliendа kanisani kuukaribisha mwaka mpya. Wakati kila mtu alipokuwa akiomba kwa sauti, pasta na mke wa mzee wa kanisa wanatoweka. Mumbo alipowanyemelea aliwakuta wakila uroda kwenye mikonge. Huu ulikuwa usaliti uliojitokeza kati ya mume na mume.

Kuna usaliti pia ambapo mwanamume anamsaliti mwanamke hasa katika sehemu ya kwanza ya riwaya. Katika hadithi ya Mwanamuka, mumewe anamsaliti kwa kumtunga mimba kijakazi wao na hatimaye kumwoa. Mume wa Mwanamuka anamsaliti kwa kuoa kijakazi wao kwa sababu Mwanamuka hakuwa na uwezo wa kuzaa na hicho ndicho kinakuwa chanzo cha ndoa yao kuingia doa. Hatimaye ndoa hii inavunjika. Kamene naye anasalitiwa na mumewe Cedric Lusweti. Cedric anabadilika na kuanza kumpuuza punde tu baada ya wao kuoana. Anaanza kumtesa Kamene na kumchukia. Chuki hiyo inakuwa mbaya zaidi mamake Cedric anapoingilia ndoa yao na kumthibiti Cedric kwa kila kitu na kumweleza namna alivyotaka waishi na mkewe.

Mamake Kamene pia alisalitiwa na mumewe kwa kumpuuza na kumchukia Kamene punde tu alipozaliwa. Hata hakupendekeza jina kama utamaduni ulivyomhitaji. Hii ni kwa sababu babake alitarajia mtoto mvulana lakini Kamene anapotokea kuwa wa kike babake anamkana kuanzia kuzaliwa kwake. Aidha, Nyalgondho anamsaliti Mwanamke wa Ziwa kwa kumpuuza baada ya kumwoa. Nyalgondho alikuwa maskini na alipotajirishwa na Mwanamke wa Ziwa kwa kumpa mifugo wengi anakuja kugeuka na kumdharau hata kuongeza wanawake wengine. Alianza kulewa sana na kumtesa Mwanamke wa Ziwa ambaye baada ya kuchoka naye, anachukua mifugo wake na kurudi nao ziwani alikotoka.

### 3.3.15 Mwanamume ni Mnafiki

Unafiki wa Mwanamume unajitokeza katika kisa cha Mumbo anaposimulia namna Pasta aliyechukuliwa kuwa kielelezo cha maadili katika jamii anapotokea kuwa ndiye anayemnyemelea mke wa mzee wa kanisa na kula naye uroda kwenye mikonge wakati wa usiku. Mbele ya watu na waumini wake, mhubiri alijifanya mcha Mungu na hata kuwaelekeza watu kuhusu uadilifu ilhali yeye anapatikana na mke wa mtu wakila uroda. Jambo hili linaonyesha unafiki wa Mwanamume hasa aliyeachiwa jukumu la kuielekeza jamii katika masuala ya kidini. Unafiki wa Mwanamume pia unadhihirika katika kisa cha Cedric na Kamene. Baada ya ndoa ya kwanza ya Kamene kuvunjika alichukua tahadhari asijiingize katika ndoa ambayo ingempa uchungu tena. Hakuwaamini tena wanaume. Hata hivyo, Cedric anampumbaza na kujifanya mwema. Kila mara alimchekesha na kumwonyesha mapenzi moto moto. Hata hivyo, Cedric anabadilika baada ya kuoana na kuwa mume asiyejali. Anatokea kuwa mbinafsi, mwenye chuki na asiye na utu kiasi cha kutomjali mkewe hata baada ya kujifungua kwa upasuaji. Nyalgondho naye

anampumbaza Mwanamke wa Ziwa kwamba alikuwa mume aliyewajibika na kujifanya mtu mpole na mwema. Baadaye anajitokeza kuwa mpuuzi na mlevi kupindukia. Anaonyesha tamaa iliyokithiri na kuoa wanawake wengine na kuanza kumdharau Mwanamke wa Ziwa. Haya yanadhihirishwa na msimulizi anaposema;

> Nyalgondho mtoto wa kimaskini,
> Ambaye hakuota akilini,
> Kuwa atatoka ufukarani,
> Au awe na mke nyumbani,
> Sasa akakosa shukrani,
> Asiye mtu, hayawani (uk. 67).

### 3.3.16 Mwanamume ni Mwenye Tamaa

Sifa nyingine ya Mwanamume inayodhihirika katika visa hivi ni kwamba mwanamume ni mhusika mwenye tamaa. Tamaa yake inadhihirika kupitia kwa hadithi mbalimbali kama vile kisa cha Kasina, kisa cha Nyalgondho, kisa cha Nyakor, kisa cha Mumbo miongoni mwa vingine. Katika kisa cha Kasina tunamwona Mwanamume kama mtu asiyeridhika na alicho nacho. Hii ndiyo sababu Mwanamume anawaoa wake wengi. Msimulizi anatueleza:

> Kasina Usina Sini alitokana na ukoo uliopenda kuoa wanawake wengi sana. Hakuna hata mwanamume mmoja ambaye aliridhika na mke mmoja tu (uk. 217)

Tunaelezwa kwamba babu yake Kasina alikuwa na wake watano. Babake Usina naye alikuwa na wake watatu na Kasina mwenyewe alioa wake wawili na kuwa na mahawara wengi nje ya ndoa. Tamaa yake inakuja kumponza wakati watoto aliowazaa nje wanapomjia kwake na kutaka kutambuliwa kama watoto wake. Aidha katika kisa cha Sir Pipo, wazee waliojadiliana na Sir Pipo kuhusu mahari ya kulipiwa Lulu wanaonyesha tamaa iliyokithiri mpaka. Wanamtaka Sir Pipo kutoa blankenti jipya la sufi, shuka tatu, kibuyu cha asali ya msitu, ng’ombe sita, fahali wawili na shilingi laki moja u nusu. Hii

ilikuwa tamaa kubwa ikikumbukwa kwamba ni Sir Pipo ndiye aliyegharamia masomo ya Lulu hata akapata shahada. Kisa cha Nyalgondho nacho kinaonyesha tamaa ya Mwanamume kwani naye anaoa wanawake wengine baada ya kutajirishwa na Mwanamke wa Ziwa. Visa hivi vyote vinaonyesha kwamba kweli Mwanamume ni mhusika mwenye tamaa.

### 3.3.17 Hitimisho

Kwa kuzingatia yote yaliyoangaziwa katika sura hii, imebainika kwamba ni migogoro ya kimawazo ndiyo iliyowawezesha waandishi wa riwaya hizi mbili yaani, *Mkamandume* (2013) Said A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2012) Wamiltila K. kuwakuza wahusika wao vyema zaidi. Kupitia kwa migogoro hiyo ya mawazo, ndipo waandishi wa riwaya hizi waliweza kutimiza malengo yao na kupitisha ujumbe waliokusudia kuwapa wasomaji wao. Kupitia kwa ukuzaji mwema wa wahusika ndipo hata ujumbe wao uliwasilishwa kwa njia inayoeleweka. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba migogoro ya kisaikolojia ni sehemu muhimu ambayo haiwezi kupuuzwa katika riwaya ya Kiswahili. Sura inayofuata (ya nne) ilishughulikia namna migogoro ya mawazo ilivyowawezesha waandishi wa riwaya teule kukuza ploti zao kwa nmna inayovutia.

# SURA YA NNE

# MIGOGORO YA KIMAWAZO NA PLOTI KATIKA RIWAYA ZA *MKAMANDUME* NA *UNAITWA NANI?*

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imelenga kulijibu swali la tatu la utafiti ambalo liliuliza: migogoro ya kisaikolojia inakuzaje riwaya kimsuko na kuifanya kuwa na mshikamano mwema katika ploti yake? Kwa mujibu wa Wamitila (2003), ploti ni matukio yanayojenga hadithi. Dibell (1988) anasema kwamba ploti ni ujenzi wa matukio muhimu katika hadithi. Anafafanua kwamba mpangilio wa matukio katika hadithi lazima uwe na umuhimu wa kuendeleza hadithi ndipo yarejelewe kama ploti. Anatoa mfano kwa kusema kwamba, kusuka nywele au kufungua mlango ni matukio ya kawaida ambayo hayawezi kurejelewa kama ploti. Hata hivyo, matukio haya yanapopangwa kwa namna fulani inayoathiri matukio mengine katika hadithi kiasi cha kuweza kuzua taharuki itakayoamsha hamu ya msomaji kutaka kujua matukio mengine ya baadaye, basi mshikamano huo wa matukio utarejelewa kama ploti.

Robert Di Yanni (2004) naye anasema kwamba ploti na muundo wa hadithi hutegemezwa kwenye matukio mbalimbali katika hadithi yenyewe. Kila ploti ya hadithi hutuwezesha kufungua kurasa za hadithi tukitaka kufahamu yaliyojiri baadaye. Anasema kwamba ploti nyingi za kazi za fasihi huegemezwa kwenye migogoro au mivutano kati ya makundi mawili pinzani na migogoro yenyewe inapotatuliwa, hadithi hufikia mwisho.

Brook (1992) kwa upande wake anasema kwamba ploti ni mshikamano wa matukio katika hadithi ambao utaiwezesha hadhira kubaini kaida za ki-Aristotle zinazosisitiza mwanzo mwema, katikati na mwisho wa hadithi. Utafiti huu ulitumia neno ploti kwa

maana ya mpangilio wa matukio kimaksudi katika hadithi unaofanywa na mwandishi ili kuleta mtiririko wa mawazo yanayoweza kubainisha dhamira yake. Aidha, sura hii iliegemezwa kwenye mhimili wa tatu wa nadharia ya upembuzi unaosisitiza vipengele vitatu. Vipengele hivi ni:

i. Muungano wa mikinzano – katika kila mgogoro kuna migogoro mingine midogo midogo ambayo lazima iungane ili kufanikisha mgogoro mkuu.
ii. Ukamilifu wa mikinzano – migogoro mbalimbali hutegemeana na kukamilishana kiasi cha kuwa na mtagusano na mwingiliano wa vipengele mbalimbali vya migogoro hiyo ili migogoro yenyewe iweze kusimama. Kila mgogoro mdogo unakuwa sehemu inayokamilisha mgogoro mkuu.
iii. Mabadiliko ya migogoro – kwa kuwa kuna mabadiliko ya mara kwa mara kwenye migogoro, migogoro mipya hutokea kila mara hata baada ya migogoro ya awali kusuluhishwa.

Ili kuweza kuchanganua migogoro ya kimawazo katika riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?* ilikuwa vigumu kuepuka vipengele hivi ambavyo vilikuwa muhimu katika uchanganuzi huu. Brook (1992) anasema kwamba muundo wa hadithi hutegemea taharuki kwani ndiyo humwezesha mwandishi kuweka wazi matukio yake hatua kwa hatua huku akibana baadhi ya matukio makusudi na hatimaye kuonyesha namna migogoro yake inavyotatuliwa mwishowe. Sura hii iliegemea zaidi vipengele vitatu vya mhimili wa tatu wa nadharia ya upembuzi na kubainisha namna vipengele vyenyewe vilichangia kukuza ploti za riwaya hizi mbili.

## 4.1 Migogoro ya Kimawazo na Ploti Katika Riwaya ya *Mkamandume*.

Sehemu hii imeshughulikia namna migogoro ya mawazo ilivyomwezesha mwandishi wa riwaya ya *Mkamandume* kukuza ploti yake kwa njia ya kuvutia.

### 4.1.2 Muungano wa Mikinzano

Kipengele cha muungano wa mikinzano kinasisitiza kwamba katika kila mgogoro huwepo migogoro mingine midogo midogo inayoungana ili kukamilisha mgogoro mkuu, mwandishi wa riwaya hii ameitumia nafasi hii vyema kukuza ploti yake. Mgogoro mkuu unaobainika katika riwaya hii ni ule wa kitabaka ambao umekamilika tu kwa sababu ya kuwepo kwa migogoro ya kimawazo miongoni mwa wahusika mbalimbali. Kupitia kwa migogoro ya kimawazo ya wahusika mbalimbali, tunaweza kubaini kuwepo kwa mgogoro wa kitabaka na chanzo chake. Mwanzoni kabisa mwa riwaya (uk. 2) tunapata mgogoro wa kwanza wa kimawazo wa Mkamandume anapojisaili kuhusu asili yake. Nafsi yake inamkanya dhidi ya kujichunguza asili lakini kuna sehemu ya nafsi hiyo hiyo inayomhimiza kujichunguza na kutokana na mgogoro huu, inabainika kwamba kulikuwa na watu mbalimbali katika Malelejimema wenye asili mbalimbali ambao hata matabaka yao yalitofautiana. Mkamandume anashangaa ni kitu gani kinatofautisha wanaojiita wenyeji kindakindaki wa Malelejimema na wale wanaoitwa wageni. Mawazo ya Mkamandume yanamwelekeza kwamba tarihi ya Malelejimema inasheheni maslahi ya upande mmoja, hasa ule upande wenye nguvu.

Mgogoro huu umejitokeza mapema kimakusudi ili kuvuta umakinifu wa watu na hamu yetu ya kutaka kujua mambo matatu: asili ya Mkamandume na Malelejimema, asili ya mgogoro huu wa kitabaka na namna mgogoro wenyewe utakavyosuluhishwa. Mawazo ya Mkamandume yanatuelekeza kuelewa kwa nini Mkamandume ameshindwa kuikimu

familia yake. Jambo hili linaelekea kuwaathiri mke na watoto wake ambao pia migogoro yao ya kimawazo inachangia kujenga mgogoro mkuu. Tufaa anapigana na dhamiri yake na kujiuliza kwa nini anamchukia mwanawe ki-Katija. Anashangaa ikiwa kweli anamchukia mwanawe aliyemzaa. Mawazo haya kinzani yanatokea kuyajaliza yale ya Mkamandume ya mwanzo kuhusu kukosa kukimu familia yake na kuishia kumpendelea mwanawe mmoja tu, ki-Katija na kuwapuuza wengine wote waliosalia katika familia hiyo. (uk. 15)

Aidha, mgogoro ule ule wa mwanzo katika mawazo ya Mkamandume, unakuja kubainisha athari zake kupitia kwa mawazo ya mwanawe, Time. Time anawazia athari za kuwepo kwa uhasama miongoni mwa Wamalelejimema. Haya yanajitokeza baada ya Mzee Mkasi kumweleza kwamba aliogopa damu kwa kuwa alikuwa ameona nyingi ikimwagika. Mawazo kinzani yanamtatiza Time ni upande upi Mzee Mkasi angestahili kusimama wakati wa vita vya uhuru. Haya yote bado yanaendeleza tu ule mgogoro wa kitabaka uliobainishwa mawazoni mwa Mkamandume.

Kuna wahusika wengine ambao pia migogoro yao ya mawazo inachangia na kukamilisha ploti na vilevile kuendeleza  mgogoro mkuu. Baadhi ya wahusika hawa ni Soud, Bwan Sleyyum, Mzee Mkasi, Nadia miongoni mwa wengine. Mawazo ya Soud yanakinzana na yale ya wazazi wake kuhusu utabaka. Haya yanadhihirishwa na mgogoro wa kisaikolojia unaojitokeza mawazoni mwa Soud kuhusu Mungu na mafundisho ya kidini. Wazazi wa Soud hasa mamake anamweleza kwamba Mungu ndiye aliwaumba binadamu na kuwafanya wengine maskini na wengine matajiri. Hivyo basi, kila mja anastahili kuridhika na nafasi yake maishani aliyopewa  na Mungu. Soud naye anawaza kwamba

Mungu mwenye uwezo na mhimiza haki hawezi kuwa na mkono wa ubaguzi kama anavyosisitiza mamake. Kupitia kwa mawazo haya, tunamwona Soud akitatizika na kujiuliza ni kwa nini maisha yawe nusura kwa binadamu fulani na angamizo kwa mwingine (uk. 223)

Mgogoro mwingine wa kisaikolojia katika mawazo ya Soud ni ule unaodhihirisha utabaka. Unyanyasaji wa viongozi umewafilisisha wananchi kiasi cha kutoweza kujimudu kimaisha au hata kugharamia mahitaji yao ya kila siku kama chakula. Mgogoro huu wa mawazo unatilia nguvu zaidi ule wa kitabaka ambao ulijibainisha mwanzoni mwa riwaya (uk. 127-128)

Migogoro ya mawazo ya Mzee Mkasi nayo inakuza ploti kwani kupitia kwayo tunapata kufahamu yaliyowahi kutokea miongoni mwa Wamalelejimema. Mawazoni alijiuliza kama kulikuwa na uadui au la baada ya wale walioitwa wageni kufukuzwa. Kwa mujibu wa Mzee Mkasi, chuki imezidi. Anafikiri kwamba mmea wa chuki umezidi kunawiri na inaonekana kwamba utadumu milele. Jambo hili linaendeleza mzozo wa kitabaka ulioanzishwa na wakoloni. Wenyeji walidhani kwamba kuwafukuza wageni kungeleta usawa na kumaliza utabaka miongoni mwao. Hata hivyo jambo hilo linatokea kuwa baya zaidi kwani baada ya wageni kuondoka ndipo pengo lililokuwa kati ya maskini na wenye mali lilizidi kupanuka zaidi (uk. 180)

### 4.1.3 Ukamilifu wa Mikinzano

Kipengele cha ukamilifu wa mikinzano katika nadharia ya Upembuzi kinasisitiza kwamba migogoro mbalimbali hutegemeana na kukamilishana na kila mgogoro mdogo unakuwa sehemu inayokamilisha mgogoro mkuu. Ni wazi kwamba ploti husheheni

mambo mengi ili iweze kukamilika. Kwa mujibu wa Brook (1992), ili mwandishi aweze kuafikia dhamira yake lazima afinyange kazi yake vizuri ili kazi hiyo iwe kamilifu. Kwa sababu hii, mwandishi analazimika kufinyanga fani na maudhui kwa ufundi ili kazi yenyewe ikamilike. Katika riwaya ya *Mkamandume*, mwandishi amedhihirisha namna migogoro ya kisaikolojia inavyojitokeza miongoni mwa wahusika mbalimbali na jinsi ilivyoibua maudhui tofauti tofauti ambayo ndiyo ameyatumia kuendeleza ploti yake.

Katika riwaya hii, mwandishi ametanguliza masimulizi yake kwa migogoro ya kimawazo ya Mkamandume ambayo ndiyo iliyotuelekeza kwenye maudhui ya utabaka. Maudhui haya ndiyo yanayoendelezwa na kuzaa mengine kama vile ya kisasi, mapenzi, usaliti, dhuluma dhidi ya raia miongoni mwa mengine. Mgogoro huo wa mwanzo ndio unaoendelezwa na mwandishi na kutuonyesha kwamba utabaka huo ndio uliozaa ulafi wa matajiri na kuharibu mazingira kiasi kwamba maskini wasingemudu hata kujipa chakula chao cha kila siku. Haya yanakamilishwa na mgogoro mwingine wa mawazo unaotokea akilini mwa Mkamandume anaposhangaa kwa nini watu hawathaminiani tena. Kila mmoja amekuwa adui wa mwenzake. Kwa kuwa mashamba hayatoi mazao tena, Mkamandume anaamua kufyeka kila kitu kutoka kwa shamba lake (uk. 23). Baadaye mgogoro mwingine unakuja kutokea mawazoni mwake anapojilaumu kwa nini aliyatenda hayo.

Aidha, migogoro ya kimawazo inayojitokeza akilini mwa Soud inaendeleza na kukamilisha mgogoro wa mwanzo wa utabaka. Mawazo ya Soud yanaangazia uhasama ulioletwa na utabaka huu kiasi cha kwamba ndoa kati ya matabaka haya mawili iliharamishwa na wazazi katika pande zote. Jambo hili linamwathiri kwani alitokea

kumpenda Time ambaye alikuwa wa tabaka la chini huku wazazi wa Soud wakiwa wa tabaka la juu. Mawazo yenyewe yanadhihirika anapowaza:

> Lakini tamko hilo linasaidia nini sasa? Lina maana gani ya ndani zaidi ya kuashiria lile tatizo la kuchanganya damu? Labda Time anajaribu kumkumbusha yeye Soud asikate tamaa na kwamba kule kukataliwa kwake alipokwenda kuposa Time kwa sababu ya kuchanganya damu kwake kusimpe arudi nyuma (uk. 67).

Mgogoro mwingine wa mawazo unaotumiwa kukamilisha ule wa kitabaka ni ule unaojitokeza mawazoni mwa Soud. Ingawa mgogoro huu unahusu mapenzi ya Soud kwa Time, unachangia kuendeleza ploti kwani unajitokeza kuendeleza ule uhasama uliopo baini ya matabaka haya mawili. Soud anawazia iwapo akubali kuendeleza penzi lake kwa Time hata baada ya Mkamandume kukataa au la. Suala hili linaonyesha namna tabaka linalozungumziwa linaathiri hata mapenzi miongoni mwa watoto ambao wakati mwingine hawalithanini sana.

Iyo hiyo migogoro ya kimawazo ndiyo inayoendeleza maudhui ya mapenzi kati ya Soud na Time na kuendeleza ploti kwa kuzua taharuki kwani kwa upande mwingine tunamwona Nadia pia ambaye anampenda Soud ingawa anashindwa kumweleza moja kwa moja. Mawazo haya ndiyo anatumia mwandishi kuzua hamu yetu ya kutaka kujua yatakayotokea mwishoni. Je, kati ya mabinti hawa wawili ni yupi atakayetokea kupendwa na Soud zaidi ya mwingine? Wazo lili hili ndilo linalompa Nadia umuhimu katika ujenzi wa ploti ya riwaya hii kwani kupitia kwa mikinzano ya mawazo yake tunapata kufahamu mapenzi yake kwa Soud. Nadia anatokea kuwa muhimu kwa kuwa mbali na kujitokeza kuwa mpinzani wa Time, baadaye mwandishi anamtumia kuendeleza harakati za kupigania haki za wanyonge na kupinga dhuluma walizofanyiwa wanyonge

kwa sababu za kitabaka. Mbali na hayo kuna mgogoro wa kimawazo unaompitia Nadia akilini ambao ameutumia kuendeleza maudhui hayo ya mapenzi anapowaza:

> Tazama kwa mfano anavoyng'angania kwamba hana matamanio ya kiume kwake yeye Nadia. Ana kasoro gani Nadia kwani? … hajuti kumfuata hapa Malelejimema. Aaa, anasema nini Nadia? Kumfuata Soud au kuifuata Malelejimema yenyewe? (uk. 122)

Mgogoro huu wa kimawazo ni muhimu kwa ploti hii kwani ndio unaotudokezea sababu ya kuja kwa Nadia Malelejimema ambayo ilikuwa ni kutafuta mapenzi kutoka kwa Soud na vilevile kutafuta haki dhidi ya mauaji ya nyanyake wakati wa vita vya uhuru. Aidha, ni baada ya mawazo haya ndiyo yanampa mwandishi nafasi ya kutumia kisengerenyuma kukamilisha ploti yake. Hiki kisengerenyuma ni sura nzima inayotueleza namna Soud na Nadia walivyopatana kule London.

Mgogoro mawazoni mwa Time pia unatekeleza jukumu muhimu la kukuza ploti. Time anashangaa kwa nini Mzee Mkasi aogope damu kwa sababu ameona nyingi ikimwangika. Anawaza:

> Kama hiyo ni kanuni ya ujumla, mbona wengine kama yeye walioina damu ikimwagika nyingi wanataka kuiona bado ikiendelea kumwagika? Na hata wako tayari kushiriki kuimwaga zaidi na zaidi? (uk. 167)

Mgogoro huu umemwezesha mwandishi kutekeleza mambo mawili kwa wakati mmoja. Kwanza, umemwezesha kuzua maudhui ya ukandamizaji wa mwanamke kwa kisingizio cha utamaduni. Mawazo haya yanadhihirika baada ya Mzee Mkasi kumruhusu Time kumchinja kuku. Hili ni jambo ambalo lilienda kinyume cha utamaduni wa Kilelejimema kwani mwanamke hakuruhusiwa kumchinja kuku. Na hili linafanya msomaji kuelewa mengi kwani kupitia kwa mawazo ya Time tunaelewa kwamba mtoto hasa wa kike wa

kilelejimema hakuwa na uwezo wowote wa kujichagulia mchumba ila jukumu hili lilikuwa la wazazi wake. Pili, mgogoro huu wa kimawazo unazua taharuki ya kumfanya msomaji kutaka kujua ni jambo lipi lilitokea kiasi cha damu kumwagika nyingi na kumfanya Mzee Mkasi kuiogopa. Hili linatuelekeza kwenye masimulizi ya baadaye ya Mzee Mkasi ambayo yalielezea vita vilivyoleta uhasama miongoni mwa Wamalelejimema na wengi wao kuuawa kama vile nyanyake Nadia na wazazi wa Soud.

Aidha, migogoro ya mawazo inayomjia Soud kuhusu chuki iliyoko baina ya binadamu wote ulimwenguni bila ya kujali kabila rangi au nchi za wahusika pia inachangia kukamilisha mgogoro mkuu katika riwaya hii.

> Kitu gani kinachokufanya wewe ubakie nchi hii Soud? … kwa nini nisiishi humu mwetu? Kwa nini nisibaki Malelejimema?... Aaa hivyo ndivyo anavyoona yeye. Si lazima iwe wanavyoona wao. Aaa ati ndugu! Watu wanaotengana kwa masafa ya ardhi na masafa ya akili na fikra wanawezaje kuwa marafiki wa kweli? Watu wa nchi tofauti wanawezaje kuwa ndugu?”

Mgogoro huu unaendeleza uhasama uliokuwepo kati ya mataifa na ambao unaonekana kuwa mgumu kumalizwa. Mawazo mengine kinzani ya Soud yanayoendeleza ploti ya riwaya hii ni yale yanayohusu ndoa. Anaturejesha nyuma na kutueleza namna Bwan Sleyyum alivyomwita na kumweleza kuwa walipanga na wazazi wa Soud kuwa Soud amwoe Shafiqa. Bwan Sleyyum alitaka jambo hili litimie kwa kuwa hakutaka Shafiqa aolewe na mtu asiye wa rika au tabaka lake. Hili linadhihirisha kuendelezwa kwa mgogoro mkuu wa kitabaka ambao ndio unatawala riwaya nzima.

Mkamandume naye anawaza kuhusu zamani na sasa. Ingawa hataki kulinganisha hali ya zamani na sasa, anapata kila wakati akiwazia matukio ya zamani. Mgogoro huu wa mawazo unatumiwa kuendeleza ploti kwa kutudhihirishia mabadiliko ambayo yalikuwa

yametokea katika jamii hii (uk. 311). Mkamandume anajipata analinganisha hospitali ya sasa na ile ya zamani. Anashangaa ni kwa nini mambo yamebadilika sana na hali kuzidi kuzorota, kinyume cha matarajio yao walipopigania uhuru wa Malelejimema. Mwandishi anatumia mgogoro huu wa mawazo kutufafanulia matukio ya awali kuonyesha kwamba hata ingawa walioitwa wageni waliondolewa haielekei kwamba Wamalelejimema walikuwa karibu kupata nafuu (uk. 307).

Mawazo haya ya Mkamandume yanatuonyesha namna maendeleo katika nchi ya Malelejimema yalikuwa ya kubahatisha na hayangelinganishwa na yale yaliyopatikana Ulaya. Anashangaa ni kwa nini barabara na hata nyumba za kimalelejimema hazikukaribia kujengwa vizuri kama zile za Ulaya alizoziona kwenye sinema. Mwandishi anatumia mgogoro huu wa kimawazo kuendeleza maudhui ya uongozi mbaya na ukoloni mamboleo. Anataka kuendeleza ploti yake kwa kuonyesha kwamba hata ingawa Waafrika waliwapiga na kuwaondoa wakoloni ambao ndio walioonekana kuwakandamiza, hata na wao wenyewe wameshindwa kujitawala kwani mambo yamezidi kuzorota zaidi chini ya uongozi wao.

> Hata yeye asiyejua thamani ya nyumba alijua kwamba zile hazikuwa na sifa nzuri kama zile alizoziona yeye kwenye sinema na magazeti (uk 315).

Mawazo mengine ya Mkamandume yanayochangia kukamilisha mgogoro mkuu yanadhihirika anaposhangaa Soud alikuwa mtu wa aina gani ambaye alienda kumposa bintiye hata baada ya kujua kuwa Mkamandume ndiye aliyewaua wazazi wake (Soud). Anashangaa kwa nini anawaza kumhusu Soud ingawa hakutaka kumwazia. Anajiuliza kwa nini Soud alijitolea kumfanyia mema hata ingawa yeye alimdhulumu. Mgogoro huu

umejitokeza kuendeleza maudhui ya utu ambao unaenda sambamba na dhuluma zinazotokana na mgogoro wa kitabaka.

Aidha, mgogoro wa mawazo ya Mkamandume unaendeleza ploti kwa kuzua maudhui ya uozo katika jamii na chanzo chake ambacho ni pesa. Anashangaa kwa nini watu wameweka pesa mbele ya kila kitu; utu haupo tena, anaona pesa kuwa chanzo cha maovu yote yanayotokea Malelejimema. Anaona pesa kama nguvu inayoidhibiti jamii. Pesa imegeuza baadhi ya wanajamii kuwa miungu wadogo. Mkamandume anafikiria kwamba pesa ikitia kijiko hukoroga, ikitia mkono husokotasokota, ikitia kisu hukeketakeketa na hatimaye humtupia mtu kitanzi na kumyonga huku mnyongaji amejawa na raha na fahari. Mawazo haya yanatuonyesha uozo na uhaini unaojitokeza katika jamii ambao chanzo chake ni pesa (uk. 325). Hili bado linaturejesha tu katika ule utabaka uliokita mzizi katika jamii hii. Hata utabaka wenyewe chanzo chake ni pesa kwani matabaka yenyewe huwepo kutegemea uwezo wa wanajamii kifedha na kiuchumi. Kwa Mkamandume, tamaa ya pesa ndiyo huleta wizi na ufisadi kama ule wa bosi wake aliyekuwa kijana mdogo na mwenye suruali na shati moja tu na suruali yenyewe ilijaa viraka vitupu viatu vya ndara na mwili wake ng'onda. Amebadilika na kuwa tajiri mkubwa. Mkamandume anawaza:

> Mtazame leo alivyo, pesa imemgeuza kwa maana zote pesa inavyoweza kumgeuza mtu: roho, kiwiliwili na kivazi (uk 326).

Mbali na hayo, Mkamandume anawaza kuhusu msaadaa aliompa Tukaije wa kumtwika hando pale kisimani. Bi. Tukaije ambaye alikuwa mkewe jirani yake anamfanyia mzaha na kumtaka amtwike hando. Mkamandume anapofanya hivyo, Tukaije anaangua kicheko

na kuondoka. Bwan Rajab anatokea na kumsalimia Mkamandume ambaye hamjibu. Mgogoro huu mawazomi mwa Mkamandume unaonyosha kwamba uhusiano kati yake na mumewe Tukaije haukuwa mzuri. Mawazo haya pia yametumiwa na mwandishi kukuza ploti kwa kuzua maudhui ya chuki miongoni mwa wanajamii na ndoa za lazima na mapema kwani ni kupitia kwa mawazo haya ndipo tunapata kubainisha kwamba Tukaije aliolewa kwa lazima na mtu aliyemzidi umri kwa miaka mingi kiasi cha kuwa rika la babake (uk. 370).

Mwishoni mwa riwaya (uk. 462) mwandishi anatamatisha hadithi yake kwa kutudhihirishia kwamba migogoro ya kitabaka na matatizo yote katika jamii yanatokana na uongozi mbaya. Mawazo ya Mkamandume yanatuonyesha pande mbili za uongozi. Upande wa uongozi wa kidikteta uliowekwa kwenye msingi wa kuwanyanyasa wanyonge na upande mwingine wa uongozi mwema unaokita msingi wake kwenye utu, mapenzi, amani na utulivu kwa wananchi wote. Ni kwa msingi wa kutafuta upande huu mwema wa uongozi ndipo tunaona vita vikichacha na watu kujitokeza kupigana vita na kuleta uongozi uliowajali wananchi. Hawakujali risasi au kuuawa mradi wapate kilichowakwepa kwa miaka mingi – uongozi mwema. Ni katika harakati hizi ndipo Mkamandume na wananchi wengine walijitolea mhanga na kupoteza maisha yao walipopigwa risasi na kuuawa wakati wa maandamano.

Kwa kurejelea hii mifano yote, inabainika kwamba mgogoro mkuu ambao ulikuwa ni wa kitabaka usingeendelezwa bila ya kuwepo kwa migogoro ya kimawazo. Migogoro mbalimbali ya kimawazo imetumiwa na mwandishi kukuza maudhui mbalimbali ambayo

yameungana na kujenga ploti ya riwaya hii na hatimaye kukamilisha mgogoro huo wa kitabaka kama alivyokusudia mwandishi.

### 4.1.4 Mabadiliko ya migogoro.

Kipengele cha mabadilko ya migogoro katika nadharia ya Upembuzi kinasisitiza kwamba migogoro mipya huchipuza hata baada ya migogoro ya awali kutatuliwa. Kipengele hiki ni muhimu katika kuchanganua ploti ya riwaya hii kwani kinadhihirisha kwamba migogoro yote hutokana na baadhi ya migogoro ya awali ambayo ilitatuliwa. Mwandishi wa riwaya hii anaweka msingi wa ploti yake kwa kuzua mgogoro wa mawazo akilini mwa Mkamandume. Kupitia kwa mgogoro huo, anataka kutufafanulia asili ya Mkamandume na Malelejimea kwa jumla (uk. 2). Jambo hili ni muhimu kwa sababu ploti yake inaegemezwa katika mambo haya mawili yaani, asili ya Mkamandume na ile ya Malelejimema. Mawazo ya Mkamandume yanatufafanulia kwamba hapo awali palikuwa na jamii ya wavuvi waliokuja kuhamia Malelejimema na kuwakuta wakulima. Kwa maoni ya Mkamandume, dunia yote haina wenyeji. Anaweka msingi wa ploti kwa kutupa taharuki ya kujiuliza wenyeji halisi wa Malelejimema walikuwa akina nani? Jambo hili linaonyesha kwamba hata hapo awali palikuwa na migogoro miongoni mwa mababu zao kwani hakuna aliyeweza kudai kwamba yeye ni mwenyeji kindakindaki wa Malelejimema

Mkamandume anapogeuka na kutazama alikotoka nyuma anaona kwamba mgogoro ule wa awali ndio ulioleta uhasama miongoni mwa Wamalelejimema ingawa hakuna aliyekuwa na haki ya kudai umiliki wa Malelejimema. Analinganisha Malelejimema ya kale na Malelejimema ya sasa. Anaona tofauti kubwa. Hapo awali Malelejimema ilikuwa

na migogoro kati ya wenyeji na wakoloni. Hata hivyo, maisha hayakuwa magumu sana kwani mvua ilinyesha na wakapata chakula chao cha kila siku. Hata hivyo, wenyeji walipigana na wakoloni na kuwafukuza nchini mwao wakiwa na msimamo kwamba wageni waliwakandamiza wenyeji (uk. 6). Mgogoro huu unatatuliwa kwa vita na hatimaye wageni kuondoka Malelejimema. Baada ya wageni kuondoka, wenyeji wanachukua hatamu za uongozi na kufanya hali kuwa mbaya zaidi. Mgogoro mpya unazuka kati ya viongozi  na wananchi kwani unyanyasaji unatokea kuwa mbaya zaidi huku viongozi wa kimalelejimema wakifanya mengi maovu kuliko wale wa kikoloni. Mkamandume anawaza kwamba hapo zamani Wamalelejimema hawakulala na njaa wala kupita wakiomba ovyo ovyo. Lakini mambo yamebadilika kwani njaa imetawala na unyanyasaji umekuwa mbaya zaidi. Hii ndiyo maana anawaza:

> Mtindo ni ule ule wa waambangoma: kila mtu huvutia kwake. Lakini waambangoma wa sasa ni wa rangi ya aina nyingine. Weusi. Wao wanavuta bila hisia wala imani. Wanavuta kwa nguvu mno mpaka ngoma inararukiana (uk. 6)

Mawazo haya yanatudhihirishia kwamba ingawa mgogoro wa awali kati ya wenyeji na wakoloni ulitatuliwa kwa vita, mgogoro mwingine umechipuza miongoni mwa wenyeji na viongozi wao na huu unaonekana kuwa mbaya kuliko ule wa awali. Mgogoro huu wa mawazo ni muhimu katika kukuza ploti kwani unatupa msingi wa kuegemeza mgogoro wetu mkuu ambao ni wa kitabaka na chanzo cha unyanyasaji katika Malelejimema. Migogoro ya mawazo ya Mkamandume inatuchorea taswira ya mambo yalivyokuwa awali lakini yamekuja kubadilika. Katika mgogoro wa awali kati ya Mkoloni na Mwafrika matumaini yalikuwepo lakini hayapo katika mgogoro huu wa sasa. Anashangaa kwa nini mambo yameharibika kiasi hicho. Ndugu sasa wamekuwa maadui. Mkamandume anawaza:

> Kwa nini mambo yameharibika hivi? Nini kimetokea? Kwa nini ndugu au mwenzi sasa amekuwa adui? (uk. 20)

Mgogoro huu unatubainishia wazi namna mambo yalivyoharibika. Mabadiliko yamekuwa katika jamii hii lakini migogoro ya sasa imekuwa mibaya zaidi.

Migogoro ya mawazo ya Time nayo inaonyesha namna pamekuwa na mabadiliko katika jamii ya Wamalelejimema. Time anatatizika na kujiuliza kwa nini sasa pana mtu anayeogopa kuona damu ikitiririka ilhali jamii hii haikuogopa damu hapo awali. Babake (Mkamandume) hapo awali hakuogopa kuona damu ikimwagika na ndiyo maana yeye na marafiki zake kama Silimia waliwafyeka watu vichwa wakati wa vita vya kupigania uhuru. Wakati huo mgogoro uliokuwepo ulitatuliwa kwa vita. Aidha, mawazoni mwa Time panazuka mgogoro mwingine wa kitamaduni. Hapo awali, mwanamke hakuruhusiwa kumchinja kuku lakini Mzee Mkasi anamruhusu kumchinja kuku kwani alielewa kwamba mambo yalikiuwa yameanza kubadilika na hivyo basi hakuona ubaya wowote wa Time kumchinja kuku. Jambo hili linakinzana na utamaduni wa Malelejimema (uk. 167).

Kupitia kwa mawazo ya Soud tunaona migogoro ya kitabaka na chuki kati ya tabaka la chini na tabaka la juu. Kwa kuwa Soud alilelewa katika tabaka la juu, wazazi wake hawakumtaka awazoee wafanyakazi wao kama vile Mpikachai na Maliyatabu kwani waliamini kwamba wangemdhuru. Mgogoro huo unakoma baada ya wazazi wa Soud kuuawa na nchi kupata uhuru. Hata hivyo, mgogoro mpya wa kitabaka unajitokeza kwani tunamwona Mkamandume akikataa posa ya Soud kwa bintiye Time kwa msingi wa kitabaka. Haya yote yanakuja kubainika tu kupitia kwa migogoro ya mawazo ya Soud (uk. 218).

Mkamandume naye haishi kulinganisha mambo ya zamani na ya sasa. Analinganisha namna hospitali ilivyokuwa zamani na namna ilivyo sasa, anaona tofauti kubwa. Anasema kwamba hata ingawa wakati ule kulikuwa na ubaguzi wa rangi, hospitali za wakati huo zilikuwa safi, nidhamu kwa wafanyakazi na huruma ilikuwepo (uk. 307). Anawaza kwamba dawa zilikuwa zikitafuta wagonjwa siku zile na chakula nadhifu pia kilikuwepo. Hospitali za baada ya ukoloni nazo zilikuwa chafu na wagonjwa wanatusiwa. Dawa muhimu hazipo tena. Hii ndio maana Mkamandume anawaza:

> Kwa nini hospitali i hivi leo? Kwa nini i hivi na watu ni wale wale? Hapana, watu wamebadilika pia" (uk. 307)

Jambo hili linabainisha kwamba hapo awali wakati wa ukoloni Wamalelejimema walibaguliwa kitabaka lakini huduma zenyewe zilikuwepo. Mabadiliko yanapotokea katika jamii hii wanakuwa na migogoro miongoni mwao kiasi kwamba wanashindwa kufadhili huduma muhimu kama vile matibabu. Kupitia kwa haya, ploti ya riwaya hii inazidi kusukwa vyema kwani chanzo cha matatizo ya Malelejimema kinabainishwa kuwa ni uongozi mbaya miongoni mwa Wamalelejimema. Mkamandume anawazia zamani na sasa. Ingawa nafsi yake haitaki kulinganisha sasa na zamani, anajipata amewazia jambo hili sana. Anaona kwamba zamani kulikuwa na nafuu kuliko sasa. Sasa aliyoitazamia kuwa ingekuwa na furaha imekuwa kama miiba. Mwandishi anasema:

> Kwa nini zamani inarejea katika fikra zake katika wakati uliotazamiwa kuwa na nafuu. Kwa nini sasa anahisi kwamba zamani ilikuwa na nafuu kuliko sasa? (uk 311)

Wazo hili linatudhihirishia kwamba hapo awali kulikuwa na changamoto na migogoro miongoni mwao. Lakini baada ya kusuluhisha migogoro hiyo kwa njia ya vita, pamezuka

migogoro mingine mipya miongoni mwao na ambayo imekuwa migumu zaidi kutatua. Kwa njia hii, mwandishi amefaulu kukuza ploti yake vyema kwa kuzua taharuki na kuturudisha nyuma kutupa picha ya Malelejimema ilivyokuwa na jinsi ilivyo sasa na kwa nini mgogoro uliopo kwa sasa unaendelea hata kama Wamalelejimema walifikiria kwamba maisha yangekuwa nafuu baada ya kuwaondoa wakoloni.

### 4.2.0 Namna Migogoro ya Kisaikolojia Ilivyomwezesha Mwandishi wa Riwaya ya *Unaitwa Nani?* Kukuza ploti

Riwaya ya *Unaitwa nani?* (2020) ni riwaya yenye muundo wa pekee kwani inasheheni hadithi mbalimbali zenye uhusiano zilizotumiwa na mwandishi kueleza mgogoro uliopo kati ya mwanamume na mwanamke. Riwaya yenyewe ina sehemu mbili na wahusika wawili wakuu yaani mwanamke na mwanamume. Sehemu ya kwanza ina hadithi sita tofauti tofauti zilizotumiwa kuweka wazi dhuluma za wanaume dhidi ya wanawake. Sehemu ya pili ambayo inaangazia mwanamume nayo ina hadithi sita vilevile. Ingawa hadithi hizi zina wahusika mbalimbali, wahusika hawa wote wametumiwa kuwawakilisha wawili tu – mwanamke na mwanamume.

### 4.2.1 Muungano wa Mikinzano

Kipengele cha muungano mikinzano katika nadharia ya upembuzi kina umuhimu mkubwa sana katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2012) ikizingatiwa kwamba riwaya hii ina visa mbalimbali ambavyo vikiletwa pamoja vinasimulia kisa kimoja cha mwanamke na mwanamume. Ibainike kwamba visa hivi vimeunganishwa pamoja kusawiri kisa cha mwanamke na kile cha mwanamume. Katika riwaya hii, mgogoro mkuu unaotawala ni mgogoro kati ya mwanamke na mwanamume. Kwa miaka mingi, jamii nyingi za Kiafrika zimeshuhudia mgogoro huu, huku kila jinsia ikilaumu jinsia nyingine. Wanawake

wameshikilia kwamba wanaume wamekuwa wakiwadhulumu, kuwanyanyasa na kuwatesa na hivyo basi siyo watu wa kuaminiwa kwani hawana utu. Mwanamume naye anamwona mwanamke kama mtu aliyejaa hila, ujanja, tamaa na asiyeweza kuridhika kwa chochote. Sehemu ya kwanza inahusu mwanamke anayesimulia dhuluma nyingi anazopitia mikononi mwa mwanamume. Ni wazi kwamba visa vyote katika sehemu hii ya kwanza vinasimuliwa mawazoni mwa mwanamke aliyelazwa hospitalini akiwa mahututi na hawezi kutamka lolote ila neno mwanamke. Hivyo basi, masimulizi yote sita ni ya mawazoni.

Katika utangulizi wa sehemu ya kwanza, kuna mwanamke aliyelazwa hospitalini na amezingirwa na watu anaokisia kuwa madaktari na wauguzi wa jinsia ya kiume. Wote wanamdhihaki na kumuuliza alifanya nini kiasi cha kujikuta katika hali hiyo. Je, alimnyemelea mume wa mwenzake? Au alipatikana akifanya biashara haramu ya ngono? Au alimfanyia mumewe ujeuri ndipo akampiga kiasi hicho? Wanamlazimisha ataje jina lake na hata wanampa mifano ya majina wanayotaka ayataje: majina kama Jezebel (mwanamke laghai), Delila (mwanamke msaliti) au Pandora (mwanamke mwovu). Majina haya wanayoyapendekeza yanatuonyesha mtazamo wa mwanamume kumhusu mwanamke. Hii inaonyesha kwamba mwanamume ana mtazamo kuwa mwanamke ni msaliti, mwovu na mwenye hila. Mwanamke naye anataka atambuliwe kama mwanamke siyo kwa kutumia majina yasiyo na uzito wowote kwake. Tunapata mgogoro wa moja kwa moja mwanamke na mwanamume wanapobishana kuhusu jambo hili (uk. 13).

Mwanamume ana mtazamo hasi kumhusu mwanamke. Hii ndiyo maana mmoja wao anamuuliza daktari kwa nini imemchukua muda mrefu kuonyesha mabadiliko naye daktari anamjibu kwamba hivyo ndivyo walivyo wanawake kwani hata mifupa yao ni

dhaifu na minyonge (uk. 13). Wanaume wanashikilia kwamba hakuna mwanamke yeyote ambaye angeweza kutawala kwani ni wanyonge wasioweza kufanya maamuzi ya busara. Hata hivyo, mwanamke aliyelazwa ana mawazo tofauti kwani alitaka kuwakosoa na kuwaeleza kwamba kulikuwa na mwanamke wa Kichina kwa jina Wu Zeitan aliyekuwa mfalme baina ya mwaka 625-705 (uk. 31).

Mawazo haya yanaendelezwa katika hadithi ya kwanza ya Kasekesi. Kabla ya Kasekesi kuolewa, baba na mama wanamshauri lakini mashauri yao yanakinzana. Baba anamshauri kwamba asikubali kuolewa na mwanamume yeyote asiyejua kutunza utamaduni. Akubali aolewe na mwanamume wa kwao kwani ndio wanaojua kutunza utamaduni wao. Aidha anamweleza Kasekesi kwamba amridhishe kwa lolote atakalo kwani mume ndiye kiongozi wa nyumba. Mama naye anamshauri kuzingatia kinyume cha yale aliyofundisha baba. Mama anamweleza Kasekesi kwamba atafute mume asiye mtamaduni na asikubali kudhalilishwa kwa njia yoyote ile. Atafute mume atakayekuwa na utu na kumchukulia kama mwenzi wake bali sio kama bidhaa inayoweza kununuliwa sokoni.

Kasekesi anachanganyikiwa na mashauri haya kwani hajui afuate ya nani na anapoolewa na Agusto anashindwa na la kufanya. Maisha yao yanakuwa ya utulivu hadi Agusto anapofilisika, kuingilia ulevi na hatimaye kufa. Baada ya kufa kwa mumewe, jamaa za mume walimsingizia kwamba ndiye kamuua mumewe. Utamaduni unaotokea kumpendelea mwanamume unamwadhibu Kasekesi kiasi cha kuvuliwa nguo zake na kulazimishwa kutembea sokoni akiwa nusu uchi ili akiri kumuua mumewe. Hata hivyo anakataa na baada ya kuteswa sana anafukuzwa. Haya yote yanaonyesha uhusiano uliopo

baina ya mwananke na mwanamume. Uhusiano huu umejaa tuhuma, ila na ubabe kwa upande wa mwanamume.

Kisa cha Mwanamuka nacho chaonyesha namna mwanamke anavyobebeshwa mzigo mzito wa maisha. Kisa hiki kinachangia mgogoro mkuu kati ya mwanamke na mwanamume kwani kinabainisha namna mwanamume anapiga vita elimu ya mwanamke. Mhubiri, wanakijiji na hata mkuu wa wilaya hawakuona maana ya kumwelimisha mwanamke kwani angeishia kuolewa tu. Kwa hivyo, mamake Mwanamuka alihangaika mwenyewe mpaka naye mwishowe akachoka na kumwoza. Mwanamuka anakosana na mumewe aliyemwoa kijakazi wao kwa kuwa Mwanamuka alikuwa tasa. Kisa hiki kinaendeleza mgogoro kati ya mke na mume kwani matatizo katika ndoa kama kukosekana kwa mtoto mara nyingi ni mke huwa wa kulaumiwa.

Kisa cha Nyakor kinakoleza mgogoro ulioko kati ya mwanamke na mwanamume kwa kuweka wazi mambo matatu: utamaduni, ndoa na elimu. Nyakor ni mwanamke aliyeelimika lakini kila wakati walipokosana na mumewe alikimbilia kisingizio cha elimu kwamba Nyakor alimdharau kwa sababu ya kisomo chake. Mbali na hayo Nyakor anavumilia katika ndoa iliyojaa uhaini wa mumewe huku akitarajiwa kumtii kwa vyovyote vile. Mumewe anapofariki, utamaduni unamkandamiza na kumlazimisha kwamba lazima arithiwe; jambo analolikataa na hata kuishia kukosana na wazee. Mgogoro huo huo ndio unaoonekana katika hadithi za Zahra na Kamene na migogoro hii yote imetumiwa na mwandisha kutilia nguvu msimamo wa kike kwamba mwanamume ni katili na mbinafsi asiyejali maslahi ya mwanamke bali hujali maslahi yake mwenyewe.

Katika sehemu ya pili, tunapata visa vinavyohusu uhaini wanaofanyiwa wanaume na wanawake kwani inadhihirika kwamba wanawake ni wasaliti, wenye ila na waovu wasiowajali wanaume. Sehemu ya pili nayo inaaza kwa masimulizi ya mwanamume aliyelazwa hospitalini. Hana uwezo wa kuzungumza ila kutamka neno moja tu – mwanamume. Tunapewa taswira ya madaktari na wauguzi wa kike waliomzingira huku wakimdhihaki. Wanamuuliza jina lake na kusisitiza kwamba lazima alitaje. Hata hivyo, yeye anataja tu kwamba yeye ni mwanamume. Mtazamo wa mwanamke kumhusu mwanamume unadhihirika wakati wanapomwita Samsoni. Yanayodhihirika ni kwamba mwanamke amemchukulia mwanamume kama mtu mwenye fujo, muuaji, na mwenye kiburi. Hii ndiyo maana wanasema kwamba anatafuta nguzo za nyumba azisukume ziwaangukie kama alivyofanya Samsoni katika Biblia. Aidha wanawalinganisha wanaume na watoto na kwamba ndevu zao siyo ishara ya ukomavu wao kwani hata wakiwa watu wazima wangali wanataka wafanyiwe kila kitu kama watoto (uk. 114)

Kisa cha Mumbo nacho chaonyesha usaliti wa mwanake kwa mwanamume. Anaanza kisa chake kwa kusema kwamba alikuwa ameapa kutooa maishani. Haya yalitokana na ukweli kwamba wanawake wengi waliwahadaa waume zao na kula uroda na wamaume wengine nje ya ndoa. Kwanza, alimkuta mke wa ami yake akila uroda na Kasu (aliyekuwa mchimba vichuguu). Vilevile, anamkuta mhubiri (babake Kaminda) akila uroda na mke wa mzee mmoja wa kanisa usiku wa kuamkia mwaka mpya. Mumbo anapokuja kuoa, ndoa yake inakuwa nzuri hadi anapopoteza kazi. Hapo ndipo mkewe anaanza kumdharau na juhudi zake zote alizojaribu kufanya ili aikimu familia yake. Hatimaye, mkewe anatoroka na watoto wake wote na kumwachia upweke.

Kaminda Mwana-a-Pasta naye alihadaiwa na mkewe (Sasi) ambaye mwanzoni alijifanya anataka msaada kutoka kwa Kaminda kwani alikuwa amefungiwa nyumba. Kwa ujanja na hila alifaulu kumpumbaza Kaminda ambaye alikuja kumwoa. Baadaye Kaminda anakuja kugundua kwamba Sasi alikuwa na binti mkubwa wa kidato cha kwanza aliyemwacha kwa babu na nyanyake. Kaminda anapogundua siri hii na kumuuliza Sasi, anakuja juu na kutaka kumuua Kaminda ambaye kwa bahati nzuri anaponyoka na kutoroka

Kisa kingine ni kile cha Sir Pipo aliyehangaika kumwelimisha Lulu ambaye anakula njama na jamaa zake kumpunja Sir Pipo kwa kumtoza kiwango kikubwa cha mahari bila kujali kwamba ni Sir Pipo ndiye aliyemlipia karo. Baadaye Lulu anajiingiza katika chama cha akina mama na kusahau majukumu yake ya nyumbani kama mke. Hatimaye, anakuja kutalaki mume wake kwa kuwa alitaka uhuru wake wa kutembea popote alipotaka ulimwenguni. Kisa cha Purupesa nacho kilikuwa cha kusikitisha kwani alipomwoa Truvessa alifikiri alipata mke ambaye angemwondolea upweke lakini wanatokea kuzozana kila mara na usiku mmoja Purupesa alipoenda kustarehe katika kilabu cha *Avocado Wasp* ndipo alimpata mkewe akisakata densi akiwa uchi wa mnyama. Jambo hili linazua mgogoro miongoni mwao na kuwafanya wavunje ndoa yao.

Visa hivi vyote vinaunganishwa pamoja kuleta ithibati kwamba mwanamke ni mjanja, laghai na mwenye hila kila wakati. Hivyo basi visa hivi navyo vinakoleza mtazamo wa kiume wa kumtazama mwanamke kwa jicho la shauku.

### 4.2.2 Ukamilifu wa Mikinzano

Kipengele cha ukamilifu wa mikinzano katika nadharia ya upembuzi kinasisitiza kwamba migogoro mbalimbali hutegemeana na kukamilishana na hivyo basi hakuna mgogoro

unaoweza kusimama kivyake. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*, kuna migogoro ya aina mbalimbaliu aliyotumia mwandishi kukamilisha mgogoro wake mkuu ambao ni mgogoro kati ya mwanamke na mwanamume. Pia, haitasahaulika kwamba sehemu zote mbili zimejengwa katika mawazo ya watu wawili – mwanamke na mwanamume ambao wamelazwa hospitalini wakiwa mahututi na hawawezi kuzungumza. Hivyo basi, visa hivi vyote vinasimuliwa mawazoni mwao. Kuna migogoro mbalimbali iliyokuzwa ambayo inategemeana na kukamilishana ili kujenga mgogoro mkuu kati ya mwanamke na mwanamume. Migogoro hii ni kama vile migogoro kati ya wanandoa, migogoro ya kitamaduni, migogoro ya kitabaka miongoni mwa migogoro mingine. Migogoro hii yote imedokezwa katika visa vya wanawake na wanaume mbalimbali.

Katika hadithi ya Kasekesi mwandishi anasimulia mitazamo tofauti kuhusu ndoa kati ya mwanamume na mwanamke. Kupitia kwa ushauri wa baba na ule wa mama tunapata mitazamo tofauti za ndoa. Wanaume wakiwakilishwa na baba wanaamini kwamba ndoa inayofaulu ni ndoa ambayo mwanamke ananyenyekea na kumridhisha mumewe kwa kila kitu bila swali lolote. Aidha, wanaamini kwamba mtazamo wa kitamaduni unaompa mwanamume nafasi kubwa kuliko mwanamke katika ndoa ndio unaostahili kuhimizwa. Kwa upande mwingine, wanawake – wakiwakilishwa na mama – wana msimamo tofauti. Wanaamini kwamba ndoa nzuri ni ile iliyojengwa  kwenye msingi wa kuheshimiana bila kumdhalilisha mmoja na kumdharau kuwa jinsia dhaifu. Hii ndio sababu mama anamshauri Kasekesi kumtafuta mume atakayemheshimu kama kiumbe mwenye hisia bali siyo kama bidhaa inayostahilli kuuzwa sokoni. Migogoro hii ya kimawazo inajenga ploti na kukuza ule mgogoro wa kijinsia ambao ndio msingi wa riwaya yenyewe.

Hata baada ya Kasekesi kuolewa, anapata mume aliyekuwa na msimamo kama wa babake kwani anamkataza Kasekesi kufanya kazi yoyote na kumfanya kumtegemea mumewe kwa kila kitu. Nafasi ya utamaduni kumkandamiza mwanamke katika ndoa pia inajitokeza katika hadithi hii baada ya mumewe Kasekesi kufa. Wazee wanamdhulumu Kasekesi na kumlazimisha kulala katika chumba kimoja na maiti ya mumewe ili kuthibitisha kwamba hakuhusika au kusababisha kifo chake. Hata baada ya kumtesa sana wakitarajia angekufa, Kasekesi hafi, jambo linalowagadhabisha sana kwani walitarajia afe. Hatimaye, wanamfukuza kutoka katika kijiji hicho.

Mwanamuka naye ananyanyaswa na jamii kwa kuozwa akiwa angali mdogo. Anapoingia katika ndoa, migogoro kati yake na mumewe haikomi kiasi cha mume wake kumtunga mimba kijakazi wao na kumwoa kama mke mwenza wa Mwanamuka. Kisa cha Nyakor kinasheheni migogoro ya ndoa na ya kitamaduni ambayo inachangia na kukamilisha mgogoro wa kijinsia. Nyakor anapoolewa, ndoa yake haiishi msukosuko kwani mumewe kila mara alihisi kwamba anadharauliwa kwa sababu Nyakor anaona kwamba amesoma hadi chuo kikuu na kupata shahada. Mambo yanakuwa ni yayo hayo ya mivutano ya kila siku hadi mumewe Nyakor anapoaga dunia. Hapo ndipo utamaduni unapoingilia kati na kusisitiza kwamba Nyakor lazima arithiwe ingawa yeye anakataa katakata jambo hili.

Mambo ni yayo hayo katika kisa cha Kamene na Kaseli. Kamene anapoolewa na Lusweti, mumewe anabadilika ghafla na kuanza kumsikiliza mamake kuliko mkewe. Kinacholeta migogoro kati yao ni ile hali ya Lusweti kuthibitiwa na mamake kama kinyago. Chochote alichotaka mama, Lusweti alitenda bila kufikiria hata kama lingemdhuru mkewe. Uhusiano wao unakuwa mbaya kiasi cha wao kutengana. Hata baada ya kutengana Lusweti alifanya njama Kamene akashambuliwa alipojaribu kutafuta

haki za mtoto wao kutoka kwa Lusweti. Mamake Kaseli naye anadhulumiwa kwa kosa la Kaseli. Wakati wa tohara mangariba walishindwa kutekeleza kazi yao na hivyo Kaseli akalaumiwa. Ikabidi mamake atoroke naye ili kuepuka ghadhabu za babake Kaseli. Migogoro hii yote inachangia kuendeleza ploti ya riwaya hii na kukuza mgogoro wa kijinsia.

Katika sehemu ya pili mwandishi kupitia kwa mawazo ya mwanamume aliyelazwa hospitalini anadhihirisha dhuluma wanazotendewa wanaume katika ndoa. Visa hivi amevisimulia kupitia kwa: Mumbo, Kaminda Mwana-a-Pasta, Wamae, Sir Pipo, Purupesa na Kasina Usina Sini. Kisa cha Mumbo kinaanza anapoapa kwamba asingeoa maishani. Hii ni kwa sababu alikuwa ameshuhudia namna wake za watu walivyokuwa wakila uroda nje ya ndoa huku wanawapumbaza waume zao kwamba walikuwa waaminifu. Aliwapata Daphina (mke wa ami yake) na Kasu wakila uroda na vilevile mke wa mzee wa kanisa akila uroda na mhubiri kichakani usiku wa mkesha wa mwaka mpya. Baadaye Mumbo anapooa, mkewe anakuja kumhangaisha na hatimaye kutoroka na watoto  Mumbo alipopoteza kazi.

Kaminda naye alihadaiwa na Sasi ambaye alimdanganya akajipata katika ndoa bila ya yeye mwenyewe kupanga. Baada ya kuoana ndipo Kaminda anagundua kwamba Sasi alikuwa na binti mkubwa ambaye alikuwa katika kidato cha kwanza. Kaminda anapomuuliza, Sasi anapanga njama ya kumuua lakini Kaminda anaponea chupuchupu na kutoroka kutoka kwake na yale mavazi tu aliyokuwa amevaa mwilini. Mambo yanakuwa yayo hayo ya kusalitiwa katika visa vya Wamae, Sir Pipo na Kasina ambao wote pia

wanatokea kusalitiwa na wanawake na kuachwa wakihangaika. Hata katika kisa cha Purupesa aliishia kuangamia.

Kwa jumla visa hivi ndivyo vilipojumuishwa viliunda riwaya ya *Unaitwa Nani?* Anwani hii ndio msingi wa mgogoro wa kijinsia ambao unasisitizwa katika riwaya nzima. Kila jinsia haielewi jinsia nyngine. Mwanamume hamwelewi mwanamke kabisa na ndiyo maana anag'ang'ania kumuuliza jina lake nani. Kwa kawaida jamii imemwelewa mwanamke kijuujuu tu bali siyo kwa undani. Mwanamke anataka jamii imwelewe kwa kina; matatizo yake, hofu yake na umuhimu wake ila kinachojulikana kwa jamii ni jina tu la nje ambalo mara nyingi hupotosha. Hivyo pia ndivyo ilivyo na jinsia ya kiume ambayo haieleweki na jinsia ya kike. Hiki ndicho chanzo cha mgogoro wa kijinsia katika riwaya ya unaitwa nani? Mgogoro huu umeweza kufanikishwa vyema zaidi kupitia kwa migogoro ya kimawazo.

**4.3.0 Hitimisho**

Sura hii imeweza kudhihirisha kwamba migogoro ya kimawazo iliwawezesha waandishi wa riwaya za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012) kusuka ploti zao kwa njia zinazofaulisha masimulizi yao. Mhimili wa tatu wa nadharia ya Upembuzi ambao ulitumiwa kuchanganua data katika sura hii uliundwa kwa vipengele vitatu ambavyo ni: muungano wa mikinzano, ukamilifu wa mikinzano na mabadiliko ya migogoro. Vipengele hivi vilichunguzwa moja kwa moja na kutumiwa kubainisha umuhimu wa mgogoro wa kimawazo katika ukuzaji wa riwaya teule. Hivyo basi, ni sahihi kusema kwamba migogoro ya kimawazo ina umuhimu mkubwa katika kuendeleza ploti ya riwaya yoyote kwani migogoro mingine yote huchipuka kutokaa na ile ya ndani kwa

ndani. Sura inayofuata (ya tano) ilishughulia: matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1. Muhtasari

Tasnifu hii imehakiki namna migogoro ya kimawazo ilivyowawezesha waandishi wa riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?* kusuka ploti zao huku wakiwakuza wahusika wao. Aidha, maudhui yalihakikiwa na kubainisha kwamba migogoro ya kimawazo ndiyo iliyojenga takriban maudhui yote katika riwaya hizi.

Sura ya kwanza ilibainisha usuli wa utafiti na kuonyesha kuwa pana pengo kuhusu migogoro ya kimawazo kwani migogoro iliyowahi kushughulikiwa ilihusu utamaduni, utabaka, jinsia na kadhalika bila kubainisha kwamba chanzo cha migogoro hii yote ilikuwa migogoro ya kimawazo. Migogoro iliyowahi kutafitiwa ilihusu tamthilia bali si riwaya. Aidha, sura hiyo iliweka wazi malengo matatu ya utafiti. Sura ya kwanza pia iliweka mipaka ya utafiti na kuangazia yaliyoandikwa na waandishi wa awali kuhusu migogoro huku ikiweka misingi ya nadharia. Nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ni nadharia ya Upembuzi.

Sura ya pili ilitoa muhtasari wa riwaya za *Mkamandume* (2013) Said A. Mohamed na *Unaitwa Nani?* (2012) Wamitila K. na kubainisha namna migogoro ya kisaikolojia ilivyowawezesha waandishi wa riwaya hizi kukuza maudhui mbalimbali. Baadhi ya maudhui yaliyokuzwa kupitia kwa migogoro ya kimawazo yalikuwa: uharibifu wa mazingira, dhuluma dhidhi ya raia, ukiukaji wa haki za watoto, unyanyasaji wa kijinsia, umaskini miongoni mwa mengine.

Sura ya tatu iliangazia namna migogoro ya kimawazo ilivyowawezesha waandishi wa riwaya hizi kuwakuza wahusika wao. Wahusika wenye umuhimu mkubwa kwenye riwaya ndio walioteuliwa na kuchanganuliwa. Woloch (2003) anasisitiza kwamba wahusika wote katika kazi ya fasihi ni muhimu ingawa kuna baadhi ya wahusika wajenzi ambao majukumu yao huingiliana kiasi cha kwamba kuwachanganua baadhiyao kunaweza kuwawakilisha waliosalia. Ni kwa msingi huu ndipo sura hii iliwateua baadhi ya wahusika ambao waliwawakilisha wengine. Wahusika wakuu nao walichanganuliwa kwa msingi wa kutekeleza majukumu makuu kiasi cha kwamba kuwapuuza kungeweza kuathiri utafit huu au hata kuufanya kuwa chapwa.

Sura ya nne ilichanganua namna migogoro ya kimawazo ilivyowasaidia waandishi wa riwaya za *Unaitwa Nani?* na *Mkamandume* kusuka ploti zao kwa njia iliyozua taharuki na kuwafanya wasomaji wao kusoma riwaya hizi mpaka mwisho licha ya kwamba riwaya ya *Mkamandume* ndiyo riwaya ndefu zaidi ya Kiswahili iliyowahi kuandikwa katika karne ya ishirini na moja. Riwaya ya *Unaitwa Nani?* nayo ilizua mtindo wa kipekee na kueleza visa vingi vyenye uhusiano kwa lengo la kukamilisha dhamira moja.

### 5.2. Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu ambayo yalikuwa ni:

1. Kubainisha jinsi migogoro ya kimawazo ilivyoweza kuzua dhamira zinazopingana. Lengo hili lilishughulikiwa katika sura ya pili kwa kuzingatia mhimili wa kwanza wa nadharia ya Upembuzi unaosisitiza kwamba migogoro hujitokeza mara kwa mara katika kila jamii.

2. Kufafanua namna migogoro ya kimawazo ilivyowawezesha waandishi kuwakuza wahusika katika riwaya za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012). Lengo hili lilichunguzwa katika sura ya tatu kwa kutumia mhimili wa pili wa nadharia ya Upembuzi ambao ulisisitiza kwamba kila mgogoro una upekee wake unaoutofautisha na migogoro mingine.

3. Kuchunguza namna migogoro ya kisaikolojia ilivyowawezesha waandishi kukuza riwaya zao kimsuko na kuzifanya kuwa na mshikamano mwema katika ploti zao. Lengo hili lilichunguzwa katika sura ya nne kwa kuzingatia mhimili wa tatu wa nadharia ya Upembuzi. Mhimili huu uliangazia vipengele vitatu ambavyo ni:
    i. Muungano wa mikinzano – katika kila migogoro kuna migogoro mingine midogo midogo ambayo lazima iungane ili kufanikisha mgogoro mkuu.
    ii. Ukamilifu wa mikinzano – migogoro mbalimbali hutegemeana na kukamilishana kiasi cha kuwa na mtagusano na mwingiliano wa vipengele mbalimbali vya migogoro hiyo ili migogoro yenyewe iweze kusimama
    iii. Mabadiliko ya migogoro – migogoro mipya hutokea kila mara hata baada ya migogoro ya awali kutatuliwa.

Kwa kuzingatia malengo haya matatu, matokeo ya utafiti huu yalibainisha mambo yafuatayo:

a) Kwanza, migogoro ya kimawazo kati ya wahusika mbalimbali ni kipengele muhimu ambacho huwawezesha waandishi kujenga maudhui yao mbalimbali. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mkamandume* dhamira ya mwandishi ilikuwa kuonyesha kwamba chanzo cha matatizo yote katika jamii ni uongozi mbaya na ubinafsi. Mwandishi

ameweza kufikia dhamira hii kwa kujumuisha migogoro mbalimbali ya kimawazo katika kazi yake ambayo ilimwezesha kuzua maudhui kama vile tamaa, unyanyasaji, kukata tamaa, dhuluma dhidi ya wananchi miongoni mwa mengine. Aidha, katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* ukweli wa mhimili wa nadharia ya Upembuzi unaosisitiza ubia wa migogoro katika jamii ulibainika kwani kuna jamii mbalimbali zilizozungumziwa na masuala mbalimbali kushughulikiwa vilivyo hasa ndoa na dhuluma dhidi ya wanawake. Haya yote yamefungamana vizuri kwa kuegemezwa kwenye migogoro ya kimawazo inayojitokeza katika masimulizi yenyewe.

b) Pili, migogoro ya kisaikolojia ndiyo iliyowawezesha waandishi wa riwaya hizi mbili kuwakuza wahusika wao vyema. Kupitia kwa migogoro hiyo ya mawazo, ndipo waandishi wa riwaya hizi waliweza kutimiza malengo yao na kupitisha ujumbe waliokusudia kuwapa wasomaji wao. Kwa kuwakuza wahusika vyema, ujumbe wao uliwasilishwa kwa njia inayostahili. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba migogoro ya kimawazo ni kipengele muhimu na hakiwezi kupuuzwa katika kuwakuza wahusika kwenye riwaya ya Kiswahili katika karne ya ishirini na moja.

c) Migogoro ya kimawazo iliwawezesha waandishi wa riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?* kusuka ploti zao kwa weledi unaostahili. Ni wazi kwamba ploti husheheni mambo mengi ili iweze kukamilika. Kwa mujibu wa Brook (1992), ili mwandishi aweze kuafikia dhamira yake, lazima afinyange kazi yake vizuri ili kazi hiyo iwe kamilifu. Kwa sababu hii, mwandishi hulazimika kufinyanga fani na maudhui kwa ufundi ili kazi yenyewe ikamilike. Katika riwaya ya *Mkamandume*, mwandishi alidhihirisha namna migogoro ya kisaikolojia ilivyojitokeza miongoni

mwa wahusika mbalimbali na jinsi ilivyoibua maudhui tofauti tofauti ambayo ndiyo aliyatumia kuendeleza ploti yake.

d) Vilevile, kwa kuzingatia vipengele vitatu vya mhimili wa tatu wa nadharia ya upembuzi, mambo matatu yaliweza kudhihirika:

i. Kipengele cha muungano wa mikinzano kilikuwa muhimu sana katika kuendeleza ploti. Katika riwaya ya *Mkamandume*, wahusika wengi walikuwa na migogoro ya kimawazo ambayo ilihusiana, kuathiriana na hata kuishia kukamilisha maudhui mbalimbali. wahusika wenye mawazo kinzani walikuwa: Mkamandume, Bwan Aziz Kindy, Mzee Mkasi, Bosi, Bi. Tufaa, Time, Nadia, Soud na kadhalika. Hali kadhalika katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* palikuwa na mawazo kinzani kati ya mwanamume na mwanamke. Haya mawazo yalikamilika tu kwa sababu ya kuunganisha migogoro mbalimbali ya kimawazo ya wahusika.

ii. Kipengele cha ukamilifu wa muungano wa migogoro nacho kilijitokeza katika riwaya ya *Mkamandume* kwani migogoro ya kimawazo ya wahusika mbalimbali ilitumika kukamilisha mgogoro mkuu ambao ulikuwa wa kitabaka. Migogoro mbalimbali ya kimawazo ilitumiwa na mwandishi kukuza maudhui mbalimbali ambayo imeungana kujenga ploti ya riwaya na hatimaye kukamilisha mgogoro huo wa kitabaka. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*, kuna migogoro ya aina mbalimbali iliyotumiwa kukamilisha mgogoro mkuu ambao ulikuwa wa kijinsia. Itakumbukwa kwamba riwaya hii ilijengwa katika mawazo ya watu wawili – mwanamume na mwanamke waliokuwa na mawazo kinzani. Kupitia kwa mikinzano ya mawazo ya wahusika mbalimbali, mwandishi alifaulu kufikia

dhamira yake. Mawazo hayo yalikamilishana na kukuza mgogoro wa kijinsia kama alivyokusudia mwandishi.

iii. Kipengele cha mabadiliko ya migogoro kilichangia kukamilisha dhamira za riwaya hizi. Kipengele hiki kilitudhihirishia kwamba mgogoro wa kimawazo hutokana na baadhi ya migogoro ya awali ambayo ilitatuliwa na migogoro mingine kuchipuka. Waandishi hawa waliweka misingi ya ploti zao kwa kuzua migogogro ya kimawazo akilini mwa baadhi ya wahusika na kutuwekea wazi asili ya migogoro yenyewe katika riwaya hizi.

**5.3 Mchango wa Utafiti.**

Utafiti huu umedhihirisha kwamba mgogoro wa kimawazo ni kipengele muhimu katika kukuza maudhui mbalimbali, kuwasawiri wahusika na kujenga ploti ya riwaya. Mwanzoni mwa utafiti, iibainika kwamba hakuna utafiti wa kina uliowahi kufanywa kuhusu migogoro ya kisaikolojia. Watafiti wengi waliowahi kushughulikia riwaya kama vile Lomatoro (2014) walishughulikia viwango vya uhalisi na ubunifu katika riwaya teule za Kiswahili kushughulikia suala la migogoro kwa jumla kama mojawapo ya mada ndogo. Hivyo basi, utafiti huu uliziba pengo hili kwa kuchanganua riwaya teule za *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012). Matokeo ya utafiti huu yamehitimisha kwamba migogoro ya kimawazo huathiri uhusiano wa wahusika wa riwaya za Kiswahili na jamii zao na hivyo kuathiri maingiliano ya wahusika hao na jamii hizo.

Aidha, utafiti huu umeweza kubainisha kwamba migogoro ya kimawazo ndiyo huzua migogoro ya aina nyingine katika riwaya hizi na kuwawezesha waandishi kusuka ploti zao kama walivyokusudia. Migogoro ya kimawazo miongoni mwa wahusika mbalimbali

katika riwaya hizi mbili; *Mkamandume* (2013) na *Unaitwa Nani?* (2012) ilichunguzwa na ikadhihirika kwamba ukuzaji wa maudhui, wahusika na ploti kunategemea migogoro ya mawazo kwa kiwango kikubwa. Ni vigumu kukuza kipengele kingine chochote cha kukamilisha riwaya ya Kiswahili bila kuwepo kwa migogoro ya mawazo.

Kitaaluma, utafiti huu umechangia kubainisha namna migogoro ya kisaikolojia inaweza kutumiwa kuimarisha uandishi wa riwaya katika karne ya ishirini na moja ikizingatiwa kwamba wahusika wa sasa ni changamano na wamekaribia binadamu halisi.

### 5.4. Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto ya gharama ya juu ya utafiti kuliko ilivyokadiriwa. Haya yalitokea kwa sababu ya kupanda kwa gharama ya huduma za mitandao pamoja na uchapishaji wa zaidi ya nakala mbili za kila sura kwa wakati fulani. Jambo hili lilisababisha kucheleweshwa kwa utafiti kwa muda wa mwaka mmoja kwani matokeo ya utafiti wenyewe yalitarajiwa mwazoni mwa mwaka wa 2019. Mbali na hayo baadhi ya vitabu vilivyotumiwa vilikuwa ghali mno.

### 5.5. Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kuchunguza namna migogoro ya kimawazo ilivyoathiri ukuzaji wa maudhui, wahusika, na ploti kwenye riwaya mbili za Kiswahili – *Mkamandume* na *Unaitwa Nani?* kwa mujibu wa nadharia ya Upembuzi. Riwaya hizi zilifaa katika utafiti huu kwani ziliandikwa katika karne ya ishirini na moja. Utafiti huu unapendekeza kwamba utafiti zaidi unaweza kufanya kuhusu yafuatayo:

Ni muhimu kuchunguza namna migogoro ya mawazo huathiri fani na maudhui katika tamthilia kwani utafiti wa awali ambao umewahi kufanywa ni ule unaohusu migogoro ya

aina nyinginezo bila kuzingatia kwamba migogoro mingine yote huwa na asili yao katika migogoro ya kimawazo.

Pana haja pia ya kufanya utafiti kuhusu nafasi ya migogoro ya mawazo katika hadithi fupi za Kiswahili ikizingatiwa kwamba wahusika wanaopatikana katika hadithi fupi za kisasa huwa changamano na hukaribiana zaidi na binadamu halisi ambaye huwa na mawazo changamano.

Tatu, utafiti zaidi kuhusu migogoro ya mawazo katika riwaya ya Kiswahili unaweza kufanywa kwa msingi wa nadharia mbalimbali kama vile nadharia ya Saikolojia Changanuzi ya Sigmud Freud. Jambo hili litaimarisha uelewa wa jamii kuhusu fasihi andishi ya Kiswahili.

# MAREJELEO

Brook, P. (1992). *Reading for the Plot: Design an Intention in Narrative.* Cambridge: Harvard University Press.

Dibell, A. (1988). *Plot: Elements of Fiction Writing.* Cincinnati: Writers Digest Books.

DiBattista, M. (2010). *Novel Characters*. Chichester: Wiley-Blackwell Publication.

DiYanni, R. (2004). *Approaches to Fiction, Poetry and Drama.* New York: McGraw-Hill Publishers.

Eagleton, T. (1976). *Marxism and Literary Criticism of California*. California: Harper and Row Puplishers.

Eldridge, R. (2008). *Literature, Life and Modernity*. New York: Columbia University Press.

Eleanor, K. (2012). *The Dark Precursor: Dialectic*, *Structure Being.* Baltimore: The Johns Hopkins University Press.

Fanon, F. (1952). *Black Skin White Masks*. Paris: Edition de Seuli.

________(1977). *The Wretched of the Earth*. New York: Grove Press.

Firth D. G. na Lindsay W. (Ed.S)(2016) *Exploring Old Testament Wisdom: Literature and Themes.* London: Inter–Versity Press.

Goldmann, L. (1975). *Towards A Sociology of The Novel*. London: Tavistock Publications Limited.

Kahara, I (2011). "Tamthilia kama Utendi: Uchanganuzi Linganishi wa Tamthilia za *Kinjeketile* na *Mzalendo Kimathi*." Chuo Kikuu Cha Kenyatta,

Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa)

Lomatoro, P.J, (2014). "Viwango vya uhalisi na ubunifu katika riwaya teule za Kiswahili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa)

Matei A. (2011). *Fani Ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Oxford University Press

Mavisi, R. (2007)."Usawiri wa Wahusika wa kike katika kazi za Zainabu Burhani." Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa).

Mayaka, G. (1991). "Ukengeushi wa Wasomi katika Riwaya Za Euphrase Kezilahabi" Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa).

McClinton-Temple, J. (2011) (Editor) *Encyplopedia of Themes in Literature*. New York: Infobase publishing.

Morreti, F. (2006) (Editor) *The Novel volume 2. Forms and Themes*. Princetone: Princetone University Press.

Morroe, B. (1977). *Real and Imagined Worlds.*Cambridge: Harvard University Press.

Muindi, A (1990)."Usawiri wa Wahusika Makahaba Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed." Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa).

Mungah, C. (1999). "Dhana ya Maisha Katika Novela Mbili za Euphrase Kezilahabi: *Nagona*na *Mzingile."* Chuo Kikuu Cha Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa).

Murray, T. (2003). *Blending qualitative and quatitative research methods in thesis and dissertations*. California: Corwin Press, Inc

Murithi, J. (2002). “Usemezano Katika Tamthilia ya Kiswahili.” Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa).

Nanjala, C. (2015) “Mgongano wa tamaduni katika hadithi fupi za Kiswahili” Chuo Kikuu Cha Kenyatta (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa)

Nazareth, P. (1972). *Literature and Society in Modern Africa.*Nairobi: Kenya Literature Buraeu.

Ngugi, T. (1987). *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Harare: Zimbabwe Publishing House.

Said, A. (2008). *Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili* Katika Ogechi, N., Shitemi, N., na Simala, K. (Wah.) *Nadharia katika taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. (Uk. 3 – 7) Edoret, Kenya: Moi university Press.

Said, A. (2013). *Mkamandume*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Sayers, S. (1985). *Reality and Reason: Dialectic and the Theory of Knowledge*. New York: Basil Blackwell Ltd.

Soo, F. (1981). *Mao Tse–Tung’s Theory of Dialectic.* London: D. Reidel Publishing Company

Stern, R. (2005). “Peirce on Hegel: Nominalist or Realist? *Transactions of the Charles S.s PeirceSociety,”* Vol. 41, No. 1 (Winter, 2005), uk. 65-99.

Temmerman, K. (2014). Crafting *Characters: Heroes and Heroines in the Ancient Greek Novel*. Oxford: Oxford University Press.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswhili Sanifu*. Dar es salaam: O.U.P East Africa Limited

Vaughan, C.J. (1973). *Soviet Socialist Realism: Origin and Theory*. London: The Macmillan LTD,

Wafula, C. N. (2015).“Mgongano wa Tamaduni katika Hadithi Fupi.” Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa).

Wafula, R. M. (1999).*Uhakiki wa tamthilia: Historia na maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M. na Kimani, N. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi:The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2002).*Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publshers Ltd.

____________(2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K.W. (2012). *Unaitwa Nani?* Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd.

Williams D. (2014). *Reasons Behind Your Character's Actions, What Would a Character Do If....Get to Know Your Characters.* Princeton: University Press New Jersey

Woloch, A. (2003). *Minor Characters and The Space of The Protagonist in The Novel*. Princeton: University Press New Jersey

## KIAMBATISHO 1

## KALENDA YA KAZI

| | |
|---|---|
| JANUARI – APRILI 2017 | Kutafuta mada ya utafiti na kuandika makala dhanishi |
| MEI 2017 – APRILI 2018 | Kuandika rasimu ya kwanza ya pendekezo la utafiti |
| MEI 2018 – NOVEMBA 2018 | Kuandika rasimu ya pili ya pendekezo la utafiti |
| NOVEMBA – DESEMBA 2018 | Kuandika rasimu ya mwisho ya pendekezo la utafiti |
| FEBRUARI 2019 | Kutetea pendekezo la utafiti |
| MACHI 2019 | Kufanya marekebisho yaliyopendekezwa wakati wa utetezi |
| APRILI 2019 – JUNI 2020 | Kuandika sura za pili, tatu, nne na tano za tasnifu |
| JULAI 2020 | Kuwasilisha matokeo ya utafiti kwa wasimamizi |
| AGOSTI 2020 | Kufanyia tasnifu marekebisho |
| SEPTEMBA 2020 | Kuwasilisha rasimu ya pili kwa wasimamizi |
| NOVEMBA 2020 | Kuwasilisha rasimu ya mwisho kwa wasimamizi |
| DESEMBA 2020 | Kufuzu |

## KIAMBATISHO CHA 2

## GHARAMA YA UTAFITI

| | |
|---|---|
| 1. GHARAMA ZA HUDUMA ZA MTANDAO | 40,000 |
| 2. VITABU NA MAJARIDA | 60,000 |
| 3. UCHAPISHAJI WA TASNIFU | 50,000 |
| 4. USAFIRI | 30,000 |
| 5. GHARAMA ZA ZIADA | 20,000 |
| JUMLA | 200,000 |